ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	**-**	**SPIKA**
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki

11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera

22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa

39. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake

80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 23 Februari, 2018

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Bahati Khamis Kombo (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuweka hati mezani Ripoti ya Kamati ya Bajeti ya Mwaka 2017/2018. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 53

Mpango wa Huduma kwa Wanaoishi katika Mazingira Magumu

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa programu ndogo ya utaratibu wa huduma za uhifadhi wa jamii ilipokea maombi 19 mapya kwa wafanyakazi walioumia kazini Unguja na Pemba na kwa sababu dhamira halisi ya programu ni kutoa huduma kwa makundi yanayoishi katika mazingira magumu.

(a) Je, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni makundi mangapi ya watu wanaoishi katika mazingira magumu yaliyofaidika na mpango na ni kiasi gani cha fedha kilitumika kusaidia makundi hayo.

(b) Je, maombi 19 mapya yaliyopokelewa mwaka 2016/2017 wizara imeshalipa kiasi gani cha fedha kwa waathirika hao na ni waathirika wangapi ambao hadi sasa hawajalipwa.

(c) Kwa kuwa hadi kufikia mwezi Mei, 2017 kulikuwa na deni la zamani la Tshs. 30,607,830/= ambalo lilikuwa ni bakaa ya deni la waathirika wa ajali kazini waliotangulia. Je, tayari wizara imeshalilipa. Kama bado ni lini deni hilo litalipwa kwa waathirika hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza naomba niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma ambaye ameweza kutupa pumzi na tukaweza kuhudhuria hapa katika Baraza lako tukufu tukiwa wenye afya njema.

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu sasa kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 53 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 wizara imezisaidia familia 215 ambapo 92 ni za Unguja na 58 ni za Pemba. Familia za Makundeni 55 na wazazi 10 wenye mapacha 3 (3 Unguja na 7 Pemba). Fedha iliyotumika ni Shilingi Milioni Hamsini na Moja Laki Nane Thelathini Elfu (51,830,000/=) kati ya hizo Shilingi Milioni Ishirini na Moja na Ishirini Elfu kwa Unguja na shilingi Milioni Thalathini, Laki Nane na Elfu Kumi kwa Pemba.

(b) Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 wizara imeshalipa fidia jumla ya Shilingi Milioni Ishirini na Mbili Laki Sita Tisini na Nane Elfu Mia Tisa na Kumi (22,698,910/=) Unguja na Shilingi Milioni Tisa Laki Sita Tisini na Nane Elfu Mia Tisa na Kumi, na Pemba ni shilingi Milioni Kumi na Tatu (13,000,000/=) kwa wafanyakazi 22 (Unguja 6 na Pemba 16) waliopatwa na ajali kazini. Hadi sasa waathirika ambao hawajalipwa ni 11 (Unguja na 6 na Pemba ni 5).

(c) Mhe. Mwenyekiti, wizara ilifanikiwa kupunguza deni lililokuwepo hapo awali. Deni lililokuwepo hadi mwezi Disemba, 2017 ni Shilingi Milioni Kumi na Sita Laki Mbili Themanini na Moja Elfu Mia Nane na Kumi na Tatu (16,281,813/=); Unguja Shilingi Milioni Kumi na Tatu Arobaini na Mbili Elfu Mia Sita na Thelathini na Moja (13,042,631/= na Pemba Milioni Tatu Laki Mbili Arobaini Elfu Mia Moja Thamanini na Mbili (3,240,182/=). Kwa mujibu wa fedha za matumizi tulivyopanga na uingizaji wa fedha ikiwa utakwenda kama tulivyopanga tunatarajia kwamba deni hili tutalilipa katika mwaka wa fedha huu 2017/2018. Ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri lakini nina swali dogo la nyongeza.

a) Kwa kuwa wizara imeshapanga kupunguza hilo deni la zamani na inaendelea kulipa deni jipya kwa waathirika hao. Je, wizara haioni ni vyema kumalizia deni la zamani

kwanza na baadae kuendelea kulipa deni jipya, kuliko kulipa deni jipya kabla ya kumalizia lile la zamani.

b) Je, ni waathirika wangapi wanaohusika na deni hilo la zamani ambalo limebakia. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Niseme kwanza Mhe. Mwakilishi ushauri wako tumeuchukua na *inshaallah* tutaweza kulipa lile deni la nyuma na baadae waendelee hawa wapya. Kuhusiana na deni hilo watu waliobakia ni watu wanane (8), ikiwa Unguja ni wanne (4) na Pemba ni wanne (4). Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa na mimi nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nilimsikiliza kwa makini wakati akijibu swali, alisema kwamba kuna wadeni ambao walibakia hawa wanane wakiwa wanne ni Unguja na wanne ni Pemba. Je, ni sababu gani zilizopelekea watu hawa wakaweza kubakia na wenzao wakaweza kupata ile pesa ambayo ilikuwa kwa kipindi hicho na wao walihitajika kwamba wapate lakini ikawa ni tatizo mpaka kufikia wawekwe mara ya pili. Je, hatuoni kwamba kutokupatikana kwa pesa hii kurudisha nyuma pengine juhudi na ile azma ya serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa

ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, sio lengo letu wala dhamira yetu wizara kutobaki kuwalipa hawa, isipokuwa sababu kuu inatokana na kutokulipwa hawa ni uingizaji wa pesa tulizokuwa nazo. Lakini kama nilivyoahidi katika swali langu lililopita kwamba *inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu watu hawa waliobakia tunatarajia kuwalipa ndani ya mwezi huu kabla ya bajeti inayotarajiwa kufika. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 61

Changamoto Zinazoikabili Skuli ya Chekechea ya Madungu

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Skuli ya Chekechea ya Madungu ambayo ina muda zaidi ya miaka 30 toka ilipojengwa, ina changamoto nyingi ikiwemo ubovu wa majengo yake na idadi kubwa sana ya wanafunzi katika madarasa.

(a) Je, serikali inazijua changamoto zilizomo katika skuli hiyo.

(b) Je, serikali ina mpango gani kuhusu skuli hiyo katika kuongeza madarasa au kujenga ya ghorofa.

(c) Je, serikali isipochukua hatua za haraka na kudhibiti majengo hayo, si utakuwa ule msemo “usipoziba ufa utajenga ukuta”.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 61 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

a) Napenda nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kuwa serikali inazijua changamoto za skuli ya maandalizi ya Madungu.

b) Serikali ina mpango wa kujenga skuli za ghorofa za maandalizi, kwani bado tunaamini kuwa skuli za chini zisizokuwa za ghorofa bado ni salama zaidi kwa mazingira ya watoto wa chekechea kujifunza kulingana na umri wao. Eneo la skuli ya Madungu Chekechea ni kidogo kwa kuweza kuongeza madarasa mengine lakini ni wizara itaendelea kujenga madarasa na skuli za maandalizi katika maeneo mbali mbali kulingana na wingi wa watoto wanaoishi katika maeneo hayo. Hii itasaidia kupunguza msongamano wa watoto wengi darasani katika skuli za maandalizi ikiwemo Skuli ya Madungu.

c) Wizara inakusudia kuifanyia matengenezo makubwa Skuli ya Chekechea ya Madungu kabla ya kuanza kwa mvua za masika. Makisio ya matengenezo hayo tayari yamefanyika ambapo jumla ya shilingi za Kitanzania milioni 58,504,000/- zinahitajika kwa ajili ya matengenezo hayo. Napenda kumuahidi Mhe. Mwakilishi kuwa wizara imeipa kipaumbele matengenezo makubwa ya skuli hiyo ili isije kuanguka. Ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na kunitia moyo katika masuala ya kuwa wameshatenga fedha kwa ajili hiyo.

a) Je, Mhe. Naibu Waziri hii Skuli ya Chekechea ya Madungu na skuli za kama zile bado zipo katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali au zipo katika Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ au bado zipo katika jukumu lake.

b) Kwa sababu unasema umeshaipitia Skuli ya Chekechea ya Madungu na mimi nikueleze tu kwamba Skuli ya Madungu inahitaji uzio kwa sababu jioni na usiku inakuwa ni vilabu au ni maskani za watoto ambao wanajishirikisha na vitendo viovu. Wanafunzi au walimu wanapofika pale asubuhi hukuta viashiria maalum kwa vitendo vilivyofanyika usiku. Je, ni lini utatia uzio ili kunusuru pamoja na mambo mengine yanayotokezea na pia kwamba skuli ile juu ya mlima nyuma imeshakatika inataka kuegemea mabonde ya watu. Ni haraka gani ambazo utazichukua kuhimili tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

Katika suala la ugatuzi kwenye elimu ya maandalizi na msingi kuna maeneo tayari yameshagatuliwa yanashughulikiwa na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na kuna baadhi ya maeneo bado yanaendelea kushughulikiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Baadhi ya maeneo ambayo yanashughulikiwa na Wizara

ya Elimu ni pamoja na mitaala yenyewe, miradi mikubwa na ukarabati mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la Skuli ya Madungu Chekechea, mimi binafsi nimeshaitembelea nimeona kwamba kweli ipo haja ya kuwepo uzio. Lakini kwa sasa wizara haina mpango wa kuweka uzio katika skuli hiyo badala yake itaongeza ulinzi ili kunusuru matendo hayo ambayo umeyasema.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwanza naipongeza sana, sana, sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuwa na nia ya kutaka kuwaondoshea usumbufu wananchi wangu wa Mkumbuu kuwajengea skuli kuanzia darasa la kwanza hadi la nne.

Je, kama wewe Naibu Waziri hilo unalijua, wizara yako ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba lile eneo ambalo wananchi walikuwa wanalima na kwa sababu ardhi ni mali ya serikali inapohitaji kufanya kitu cha maendeleo. Lakini wizara yako ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wale wananchi waliokuwa wakilima pale ili kupata kujikimu kimaisha wamepangiwa mipango mizuri na kupatiwa fidia zao kwa sababu hivi sasa imeshatokea migogoro na nimeshaanza kupigiwa simu. Mhe. Naibu Waziri naomba majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, nalielewa suala hili na tayari Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeshapeleka fedha kwa ajili ya kujengwa skuli hii.

Kuhusu ushirikishaji wananchi ili kupata ridhaa yao, suala hili limeshafanywa likiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Lakini awali nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu fasaha anayoyatoa kwa wajumbe.

Mhe. Mwenyekiti, matatizo ya uchakavu na ubovu wa majengo vile vile unaikumba Skuli ya Maandalizi ya Kiislamu katika jimbo langu la Magomeni na wizara inafahamu hilo kwa sababu katika hotuba mbali mbali za bajeti nimepiga kelele juu ya hilo. Hivi sasa ukweli ni hatari sana kutokana na paa linavyovuja, *ceiling board* zinaanguka na ile ni skuli ya watoto na tayari Mhe. Mbunge wa Magomeni ametoa mchango wa bati mia moja. Je, wizara inasemaje juu ya utengenezaji wa jengo hili na mvua za masika zinakuja. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Ni kwamba kwa mujibu wa taratibu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali zinazohusiana na majenzi, jengo linatakiwa lianzishwe na wananchi ikifika hatua fulani jengo hilo likabidhiwe Wizara ya Elimu na ndio hapo Wizara ya Elimu inaweza kulikamilisha. Ikiwa jengo hili limepitia katika hatua hizo hizo basi zinaweza kukamilishwa. Lakini hata hivyo, nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba afike wizarani na suala hili linazungumzika. Ahsante sana.

Nam. 51

Changamoto za Ugatuzi

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa hivi sasa kumekuwa na ugatuzi kwa ngazi za wilaya kwa baadhi ya wizara za serikali ikiwemo Wizara ya Afya.

(a) Je, ni vituo vingapi vya afya vilivyogatuliwa Unguja na Pemba.

(b) Je, ni changamoto gani zilizojitokeza baada ya kugatuliwa kwa vituo vya afya.

(c) Je, ni upi wajibu wa Wizara ya Afya na ule wa Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa vituo vilivyogatuliwa ili kuviwezesha vituo hivyo kutoa huduma bora kwa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 51 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya vituo vya afya 158 vimeingia katika ugatuzi Unguja na Pemba.

Kuhusu swali ni changamoto gani zilizojitokeza baada ya kugatuliwa vituo vya afya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kulieleza Baraza lako tukufu kwamba changamoto katika mabadiliko yoyote ni jambo la kawaida, bali

katika sekta zilizoingia katika ugatuzi, changamoto hizi kwetu ni chachu na kutupa njia za kuweza kujiimarisha kukabiliana na mabadiliko haya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuzieleza baadhi ya changamoto zinazotokana na ugatuzi nazo ni pamoja na uelewa mdogo juu wa ugatuzi kwa watendaji wa Wizara ya Afya na watendaji wa Halmashauri, pia bado kazi za Timu za Afya Wilaya (*DHMTs*) hazijafahamika vizuri kwamba ni timu za afya ndio kiungo baina ya vituo vya afya na au ni halmashauri. Timu hizi ndio chanzo cha taarifa zote za afya wilayani na ndio msimamizi mkuu wa kazi za afya zinazotolewa katika vituo vya afya na katika jamii.

Mhe. Mewnyekiti**,** kwa sasa mipango kazi inayotekelezwa katika wilaya ni ile iliyopitishwa na kukubalika na Wizara ya Afya na inatokana na mpango kazi mama wa mwaka wa afya (*Comprehensive District Health Plan*). Utekelezaji wa mpango kazi huo haufuatwi na baadhi ya halmashauri kwa kiasi kikubwa. Pia, yapo malengo na viashiria ambavyo vinatakiwa kufikiwa jambo ambalo halijafahamika bado.

Mhe. Mwenyekiti**,** changamoto za kupandisha kiwango cha chanjo, kutekeleza kazi ambazo zina mchango mkubwa katika kupunguza vifo vya mama na mtoto bado pia hazijafahamika. Kadhalika masuala ya afya ni ya kisayansi zaidi hivyo yanawapa shida katika kuyafahamu kwake baadhi ya watendaji wa halmashauri.

Mhe. Mwenyekiti**,** nimetakiwa kueleza majukumu ya sekta mbili hizi katika ugatuzi nayo ni kama ifuatavyo: Wizara ya Afya itaendelea kuhusika na uandaaji wa sera, miongozo na mifumo ya kuweka viwango vya huduma na utoaji wa mafunzo, na Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ itahusika na kutekeleza sera, miongozo na kufikia

viwango vya huduma vilivyowekwa pamoja na kusimamia uwepo wa miundombinu ya afya, ikiwemo ujenzi, ukarabati na matengenezo ya majengo na vifaa. Ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza pamoja na majibu yake mazuri yenye mwelekeo katika Wizara ya Afya. Ningependa kujua tu je, ni utaratibu gani wa haraka utakaochukuliwa ili kutoa elimu kwa wafanyakazi hawa wa *DHMTs* kuwezesha kufahamu wajibu wao ili kwenda sambamba na lile lengo la ugatuzi la Serikali Kuu, ili kwa dhamira ya serikali ya kutoa huduma bora ya afya kwa wananchi wake katika halmashauri hizo za wilaya zilizopewa hilo jukumu la ugatuzi. La kwanza.

La pili, kwa kuwa amekiri kwamba baadhi ya halmashauri hazifuati mpango kazi wa mwaka kwa Wizara ya Afya (*Comprehensive District Health Plan*). Je, wizara yake pamoja na Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inayosimamia ugatuzi wana mpango gani wa kuhakikisha kwamba halmashauri zote zinafuata kikamilifu mpango huu ili kuweza kukidhi haja iliyopo ya ugatuzi. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa wizara yangu pamoja na Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inafanya kazi ya kupanga ili kuelimisha *DHMTs* pamoja na watendaji wengine. Lakini yote haya yanayojitokeza ya kutokufahamu majukumu yao ni kwamba hawana elimu ya ugatuzi.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nilieleze Baraza lako tukufu kwamba hili jambo la ugatuzi ni jambo kubwa na ni jambo jipya katika serikali yetu. Kwa hivyo, ni lazima changamoto zitatokea na ndio hizi ambazo kwa sasa wizara zinapambana ili kutoa elimu ya kutosha kwa watendaji ili kuweza kukabiliana na kuweza kutoa huduma ipasavyo kwa wananchi. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana leo kwa kuniona, pamoja na majibu marefu sana ya kupendeza ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Kwa sababu amekiri katika jibu mama kuwa kuna changamoto nyingi ambazo zimejitokeza baada ya *D by D*, lakini katika vituo vyetu vya afya ambavyo vimegatuliwa ikiwemo Jimbo la Mpendae kumejitokeza upungufu mkubwa wa *reagent* katika maabara na hadi kufikia kinamama kupimwa damu tu, lakini *test* nyengine hakuna. Je, serikali ina mpango gani wa dharura kuweza kukidhi haja hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, upungufu au ukosefu wa *reagent* katika kituo chake inawezekana ni tatizo la ufuatiliaji. Kwa sababu mpaka sasa hatujapata taarifa ya vituo vyengine vyote kama kuna mapungufu au ukosefu wa *reagent***.** Kwa hivyo, namuomba awasiliane na daktari mkuu wa kituo chake ili kujua kwamba kafuatilia kaomba au ni kitu gani ambacho kimesababisha. Hata hivyo, wakati nikiondoka hapa namuahidi kwamba nitafuatilia mimi wizarani ili nijue kwamba ni kituo hicho tu hakina au ni wizara hatuna *reagent* za kuwapatia vituoni. Kama lipo hilo tatizo namhakikishia kwamba tutalirekebisha na *reagent* pamoja na mambo mengine ambayo yanahitaji kutoa huduma kwa wananchi wetu vituoni yatapatikana.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo ameyasema, lakini vile vile naomba nimuulize swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba moja ya udhoofishaji wa suala hili la ugatuzi ni kukosekana kwa wananchi wenye elimu ya kutosha. Na kwa kuwa amesema kwamba wizara yake imeandaa sera na mikutano kuhamasisha jambo hili ili wananchi walielewe vya kutosha. Je, ni lini suala hili litaanza.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, hii haihitaji lini, hivi sasa wizara hizi zote zinazohusika na ugatuzi zina kazi kubwa na zinakutana kila baada ya muda kupanga na kuangalia ni kitu gani ambacho kitaboresha zaidi au ni kitu gani ambacho kitapeleka haraka utekelezaji mzuri katika vituo vyetu kuhusiana na ugatuzi kwa sababu ni jambo geni, ni jambo jipya. Kwa hivyo, namuahidi na ninamhakikishia kwamba mara baada ya kukamilika basi wataona mabadiliko na wataona wizara zote kila wizara ikielekea upande wake kutekeleza majukumu yake. Tunawaomba wananchi pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walete mashirikiano ya kutosha katika wizara zetu zinazohusika na ugatuzi, ili kuweza kufanikiwa kukamilisha lengo na dhamira ya serikali kupeleka huduma nzuri zaidi kwa wananchi ambao wapo chini na wanahitaji kupata huduma bora.

Nam. 68

Mikakati ya Kuimarisha Sekta ya Usafiri Baina ya Unguja na Pemba

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Kisiwa cha Pemba kimekuwa na changamoto ya usafiri wa anga na wa bahari kwa kukosekana kwa boti zinazokwenda kwa kasi na ughali wa usafiri wa ndege.

(a) Je, serikali imeliona hilo na kama wanaliona wamechukua hatua gani.
(b) Kama sekta ya usafiri wa boti za haraka hakuna mwekezaji. Je, serikali ina mpango gani wa kununua boti za kasi.
(c) Je, serikali inapanga nauli za meli na ndege au wamiliki wanajipangia wenyewe tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 68 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanza juhudi za kuondoa tatizo la usafiri kwa kununua meli mpya ya abiria ya M.V Mapinduzi II ambayo imekuwa ikisaidia kwa kiwango kikubwa kwa kutoa huduma ya usafiri kwa hapa Zanzibar kwa gharama nafuu. Vile vile, serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi inaendelea kutoa huduma za usafiri ikiwemo Kampuni ya *Azam Marine* kwa kutumia meli yake ya *Sealink I* na *II* na hufanya safari zake mara kwa mara katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Kwa upande wa usafiri wa anga, makampuni binafsi ya ndege yanaendelea kutoa huduma za kusafirisha abiria baina ya Unguja na Pemba kiasi ambacho imepelekea kupunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la usafiri wa anga.

(b) Mhe. Mwenyekiti, serikali kwa sasa haina mpango wa kununua boti za kasi. Hata hivyo, serikali kwa sasa inaendelea na maandalizi ya kununua meli ya mafuta na baadae meli ya abiria.

(c) Kwa upande wa nauli za meli za kampuni zinapendekeza nauli kwa safari za meli kwa Mamlaka ya Usafiri wa Baharini *(ZMA)*, wizara kupitia mamlaka hiyo inafanya uhakiki wa nauli ambazo zinapendekezwa na kuonekana nauli hiyo inakwenda sambamba na mahitaji ya sasa, wizara huidhinisha nauli hizo kwa makampuni na kuanza kuzitumia.

Vile vile, kwa upande wa safari za ndege Mashirika ya Ndege yanapanga bei ya nauli wenyewe ili kuleta ushindani wa kibiashara. Hata hivyo, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar tayari imeshawasiliana na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania kuangalia uwezekano wa kudhibiti bei hizo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi namshukuru waziri kwa majibu yake mazuri. Mimi nimuulize Mhe. Naibu Waziri kwa sababu bado nasisitiza kusema kwamba serikali ndio yenye jukumu kubwa la kuwasafirisha wananchi wake katika visiwa vya Unguja na Pemba. Nimuulize waziri kwamba kutokana na hali kubwa ya matatizo ya usafiri na yeye amesema hana mpango wa kununua boti, lakini pia kuna wawekezaji ambao wapo katika kipindi cha nyuma kulikuwa na mwekezaji alikuwa anaitwa kwa jina Khamis Kipara alikuwa na boti zake hapa za kasi zikienda safari. Boti zile bado zipo katika bahari au katika ufukwe wa Zanzibar. Je, serikali imewahi kumfuata wakaweza kumjua matatizo yake nini ili kuweza kusaidia usafiri huu.

Swali la pili, serikali ina mpango gani wa kuhamasisha wawekezaji kuwa ndege kubwa kwenda Pemba ili nauli ziwe bei nafuu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake ya nyongeza yenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Kiutaratibu sisi wizara yetu kupitia *ZMA* huwa tunatoa ushauri na vile vile maelekezo kwa zile boti zote ambazo zinafanya kazi na pale boti inapoharibika basi sisi hupeleka mafundi wetu kuangalia namna gani zile boti baada ya kutengenezwa zinakidhi viwango. Ni kweli aliyemtaja alikuwa na boti na boti zake hivi sasa zote zimeharibika kama ilivyoharibika meli ya *Azam Sealink II,* lakini kiutaratibu yeye sasa anahitajika kukaa na makampuni ya fedha ili kuangalia kumpa mtaji au mkopo wa kuweza kufanikisha lengo lake la kutengeneza hizo meli na baadae sisi kupitia *ZMA* kuzikagua kuhakikisha kwamba zinakidhi viwango baadae tuziruhusu.

Kwa hivyo, mimi nitamuomba sana huyu mwekezaji awasiliane na mashirika au taasisi za kibenki za kifedha ili wamsaidie katika hilo. Sisi tupo tayari kuhakikisha kwamba wale wawekezaji wote wanaotaka kuwekeza katika sekta ya meli basi tunawasaidia kufanikisha kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wetu.

Kuhusu suala la ndege mashirika makubwa kwenda Pemba ili kupunguza gharama. Kusema kweli sisi tumeendelea sana kuwaomba hawa makampuni ili yafanye hiyo kazi. Karibuni tu tulikuwa na kikao na *ATCL* na Kamati yetu ya Ardhi na Mawasiliano na tukawashauri vile vile waipeleke *ATCL* Pemba na wakatuahidi kwamba wanaangalia mpango na pale hali itakaporuhusu basi watapeleka ndege yao kule Pemba.

Vile vile *precision* ilikuwa imeanza kupeleka ndege yake kule Pemba na ilisaidia sana lakini kumetokea baadhi ya matatizo. Nina imani kubwa sana tutaendelea kuwashajihisha wawekezaji waendelee kupeleka ndege kubwa kama walivyofanya Assalam kule Pemba kuwasaidia wananchi kuepukana na adha hii ya usafiri. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuongezea majibu ya nyongeza kwa Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Mheshimiwa kama itakumbukwa baada ya kutokea ajali za kuzama kwa meli na kutokea athari kubwa ya kupoteza maisha kwa wananchi wetu na hasara kubwa iliyotokea kutokana na ajali hizo, serikali ilibidi kuchukua hatua maalum ya kubadili sheria na kanuni zake ili kuziweka katika viwango vilivyo bora zaidi kwa zile meli ambazo zinatoa huduma za usafiri katika ukanda wetu huu, ili kunusuru maisha na mali za wananchi wetu. Kutokana na vigezo hivyo, ndio maana meli nyingi nyengine zilizo katika uchakavu au zilizokuwa katika hali sio bora zinashindwa kutimiza vigezo hivyo na ndio maana vikawa havipati ruhusa ya kutoa huduma ya usafiri.

Mhe. Mwenyekiti, lakini serikali siku zote iko tayari kushirikiana na yeyote yule atakayetimiza masharti hayo ili aweze kutoa huduma katika visiwa vyetu hivi ili wananchi wapate unafuu. Na tumeweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika sekta ya usafiri msingi wake ni kuvutia wawekezaji ili wajitokeze kwa wingi ili watoe ushindani katika sekta hii na wananchi wetu wapate nafuu. Kwa hivyo, nawaomba wananchi tukumbuke kwamba, sababu za kuweka vigezo vile ni kunusuru maisha ya watu wetu na mali zao. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana kwa kuniona katika swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kuhusiana na sekta hii naomba kumuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Shirika la Ndege la *ATCL* ni shirika la Muungano na kwa kuwa tatizo la usafiri Pemba ni tatizo sugu na kila siku kunaongezeka nauli. Je, haoni sasa wakati umefika wa kutumia tiketi ile ile ya *union* kuwashawishi *ATCL* wakaanzisha safari za uhakika hata mara mbili kwa mwezi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la *ATCL* kama ifuatavyo. Kama nilivyosema hapo kabla kwamba kweli *ATCL* ni shirika la Muungano lakini sote tunajua hivi sasa limeanza kujiimarisha na mashirika yote yanapofanya biashara basi yanataka yapate faida, hasa haya mashirika ya ndege kwa sababu ni mtaji mkubwa sana unaochukuliwa. Lakini mimi nina imani kubwa sana baada ya kukaa nao na kuwaelezea haja hiyo wamesema watakwenda kufanya utafiti kwa sababu wana kitengo chao cha utafiti na baadae nina imani kubwa sana kwa ajili ya kuuendeleza Muungano wetu na maslahi ya nchi zetu zote mbili, basi tutafikia hatua nzuri katika kuliwakilisha vizuri hili suala. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri nataka kumuuliza swali dogo la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Tangu kipindi ambacho meli yetu ya MV. Mapinduzi II imepata hitilafu za kiufundi kumejitokeza tabia iliyokuwa si nzuri kwa vyombo vya usafiri vya watu binafsi. Unapofika kwenda kukata

tiketi wananchi wakifika tu wanaambiwa tiketi za *economic* zimekwisha ama wakate *business* ama *VIP*. Sasa imekuwa linaleta usumbufu na hili wananchi wamelifuatilia yaani hata kama utakuwa mtu wa mwanzo utaambiwa tiketi zimemalizika.

(a) Je, wizara yake inalijua hili.
(b) Kama hailijui ana mikakati gani ya kulifuatilia ili kuweza kuondosha usumbufu kwa wananchi wetu ambao uwezo wao ni wa kipato cha chini na wanahitaji safari za ndani na nje ya nchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo. Tatizo hili hutokezea zaidi wakati wa kipindi cha likizo hasa za wanafunzi kipindi cha Disemba. Mimi mwenyewe nilikwenda bandarini nikatoa maagizo ili kuhakikisha kwamba kila tiketi inayouzwa basi inauzwa kwa mujibu wa gharama yake, na hatua hizo zimekuwa zikifanya kazi vizuri, kwani hivi sasa kuna vibanda kama viwili vimefungiwa kutokana na kuongeza bei isiyo halali. Lakini licha ya hivyo, kila siku *ZMA* imekuwa inatoa matangazo kupitia redio au vyombo vya habari kwamba wananchi wanatakiwa wanunue tiketi katika vibanda halali na kwa bei halali na vile vile aoneshe kadi au kitambulisho chake ili kupata ile tiketi.

Watu wetu wapo milangoni, wapo ndani kukagua zile tiketi na wale ambao sasa wamekata tiketi si kwa majina yao pale tunawarejesha hawaingii na wale ambao wamechukuliwa tiketi kwa bei kubwa basi wanatoa taarifa kwetu na hatua basi zitachukuliwa kwa watu hao.

Kuhusu swali lake la pili napenda kumuarifu kwamba *ZMA* imeendelea na mikakati ya kuhakikisha kwamba wananchi wanaendelea kukata tiketi kwa mujibu wa bei zilizowekwa na hili

suala tutasimamia na wale wote watakaokwenda kinyume hatua kali zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Naibu Waziri. Swali litaulizwa kwa wizara hiyo hiyo na Mhe. Suleiman Sarahan Said wa Jimbo la Chake Chake.

Nam.71

Kuharibika kwa Meli ya Abiria ya MV. Mapinduzi II

(Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hilo ameliondoa)

HOJA ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018

Mhe. Mohamed Said Mohamed: (**Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti**) Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii adhimu kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia neema ya uhai na afya njema tukaweza kukutana tena katika chombo chetu hiki, ili kutekeleza majukumu yetu ya kulitumikia Taifa na wananchi kwa ujumla. Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii kwa niaba ya Kamati ya Bajeti, ili niweze kutekeleza masharti ya Kanuni ya 108(14) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2016, yanayoelekeza kwa kila Kamati ya Kudumu ya Baraza kuwasilisha ripoti ya shughuli zake mbele ya Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa ushirikianao walionipatia katika kutekeleza majukumu ya Kamati kwa muda wote ambao Kamati ilipangiwa

kufanya kazi zake. Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa ruhusa yako na heshima kubwa niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Mohamed Said Mohamed — Mwenyekiti
2. Mhe. Bahati Khamis Kombo — M/Mwenyekiti
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar — Mjumbe
4. Mhe. Zulfa Mmaka Omar — Mjumbe
5. Mhe. Abdalla Ali Kombo — Mjumbe
6. Mhe. Asha Abdalla Mussa — Mjumbe
7. Mhe. Simai Mohammed Said — Mjumbe
8. Ndg. Abdalla Ali Shauri — Katibu
9. Ndg. Asha Said Mohamed — Katibu
10. Ndg. Kassim Tafana Kassim — Katibu

Mhe. Mwenyekiti, Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilikutana na watendaji wa Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa wadau katika shughuli za Baraza, Kamati pia ilikutana na wadau mbali mbali kwa lengo la kubadilishana uzoefu kuhusu masuala mbali mbali yanayohusu Uchumi, Biashara, Sera za Kodi, Utalii, na Uwekezaji. Vikao hivyo vililenga kuisadia Serikali katika utekelezaji bora wa Bajeti na Mipango ya Maendeleo sambamba na kubuni njia za kuimarisha mapato kwa kuongeza ufanisi pamoja na kuibua vyanzo vipya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa dhati kabisa kuwashukuru Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza, watendaji wa serikali pamoja na wadau wote walioshiriki kwa namna moja au nyengine katika vikao vya Kamati ya Bajeti kwa mashrikiano waliyoipatia Kamati, ambayo kimsingi yameisaidia katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Utekelezaji wa Kazi za Kamati za Wizara ya Fedha na Mipango

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti ilipokea taarifa mbali mbali za Wizara hii za utekelezaji wa bajeti ikiwa ni pamoja na taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha robo ya nne (Aprili – Juni) 2016/2017, Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha robo ya kwanza (Julai – Septemba) 2017/2018 na Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha robo ya pili (Oktoba – Disemba) 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya Mapato yanayokusanywa na Serikali kuwa hayaendi sambamba na matumizi, kwa vile mapato yanayokusanywa ni madogo ukilinganisha na matumizi yenyewe. Kwa kipindi cha (Oktoba - Disemba 2017/2018) Serikali imekusanya Tsh 182.29 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 93.73 ya malengo. Kwa upande wa matumizi Serikali ilikadiria kutumia jumla ya TZS 252.27 bilioni na matumizi halisi yaliyofanyika ni TZS 204.18 bilioni sawa na asilimia 80.9 ya makisio ya jumla.

Mhe. Mwenyekiti, matumizi haya ni makubwa ukilinganisha na mapato yaliyokusanywa ya TZS 182.29 bilioni. Kamati inaishauri serikali kuweka vipaumbele katika matumizi yake ili kuweza kuwa na bajeti yenye uhalisia na yenye kutekelezeka.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa kuwa serikali inafanya matumzi makubwa zaidi katika utekelezaji wa kazi za kawaida, Kamati inaishauri serikali wakati wa kufanya matumizi yanayohusiana na miradi ya maendeleo, iweke mkazo zaidi katika uwekezaji wa miradi yenye ufanisi na tija kwa jamii. Kufanya hivyo kutapelekea kutoa fursa kwa wananchi walio wengi katika kupata ajira, kuongeza kipato, maarifa na ujuzi kutokana na miradi hiyo. Aidha, Kwa kuwa miradi mingi ya maendeleo utekelezaji wake

umekuwa wa kusuasua kutokana na kutopatikana fedha, Kamati inashauri katika utekelezaji wa miradi, kuwepo na vipaumbele kwa kutekeleza miradi michache na yenye kuleta tija kwa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya utalii ni sekta muhimu katika kukuza uchumi wa Zanzibar, kamati imearifiwa kuwa, kwa kipindi cha (Januari – Juni) 2017 kumekuwa na ongezeko la watalii ambapo watalii walioingia nchini walifikia 170,581 ukilinganisha na watalii 143,851 walioingia mwaka 2016.

Mhe. Mwenyekiti, Licha ya ongezeko kubwa la uingiaji wa watalii nchini, Kamati imebaini kuwa sekta hii bado ina changamoto kubwa katika utekelezaji wa majukumu yake, kwa vile mapato yanayotokana na utalii bado hayajatumika ipasavyo katika kurekebisha kasoro mbali mbali zilizopo katika sekta hiyo sambamba na kuwepo kwa changamoto ya utaalamu katika kuisimamia na kuiendesha sekta hii. Aidha, Kamati imebaini bado sekta hii haijatengewa fedha za kutosha katika kuutangaza utalii katika masoko ya kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, Kuhusiana na Deni la Taifa ambalo linaendelea kukuwa siku hadi siku, Kamati inaishauri serikali kuchukua jitihada za makusudi za kupunguza kasi ya ukuaji wa deni hilo, ikiwa ni pamoja na kupunguza utegemezi wa Bajeti yake kwa kukopa nje ya nchi (washirika wa maendeleo) na badala yake bajeti itegemee zaidi rasilimali fedha zilizopo nchini.

Benki Kuu ya Tanzania (Bot) Tawi la Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, Jukumu la msingi la Benki Kuu Tawi la Zanzibar ni kuishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusiana na mambo ya fedha na uchumi pamoja na kuhifadhi akiba za Benki za Biashara. Kamati ilifanya ziara Katika Benki

Kuu Tawi la Zanzibar kwa lengo la kupatiwa taarifa juu ya Utekelezaji wa Majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya uelewa mdogo wa wananchi kuhusu Majukumu ya Benki Kuu. Ili kukabiliana na Changamoto hiyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar kuwaelimisha wananchi juu ya majukumu ya benki hiyo, pamoja na fursa za uwekezaji katika masoko ya fedha zinazopatikana katika Benki Kuu. Aidha, Kamati inashauri Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wapatiwe mafunzo maalum yatakayowawezesha kufahamu majukumu ya Benki hiyo, mafanikio pamoja na changamoto zake.

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar – *ZSSF*

Mhe. Mwenyekiti, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar umeanzishwa chini ya Sheria Namba 2 ya mwaka 1998, kwa lengo la kuwahifadhi wanachama wake wanaopatwa na majanga ambayo husitisha au hupunguza kipato chao kwa sababu mbali mbali kama vile uzee, ulemavu, maradhi au kifo pamoja na majanga mengine yaliyoainishwa katika Sheria hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa changamoto za msingi za Mfuko ni mabadiliko ya Sheria ya Utumishi wa Umma Nam 2 ya mwaka 2011 yanayotokana na Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbali Mbali Nam 1 ya 2018, ambayo kimsingi yanaathiri uendeshaji wa Mfuko katika kutoa huduma kwa wanachama wake. Kimsingi Sheria hiyo inapokonya baadhi ya Mamlaka ya Mfuko, na hivyo kuondosha mantiki ya kuwa na Bodi ya Mfuko huo.

Aidha, baadhi ya maelekezo yanayotolewa na serikali yanaathiri utendaji wa Mfuko huo hususan katika suala la uwekezaji ambalo

linahitaji umakini mkubwa katika kuhakikisha Mfuko unaekeza kwa misingi ya kupata faida badala ya kuekeza zaidi katika miradi ya kuitumikia jamii *"Social Responsibilities"*.

Mhe. Mwenyekiti, Uwekezaji wa Miradi mikubwa ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar unahitaji ubia katika kuitekeleza ili kuweza kugawana hasara na tija inayoweza kupatikana. Hata hivyo, Kwa kipindi kirefu mfuko umekosa wabia wa kushirikiana katika miradi inayoekeza na kupelekea Mfuko kutumia mtaji wake pekee katika miradi hiyo ambapo ni hatari kwa uwekezaji mkubwa. Kamati inaushauri Mfuko kubadilisha mbinu za kutafuta wabia wa uwekezaji pamoja na kutangaza mafanikio yaliyopatikana katika miradi iliyokamilika kwa lengo la kuwavutia wabia hao, sambamba na kuhakikisha wanafanya uwekezaji katika miradi yenye soko kwa upande wa Zanzibar.

Aidha, Kamati inashauri Mfuko uzitangaze zaidi fursa zilizopo katika miradi yake iliyokwisha kamilika, ili kupata waekezaji ambao wataweza kuunga mkono jitihada za Mfuko huo na hatimae kuongeza tija katika baadhi ya miradi ambayo kwa sasa inaonekana kuendeshwa kwa hasara zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, ufafanuzi zaidi wa ufanisi wa mapato na matumizi ya miradi mbali mbali ya Mfuko unapatikana katika kiambatanisho namba 1 katika Kitabu cha Ripoti ya Kamati yangu.

Mhe. Mwenyekiti, Mfumo wa ukusanyaji mapato unaotumika kwa sasa katika kiwanja cha kufurahishia watoto cha Uhuru - Kariakoo unatia mashaka katika kudhibiti mapato yanayokusanywa. Kamati inaushauri Mfuko uharakishe mchakato wa kuanza kutumia mfumo wa kisasa wa kielektroniki wa kukusanya mapato utakaowezesha fedha hizo kuingia moja kwa moja kwenye akaunti ya Mfuko.

Mamlaka ya Uwekezaji na Ukuzaji Vitega Uchumi Zanzibar - *ZIPA*

Mhe. Mwenyekiti, Katika kuzingatia umuhimu na mchango wa uwekezaji katika suala zima la ukuaji wa uchumi, Kamati imelitazama kwa ukaribu mkubwa suala hilo kupitia Mamlaka ya Uwekezaji na Vitega Uchumi (*ZIPA***)** ambayo kwa Zanzibar ndiyo yenye jukumu la moja kwa moja la kusimamia vitega uchumi kwa mujibu wa Sheria Nam 11 ya mwaka 2004 ambayo imeanzisha Mamlaka hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa changamoto za msingi za *ZIPA* ni kutokukamilika huduma za *"One Stop Center"* ambazo zitamuwezesha muwekezaji kumaliza mahitaji yake yote yanayohusiana na uwekezaji katika eneo moja, suala hili limekua likizungumzwa kwa muda mrefu bila ya kufanyiwa kazi. Kamati inaishauri Serikali kupitia *ZIPA* kulipa uzito maalum suala hilo kwa kuimarisha huduma hiyo, ili kurahisisha mazingira ya mchakato wa uwekezaji nchini. Aidha, kuimarisha huduma za "*one stop center"* kutaepusha kuwepo kwa madalali ambao wanaipa taswira mbaya Mamlaka kwa kutoa taarifa zisizo sahihi kwa wawekezaji.

Maeneo Huru ya Uwekezaji Amani

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kutembelea maeneo ya Viwanda vidogo vidogo Amani ikiwa ni moja ya maeneo ya uwekezaji yaliyotengwa na serikali kwa lengo la kuendeleza waekezaji wa ndani na wa nje wa viwanda vidogo vidogo.

Mhe. Mwenyekiti, Suala la ulinzi wa maeneo ya uwekezaji ni la muhimu sana kwa usalama wa wafanyakazi, waekezaji na mali zao. Kamati ilibaini kubomoka kwa uzio wa Maeneo Huru ya Uwekezaji Amani na kwa kuwa *ZIPA* haiwezi kuufanyia

marekebisho uzio wa maeneo hayo kutokana na gharama kubwa zinazohitajika (milioni 80 kwa kilomita 20), Kamati inaishauri serikali kuipatia fedha *ZIPA* katika Bajeti ya 2018/19 kwa lengo la kuujenga uzio na kuweza kuzihifadhi vyema mali zilizomo katika maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, Kiujumla Kamati haikuridhishwa na mazingira ya maeneo ya viwanda vidogo vidogo kutokana na majengo yaliyotengwa kwa ajili ya wawekezaji kutotumika kwa muda mrefu na hivyo kuikosesha mapato Mamlaka na Serikali kwa ujumla. Aidha, baadhi ya majengo yanaonekana kuchakaa na kuvuja hali iliyochangiwa na kutofanyiwa ukarabati kwa muda mrefu sambamba na kuwepo kwa makontena yaliyokaa kwa muda mrefu bila ya kutumika na kutofahamika mmiliki wake.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaishauri *ZIPA* kuyaendeleza majengo ambayo hayajatumika kwa muda mrefu kwa kuwapatia waekezaji wengine walio tayari kufanya uwekezaji katika majengo hayo ili kuipatia serikali mapato. Aidha, Kamati inaishauri *ZIPA* iandae mpango endelevu wa kuyakarabati majengo yaliyo ndani ya eneo la uwekezaji kwa kuyafanyia matengenezo madogo madogo kila baada ya muda, kwa lengo la kuyatunza na kuiepushia serikali gharama kubwa iwapo majengo hayo yataendelea kukaa kwa muda mrefu bila ya kufanyiwa ukarabati.

Mradi wa Penny Royal (*Gibbraltar*) Zanzibar Ltd

Mhe. Mwenyekiti, Mradi wa *Penny Royal* ni mradi mkubwa unaotarajiwa kuleta fursa kubwa ya ajira tokea kuanzishwa kwake hadi wakati wa utoaji wa huduma. Mbali na ajira ambazo wananchi watafaidika nazo, jamii pia itafaidika kupitia programu mbali mbali ambazo zitasimamiwa na mradi huu ikiwa ni pamoja na kuwaendeleza wajasiriamali, kutoa elimu maskulini na michezo kwa wana kijiji.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imebaini kusuasua kwa mradi kutokana na muwekezaji kutopatiwa eneo la ziada la hekta 220 alililoliomba kwa ajili ya utanuzi wa mradi, ambapo Serikali imemuekea sharti la kuanza kuendeleza eneo alilopatiwa awali kabla kuongezewa eneo jengine. Changamoto hii inapelekea kuchelewa uendelezaji wa mradi huo na kuongezeka kwa gharama. Kamati inashauri mamlaka husika kuliangalia tena suala hilo, kwa kuzingatia umuhimu wa mradi husika na faida inayoweza kupatikana kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia imebaini kukosekana kwa Mpango Mji (*Master Plan*) wa Mkoa wa Kaskazini na wa nchi kwa ujumla kunapelekea serikali kuchelewa ama kusita kufanya baadhi ya maamuzi juu ya aina ya uwekezaji na uimarishaji wa miundo mbinu inayokusudiwa kufanyika katika uwekezaji huo. Kamati inaishauri serikali kuandaa Mpango Mji, kwani kutokuwepo kwa mpango huo kunapeleka kuibuka kwa changamoto mbali mbali kutokana na kutofahamika mipango ya baadae ya serikali katika maeneo mbali mbali na kupelekea urasimu juu ya maamuzi ya ardhi na hatimae kuzorotesha shughuli za uwekezaji. Mhe. Mwenyekiti, *Penny Royal* mpaka leo haijapata *lease*. Sasa tunaomba serikali itakapokuja kujibu kidogo ituambie ni sababu zipi ambazo hazijapatikana *lease* kwa *Penny Royal.*

Maeneo Huru ya Uwekezaji - Fumba

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara ya kuona maendeleo ya mradi wa nyumba za Fumba ambao upo chini ya kampuni ya Bakhresa (*Bakhresa Group of Company*). Mradi huo unahusisha nyumba za kuishi pamoja na ujenzi wa miundombinu, ikiwemo barabara, viwanja vya michezo na maduka makubwa (*Shoping Mall*). Aidha, Kamati iliarifiwa kwamba kwa awamu ya kwanza jumla ya nyumba 152 zitajengwa kwa ajili ya wananchi

wa kipato cha kati na cha juu. Mhe. Mwenyekiti, nasema kipato cha wananchi wa kati na cha juu kwa sababu mwananchi wa chini kabisa nyumba zile hataweza kuzifikia ndio maana tukasema hapa kwa mwananchi wa kiwango cha kati na cha juu.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa gharama kubwa ya mradi huo wa mji wa Fumba itatumika katika kuimarisha miundo mbinu ya msingi kwa kuwa eneo hilo halikua na miundo mbinu ya msingi wakati wa kuanzishwa kwake na kusababisha nyumba za mradi katika mji huo kuwa ghali sana kiasi cha mwananchi wa kawaida kutashindwa kumiliki.

Mhe. Mwenyekiti, Kutokana kwa miundo mbinu ya msingi katika maeneo ya uwekezaji huongeza gharama na hivyo kuwarudisha nyuma wawekezaji. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha miundo mbinu katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji ili kuwavutia waekezaji wenye nia ya kuekeza Zanzibar. Mhe.Mwenyekiti wawekezaji wengi wana nia ya kuekeza Zanzibar lakini ubovu wa sera yetu inaweza ukatukwamwisha katika kuekeza au kuwavutia wawekezaji, hivyo tunaiomba serikali kuwa na sera muhimu sana na sera nyepesi ambayo itaweza kuwavutia wawekezaji.

Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC)

Mhe Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kulitembelea Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (*ZSTC*) ambalo ni muhimu katika kukuza uchumi wa Zanzibar. Miongoni mwa majukumu ya Shirika ni pamoja na kununua, kuuza karafuu pamoja na mazao mengine ya kilimo kwa bei ya ushindani, kulinda ubora wa mazao ya karafuu na mazao ya kilimo, kufanya usarifu, kuongeza thamani pamoja na kutafuta masoko ya nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, Katika kuhakikisha kuwa, Shirika linakwenda sambamba na utekelezaji wa majukumu yake pamoja na kutekeleza mkakati wa mageuzi ya sekta ya karafuu, ni muhimu Shirika likazingatia sana kutatua changamoto zake mbali mbali ili hatimae malengo ya Shirika yaweze kufikiwa na kuimarishwa kwa zao la karafuu, kukuza kipato cha wakulima,uchumi wa nchi, kuongeza ajira na kupunguza umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, Miongoni mwa changamoto za Shirika ni pamoja na wakulima kutoa taarifa zisizo sahihi katika usajili wa taarifa zao zinazohusiana na ukubwa wa mashamba na idadi ya karafuu wanazozimiliki, hali inayoweza kuliathiri Shirika katika upangaji na utekelezaji wa mipango yake. Katika kukabiliana na changamoto hii, Kamati inalishauri Shirika kufanya jitihada za makusudi katika kufuatilia usahihi wa taarifa wanazopatiwa na wakulima. Aidha, kutokana na ushindani mkubwa wa soko kwa nchi nyengine zinazozalisha karafuu kama vile Indonesia, Srilanka, Brazil na India, Kamati inaishauri Shirika lifanye kazi ya kufuatilia taarifa za uzalishaji karafuu katika nchi hizo ili kuweza kupanga mikakati itakayoliwezesha Shirika kuhimili ushindani wa kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika katika jitihada zake za kuwasaidia wakulima wa karafuu wa Unguja na Pemba, limeweka utaratibu wa kuwapatia wakulima hao mikopo isiyokuwa na riba kwa ajili ya kujiandaa na uchumaji wa zao hili muhimu kwa uchumi wa Zanzibar. Licha ya jitihada za Shirika, kumekuwa na tabia kwa baadhi ya wakulima kuchelewa kurejesha mikopo, hali inayolipelekea Shirika kutumia muda mwingi pamoja na gharama kubwa ya kufuatilia mikopo hiyo. Mhe. Mwenyekiti, Kutokana na kuwepo kwa changamoto hiyo, Kamati inalishauri Shirika kuandaa utaratibu utakaohakikisha wakulima wanaopata mikopo wanarejesha kwa wakati ili kuweza kutoa fursa na kupewa mikopo wakulima wengine.

Mhe. Mwenyekiti, Pamoja na kuwepo kwa huduma ya jamii katika vituo vya ununuzi wa karafuu kama vile maji, vyoo, umeme, sehemu za kukaa wakulima wakisubiri kuhudumiwa, Kamati inatoa msisitizo zaidi kwa Shirika kuimarisha huduma za kibenki, kwa kuwa vituo vya mauzo ya karafuu vimekosa huduma hizo. Hali hii imepelekea Shirika kuchukua fedha za ununuzi wa karafuu katika vituo na kuwalipa wakulima vituoni hali inayohatarisha usalama wa wafanyakazi wa Shirika na wauzaji wa karafuu.

Kiwanda cha Makonyo

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilitembelea Kiwanda cha Makonyo – Pemba na kubaini kushuka kwa mapato ya kiwanda hicho kutokana na uchakavu wa mashine zinazotumika katika uzalishaji na kupelekea kiwanda kuzalisha kwa hasara. Aidha, Kamati ilibaini kuwa mashine za kiwanda hicho hazijawahi kufanyiwa matengenezo makubwa tokea kuanzishwa kwa kiwanda mnamo mwaka 1982 hali inayochangia pia kiwanda kufanya kazi siku 42 mpaka 62 badala ya siku 200 ambazo kiwanda kinapaswa kufanya kazi kwa mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, Ili kukabiliana na changamoto ya kushuka kwa mapato, Kamati inaushauri uongozi wa Kiwanda kuendeleza juhudi za kupunguza hasara za uzalishaji kwa kuhakikisha kiwanda kinaendeshwa kwa faida ili kupata ufanisi katika uendeshaji wake. Aidha, Kamati inausisitiza uongozi kufanya uchambuzi wa kina juu ya mahitaji halisi, sambamba na kuweka mikakati mipya na mbinu za kisasa za uendeshaji wa kiwanda hicho.

Mhe. Mwenyekiti, Utumiaji wa mbinu za kizamani za uzalishaji na uendeshaji biashara ni moja ya sababu zinazochangia kiwanda kushindwa kuzalisha kwa kiwango kikubwa. Ili kukiwezesha

kiwanda kuwa na ufanisi, Kamati inaushauri uongozi wa Kiwanda uangalie mbinu mpya za kukiendesha kiwanda hicho ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kukiendesha kwa ubia (*Joint Venture*) kwa kushirikiana na kampuni binafsi zenye uzoefu. Kufanya hivyo kutasaidia katika kuzalisha bidhaa nyingi na bora zaidi zenye kukidhi viwango vya masoko ya nje na kupunguza uzalishaji wa bidhaa zinazotokana na karafuu kutoka katika mataifa mengine kuingia nchini kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, Kwakuwa ni miaka 36 tokea Kiwanda kuanzishwa, Kamati inaona ni vyema kiwanda kifanye kazi kwa kujitegemea badala ya kufanya kazi chini ya mwamvuli wa Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC), ambapo ni vigumu kupima ufanisi halisi wa kiwanda kutokana na kubebwa na Shirika kwa baadhi ya gharama. Imefika wakati sasa kiwanda kujitegemea chenyewe moja kwa moja katika kuhudumia gharama za uendeshaji. Kamati inaamini utegemezi huo unadumaza maendeleo ya kiwanda hicho na kwa msingi huo, kuna kila sababu ya kiwanda kujiwekea mikakati madhubuti ya kuimarisha utekelezaji wa majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, Hata mtoto akishafika miaka sita anaanza kutakiwa aanze kwenda miezi sita miaka miwili aanze kwenda lakini tofauti na kiwanda hicho tangu 1982 ni miaka mingi sana na sasa lazima kiwekewe mikakati ya kuweza kuaanza chenyewe ya kujiendesha chenyewe lakini kama hakiwezi serikali kuanza kuona sera ya kuweza kubinafsisha kiwanda hichi ama kukiuza kabisa kutokana na hasara kubwa ambazo inaitia serikali.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Kilimo ina mchango mkubwa katika uchumi wa nchi na wananchi kwa ujumla ambapo asilimia 40 ya wananchi wamejiajiri katika sekta hiyo na inakadiriwa kuwa zaidi

ya asilimia 70 wanategemea sekta ya kilimo kwa namna moja au nyengine katika kujipatia kipato na kuimarisha maisha yao. Kamati ilifuatilia utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Kilimo na kubaini upungufu wa uzalishaji wa baadhi ya mazao muhimu ya chakula nchini ikiwemo zao la mpunga, licha ya jitihada za Wizara kukarabati miundombinu ya umwagiliaji maji katika maeneo mbali mbali. Hali hii imepelekea kuagiza vyakula kutoka nje ya nchi kama vile mchele kutoka nchi ya Vietnam.

Mhe. Mwenyekiti, Kukabiliana na upungufu wa uzalishaji nchini, Kamati inaishauri Wizara kupitia mradi wa Maendeleo ya Kilimo kuendelea kutoa mafunzo ya kilimo bora cha mazao mbali mbali pamoja na kuwawezesha wakulima kutumia mbinu za kisasa ili kuwezesha kuongezeka kwa bidhaa hiyo. Aidha, katika kuhakikisha usalama wa chakula nchini na kusaidia wakulima kupata soko la bidhaa zao. Kamati inaisisitiza Wizara kusimamia vyema ujenzi unaoendelea wa ghala la kuhifadhia chakula ili liwe katika kiwango kinachostahiki pamoja na kulitumia kwa malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa kuzingatia umuhimu wa Wizara hii, kupitia sekta ya uvuvi ambayo inamchango mkubwa kwa ajira, Kamati imechukua jitihada za makusudi za kukutana na Wizara ya Kilimo na Mamlaka ya Uwekezaji na Ukuzaji Vitega Uchumi Zanzibar (*ZIPA*) ili kujadili miradi ya sekta ya uvuvi iliyokwama utekelezaji wake.

Ufafanuzi wa miradi hiyo unapatikana katika kiambatanisho namba 5 cha ripoti ya kamati.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa, miongoni mwa sababu za kukwama kwa miradi ya sekta ya uvuvi ni pamoja na waekezaji kushindwa kufuata taratibu zilizowekwa katika uwekezaji wa sekta ikiwemo suala zima la kuzingatia Sheria na

Masharti yaliyowekwa nchini. Kwa kuwa uwekezaji binafsi unahitajika kwa maendeleo ya nchi, kuendelea kukwama kwa miradi ya sekta ya uvuvi kunazorotesha maendeleo ya nchi ikiwa ni pamoja na kukosa fursa za ajira zinazotokana na uwekezaji huo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaishauri ZIPA kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, kuzifanyia kazi changamoto za kisheria na kuendelea kuwapatia elimu waekezaji katika mchakato mzima wa uwekezaji nchini pamoja na taratibu zilizopo ili wawekezaji wapate uwelewa mapema kabla ya kufanya maamuzi ya uwekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, miradi mingi sana ukiangalia kiambatanisho changu hicho, inafika miradi minane ya uvuvi imekwama kutokana na sera mbovu zilizowekwa naomba sana serikali iangalie tena sera zake katika uvuvi na kuwashawishi wawekezaji ili waweze kuwekeza. Miaka 54 ya Mapinduzi hatuna hata kiwanda kimoja cha samaki ni jambo la kusikitisha sana Mhe. niombe sana serikali ilichukue hili kuona basi sera nzuri itakapokuja kutoa majibu iweze kuweka sera nzuri ya uwekezaji na kuwavutia wawekezaji wa uvuvi.

Mradi wa Ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria la Uwanja wa Ndege (Terminal II)

Mhe. Mwenyekiti, Mradi wa jengo jipya la abiria la uwanja wa ndege (Terminal II) ni miongoni mwa miradi mikubwa ya kitaifa ambao ulikadiriwa kugharimu jumla ya USD 70.4 milioni. Kamati ilipokea taarifa na kukagua mradi huo ili kuona ufanisi wa utekelezaji wake. Kutokana na kasoro mbali mbali za kiufundi zilizojitokeza, gharama za mradi huo ziliongezeka maradufu na kufikia USD 128.7 milioni. Mradi ulianza kutekelezwa mnamo mwaka 2010 kwa mkataba baina ya Serikali ya Mapinduzi ya

Zanzibar kupitia Wizara ya Ujenzi na Mawasiliano na Kampuni ya *Beijing Construction Engineering Group (BCEG)* ya China na ulitarajiwa kukamilika mwaka 2017. Kutokana na kasoro zilizojitokeza hadi leo mradi haujulikani lini utakamilika na Serikali inapaswa ianze kulipa mkopo wa mradi huo ifikapo mwaka 2009.

Mhe. hapa nataka nirudie tena kwakuwa mwaka 2009 ndio mradi ulikuwa huu uanze kulipwa lakini mujibu wa taarifa hizi ambazo walitupatia wizara, lakini juzi wakati Mhe.Waziri wa Fedha anajibu alisema ni mwaka 2017 ndio utaanzwa kulipwa sasa inaelekea hapa serikali bado haijakaa sawa katika takwimu zake tunaomba ikija itupe takwimu halisi ili basi na sisi tuweze kukaa sawa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilipata wasiwasi mkubwa juu ya utaratibu uliotumika wakati wa kuingia mkataba wa ujenzi, kiasi cha Serikali kushindwa kuiwajibisha Kampuni ya *BCEG* kutokana na kasoro za kiufundi ilizozisababisha na kuingiza nchi kwenye janga zito la deni lenye kuongezeka kwa riba pamoja na gharama na bado Serikali inaendelea kuitumia Kampuni hiyo hiyo bila ya kuchukuliwa taratibu za kisheria. Ni dhahiri kuwa Kampuni inayoendelea na ujenzi uzoefu wake bado ni mdogo kiasi cha kuchafua malengo ya mradi na kushindwa kufuata utaratibu wa Sheria za Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (*ICAO*).

Mhe. Mwenyekiti, Kwa kuwa Kamati imearifiwa ifikapo mwaka 2023, mradi wa terminal II utakuwa ushazidiwa uwezo kiasi cha kutoweza kuhudumia ndege tatu kubwa kwa wakati mmoja, Kamati inaishauri Serikali katika kutekeleza miradi yake kuzingatia mikakati ya muda mrefu na kuwekeza katika miradi itakayonufaisha wananchi kwa kipindi kirefu. Mhe. Mwenyekiti, kushindwa kuzingatia mahitaji ya muda mrefu katika utekelezaji wa miradi, kunapelekea Serikali kutosonga mbele katika

kutekeleza miradi mengine kwa kuwa baada ya muda mfupi miradi iliyotekelezwa itahitaji kufanyiwa upanuzi kwa mara nyengine tena.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuwa na wataalamu wa kutosha wa kupitia na kufahamu kwa kina mikataba ya miradi kabla haijaikubali miradi husika ili kuepusha kuzorota kwa miradi hiyo pamoja na upotevu wa fedha za Serikali. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kutoendelea kuchukua makampuni ya aina hiyo katika ujenzi wa miradi na kuwa na uwazi katika kuwapata wakandarasi na wasimamizi wa miradi wenye sifa.

Kamati inaisisitiza Serikali kuwa na usimamizi madhubuti wa watendeaji wote waliopewa dhamana katika miradi na kuhakikisha wanakuwa na uadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao, ili miradi iwe na tija kwa nchi na kuweza kuhimili ushindani mkubwa uliopo katika nyaja ya usafiri wa anga. Mhe hadi hii leo, hatujaona hata taarifa yoyote katika waliofanya uzembe wakati wa *terminal* II kuchukuliwa hatua za kinidhamu za kikazi.

Mradi wa Serikali Mtandao *(E-Government)*

Mhe. Mwenyekiti, Katika bajeti ya mwaka 2017/2018 Baraza lako tukufu liliidhinisha jumla ya Bilioni kumi na milioni hamsini (10,050,000,000) kwa ajili ya matumizi ya Mradi wa Serikali Mtandao ambapo Tsh Milioni hamsini (50,000,000) ni mchango wa SMZ na Tsh Bilioni kumi (10,000,000,000) Mchango wa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia mradi huu, Serikali ilikua na lengo la kuimarisha utendaji na utoaji wa huduma kwa kuziunganisha taasisi zake zote kupitia Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano ya Habari pamoja na kuiunganisha Zanzibar kupitia Mkonga wa

Taifa yaani *fiber optic* wa mawasiliano ya habari pamoja na kuunganisha Zanzibar kupitia mkonga wa kimataifa na visiwa vya Pemba kupitia teknolojia inayotumia waya (*Microwave link*). Kwa ujumla, Kamati imebaini mradi huu haujafanikiwa kuleta ufanisi wa utendaji kazi wa Serikali kama ilivyokusudiwa kutokana na ukweli kwamba, taasisi nyingi za Serikali bado hazijauganishwa taarifa zao katika kituo cha kuhifadhia taarifa yaani *"data center"* ambacho kimeanzishwa chini ya mradi huu. Sambamba na kusuasua huduma ya *"internet"* kupitia mradi huo kiasi cha taasisi za Serikali kuendelea kutumia makampuni ya watu binafsi kupata huduma hizo na hivyo kuiongezea gharama Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuleta ufanisi na kufikia malengo ya mradi wa Serikali Mtandao, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu wa kuhakikisha taasisi zake zote zinatumia kituo cha kuweka kumbukumbu *"Data Center",* ili kuweza kutunza kumbukumbu za Serikali kwa uhakika na kwa muda mrefu zaidi bila ya kupotea na kuharibika. Aidha kuhusiana na mfumo wa kulipia kodi kwa njia ya electroniki *"E-tax"* ambao ni sehemu ya mradi huu, Kamati inashauri mfumo huo uanze kutumiwa na taasisi za Serikali kwa lengo la kufahamu changamoto zake kabla ya kutumiwa na taasisi binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa kuwa mradi huu ni wa gharama kubwa, Kamati inaishauri Idara husika kwa lengo la kuufanya mradi uwe endelevu, kuuendesha mradi kibiashara kwa kutumia fursa mbali mbali katika miradi mikubwa nchini, ili kutanua wigo wa matumizi ya mkonga wa taifa, ikiwa ni pamoja na kusogeza kwa huduma hizo katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya uwekezaji kama vile wa nyumba za makaazi – Fumba na uwanja wa ndege (*Terminal II).*

Mhe. Mwenyekiti, taasisi za serikali ambapo mpaka tunapewa ripoti hii zilizounganishwa ni taasisi 80, sasa utaona ni jinsi gani bado mradi huu haujapata mafanikio makubwa.

Mradi wa Bandari ya Mpigaduri - Maruhubi

Mhe. Mwenyekiti, Mradi wa Bandari ya Mpiga Duri unatarajiwa kutekelezwa kwa mfumo wa ubia baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kampuni ya China *Harbor engineering Ltd (CHEC)* ambao utagharimu jumla ya USD milioni mia mbili thelathini na moja na laki nne (231,400,000). Kati ya fedha hizo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itatoa jumla ya USD milioni mia mbili (200,000,000) kupitia mkopo wa Benki ya China – *Exim Bank* na Kampuni ya China *Harbor Engineering Company Ltd* itatoa jumla ya USD milioni thelathini na moja na laki nne (31,400,000). Mpaka Kamati inafanya ziara katika eneo la Mpiga Duri, bado fedha hizo hazijapatikana kutokana na kutokukamilika kwa mapitio ya rasimu ya makubaliano ya fedha *"Draft Financing Agreement*" yanayopaswa kufanywa na Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar, ifanye mawasiliano na ufuatiliaji wa karibu, ili kuhakikisha hatua zinakamilika kwa haraka na kuuwezesha mradi kuanza kwa utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, uwepo wa diko la uvuvi ambalo vijana wamejiajiri kupitia shughuli mbali mbali ni changamoto nyengine ambayo inapaswa kuzingatiwa kabla ya mradi haujanza kutekelezwa. Kamati inaishauri Serikali wakati wa kuendeleza miradi yake izingatie vijana ambao wamejiajiri katika maeneo hayo kwa kuwapatia eneo mbadala kuendesha shughuli zao ili miradi hiyo isiwe sababu ya kuzuia ajira zao.

UKANDA WA SHUGHULI ZA MAFUTA NA GESI-MANGA PWANI

Mhe. Mwenyekiti, mnamo mwaka 1995 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kuzingatia mahitaji ya siku za usoni, ilitenga eneo katika ukanda wa pwani ya Mangapwani lenye ukubwa wa hekari 380, kwa ajili ya shughuli za kuhifadhi mafuta na gesi, bandari ya kuhudumia upakizi na ushushaji wa mafuta na gesi pamoja na bohari ya kuhifadhia zana na vifaa vya mafuta. Kutokana na kukua kwa mji, kamati imejionea uvamizi unaoendelea kufanywa na wananchi kwa kujenga maakaazi ya kudumu, na shughuli nyengine za kujitafutia riziki ndani ya eneo hilo. Pamoja na muda mrefu kupita tangu kutengwa kwa eneo hilo, mpaka kamati inafanya ziara eneo hilo halijapimwa na halijawekewa alama yoyote inayoonesha kuwa eneo hilo ni eneo la hifadhi ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kamati imeelezwa fedha iliyotengwa kwa kazi ya upimaji imeshakabidhiwa kwa Kamisheni ya Ardhi na Idara ya Upimaji, kamati inashauri kuharakishwa kwa hatua za kupima eneo la hifadhi la Mangapwani, pamoja na kuliwekea alama ili uvamizi usiendelee na kuiepushia serikali gharama zisizo za lazima za kuweza kulipa *deference* baadae.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (*ZURA*)

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa majukumu ya mamlaka hii ni kuleta ufanisi katika huduma za umeme, mafuta, gesi asilia na nishati na nyengine yoyote ambayo itakua inazalisha umeme na kuhakikisha watumiaji wa nishati hizo wanapata huduma zinazostahili.

Mhe. Mwenyekiti, mwishoni mwa mwaka 2017, *ZURA* ilianza rasmi kutumia mfumo mpya wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja

(Bulk Procurement System), kwa lengo la kuongeza ubora wa bidhaa ya mafuta wa udhibiti, pamoja na kupunguza gharama ya bidhaa hiyo. Hata hivyo, kamati imebaini kuwa kutokana na changamoto mbali mbali zilizojitokeza, mfumo huo hauwezi kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa sasa.

Mhe. Mwenyekiti, kuwepo kwa ufinyu wa sehemu ya kuhifadhi mafuta *(Storage Facilites*), kina kidogo cha maji katika bandari ya Mtoni, kiasi cha meli kubwa kutoweza kufunga nanga, pamoja na miundombinu hafifu na ya kizamani ya kushushia mafuta, ni miongoni mwa sababu zinazopelekea mfumo mpya wa *BPS* ushindwe kufikia malengo yake. Kwa sasa bado bei ya mafuta kwa upande wa Zanzibar imeendelea kuwa juu, kulinganisha na Tanzania Bara, pamoja na kuadimika mara kwa mara kwa mafuta hali iliyopelekea kuzoroto kwa shughuli za kiuchumi na kijamii na kuikosesha serikali mapato. Kutokana na changamoto hizo serikali imelazimika kusitisha uagiziaji wa mafuta kwa mfumo wa *BPS* kwa muda, na kuruhusu makampuni binafsi ya mafuta kuagiza yenyewe kama ilivyokuwa awali.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia vikao mbali mbali ambavyo kamati imevifanya na makampuni ya mafuta kwa upande wa Zanzibar, pamoja na ziara katika Mamlaka na Wakala wa Uagiziaji wa Mafuta ya *petrol* Tanzania (*PBPA*) na Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati (*EWURA*), kamati imejiridhisha kwamba, kutokana na changamoto zilizopo na mfumo wa *BPS* kwa sasa hauwezi kutekelezeka na kuleta faida.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuanza kutumia mfumo wa *BPS* na kufikia malengo ya mfumo huo, kamati inaishauri serikali kushughulikia suala la ujenzi wa bandari mpya ya mafuta, na kujenga bohari yenye uwezo wa kuhifadhi mafuta kwa wingi, pamoja na kuzingatia kuweka kifaa cha kupimia mafuta " *flow meter*" na iwapo serikali itaamua kuendelea na mfumo wa *BPS*

kwa sasa, kamati inaishauri *ZURA* kuangalia uwezekano wa kutumia bohari au "*depot*" iliopo Bandari ya Mtwara, ili kuepukana na kuadimika kwa mafuta mara kwa mara.

Mhe. Mwenyekiti, **k**amati pia imebaini kuwa kukosekana kwa mkataba baina ya *ZURA* na makampuni ya usambazaji mafuta katika mfumo uliopo sasa wa uagiziaji wa mafuta. Hivyo, kamati inaishauri *ZURA* kufunga mkataba na makampuni hayo, kwa lengo la kuwa na udhibiti bora wa mfumo uliopo wa kumlinda mteja na kuepusha kuadimika kwa bidhaa ya mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, jana Mhe. Waziri alitoa tathmini kubwa ya kuwa mafuta bado yapo kwa kiwango kikubwa Zanzibar. Lakini nadhani Mhe. Waziri, hakufanya tathmini ya kina au hakupita na uhalisia wake kuona hadi hivi sasa vituo vingi vya mafuta vimekosa mafuta, lakini na kadhia kubwa kila mara ukienda misururu ya foleni. Kwa hivyo, tunaiomba serikali kuweza kuliangalia jambo hili kwa kina zaidi, ili kuona wananchi hawasumbuki na bidhaa hii muhimu.

Mmlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu

Mhe. Mwenyekiti, ni takriban miaka minane sasa tangu Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu kuanza kufanya kazi zake rasmini chini ya mfumo wa makubaliano ya mpito yaani (*Interim Agreement*) baina ya wizara zinazosimamia uvuvi kwa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kutokana na Zanzibar kutoridhia Sheria namba 1 ya mwaka 1988 yaani (*The Deep Sea Fishing Authority Act, No. 1 of 1998*), iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuanzisha mamlaka hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa changamoto zinazoikabili mamlaka hiyo ni kupungua kwa meli za uvuvi na kushuka kwa

mapato, yanayosababishwa na mabadiliko ya kanuni za usimamizi yaliyofanywa kwa lengo la kuongeza mapato pamoja na kutokuwa na nguvu za kisheria kwa mamlaka kufanya maamuzi ya msingi ikiwemo suala zima la uajiri wa wafanyakazi. Aidha, kamati imebaini kuwa Sekta ya Uvuvi wa Bahari Kuu haijatumika ipasavyo, kiasi cha mamlaka kutegemea zaidi mapato yanayotokana na usajili wa meli za nje kupitia mauzo ya leseni pekee.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa ni muda mrefu sasa tangu mamlaka hii ianze kufanya kazi kwa mfumo wa makubaliano ya mpito (*Interim Agreement),* ni vyema serikali ikawasilisha Barazani Sheria ya Mamlaka hii kwa ajili ya kuridhiwa, na iwapo kuna changamoto katika utekelezaji wake, serikali ifikirie namna ya kuzitatua na hatimae kuiwezesha Mamlaka kufanya kazi kwa mujibu wa sheria. Aidha, kamati inazishauri serikali zote mbili kuzipitia upya kanuni za mamlaka, ambazo kimsingi mabadiliko yake yameibua changamoto mpya ya kupungua kwa meli na mapato kwa kiasi kikubwa sana.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa, kwa niaba ya Kamati ya Bajeti napenda kutoa shukurani za dhati kwa taasisi zote za serikali zilizoshirikiana na kamati wakati wa kutekeleza majukumu yake, pamoja na wadau wote walioalikwa na kufika mbele ya kamati katika kipindi chote cha kazi za kamati, kwani michango na maoni yao imekuwa ni msaada mkubwa katika kutekeleza majukumu yetu ya kuisimamia na kuishauri vyema serikali. Kamati pia inasisitiza serikali kupitia watendaji wake, kusimamia suala la nidhamu ya matumizi ya fedha za umma, ili Bajeti ya Serikali itekelezwe kama ilivyoidhinishwa na Baraza hili tukufu na hatimae kuimarisha uchumi wa nchi hii na ustawi wa watu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu ya kamati. Sasa naomba kwa heshima kubwa sana, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, wa Kamati ya Bajeti kwa ripoti yako. Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na imeungwa mkono, majadiliano yanaendelea. Mpaka sasa nina wachangiaji wanne, kwa hivyo nawaomba wale ambao wanahitaji kuchangia ripoti hii walete maombi yao. Kwanza naanza kumwita Mhe. Shehe Hamad Mattar mchangiaji wetu wa mwanzo, atafuatiwa na Mhe. Asha Abdalla Mussa na Mhe. Bahati Khamis Kombo ajiandae.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii ili niweze kuchangia kidogo kwa sababu mimi ni mjumbe katika kamati hii, lakini naongezea nyama tu kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kuniwezesha kufika hapa nikiwa salama, namtakia Rehma na Amani Mtume wetu Muhammad (*S.A.W*) pamoja na wazazi wangu waliotangulia mbele ya haki.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kuchangia hotuba hii kwa ufupi sana katika Kamati yetu hii ya Bajeti, kwanza kumshukuru sana na kumpongeza mwenyekiti kwa uwasilishaji wake. Pia sina budi niwashukuru wale wote ambao walishirikiana na sisi kwa pamoja katika kufanikisha kazi hii tuliyopewa na Baraza na tukaweza kufanikisha hadi leo tunaileta mbele yenu hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli wadau ambao walifika katika kamati hii walitupa msaada mkubwa sana, kiasi ya kwamba walitoa dukuduku zao walikuwa wakiona kwamba ile michango yao wanapoitwa hapa katika kamati mbali mbali haina maana au haisikilizwi. Lakini tuliwaahidi kwamba michango yenu hii

tutaipeleka mbele ya serikali ili ione kwamba inaleta tija katika serikali yetu. Kwa sababu mtizamo wao walikuwa wanaonesha kwa dhati kwamba wanachangia na wanaonesha njia gani serikali yetu iweze kufanya, mambo ambayo yataweza kuendeleza mbele maendeleo ya nchi yetu kwa ujumla. Kwa kweli walikuwa na moyo mkubwa sana na wanapaswa kuenziwa na kuona kwamba mchango wao ni mkubwa sana katika serikali hii. Nawapongeza sana kwa kutumia nafasi hii.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwamba ili michango yao iwe na faida basi ni vyema serikali nayo ikayafanyia kazi yale ambayo tumeyatoa humu. Mengi yameshatolewa katika ripoti hii mazuri, changamoto na ushauri. Lakini mimi niende moja kwa moja katika Wizara ya Fedha na Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwenye Wizara ya Fedha na Mipango kwenye suala zima la mapato. Hapa kwenye ripoti imeoneshwa kwamba mapato yaliyokusanywa ni madogo kuliko matumizi, hili ni tatizo kubwa kwa kweli, tutafikia wakati mgumu kama hali itaendelea kuwa hivi, basi itatuwia vigumu katika uendeshaji wa nchi. Kwa hivyo, ni vyema sana serikali ijitahidi pale ambapo pana uwezekano wa kubana matumizi ili kuona kwamba mapato na matumizi yanakwenda sambamba. Ni vyema sana Wizara ya Fedha na Mipango ilione hili, sisi tunajitahidi katika Kamati ya Fedha kuibua vyanzo vya mapato na tumeona mafanikio yake, vyanzo vingi vya mapato vimeibuka baada ya kutumia kamati hii na kweli imeiongezea mapato serikali, lakini bado inapambana na matumizi makubwa.

Kwa hivyo, Wizara ya Fedha na Mipango tujitahidi katika kufanya matumizi yake. Najua yanafanywa kwa nia njema kabisa, lakini pamoja na hayo ifanye maarifa ya kuona kwamba matumizi hayaendi makubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika suala zima la Benki Kuu ya Tanzania *BOT* Tawi la Zanzibar. Kama ilivyoelezwa katika kamati hii, benki hii ni muda mrefu sana kuwepo hapa na inavyoonesha hapa ni mwaka 1966, na ni mwaka ambao nimeanza darasa la kwanza kuanza kusoma mimi Mhe. Mwenyekiti kwa taarifa yako. Sasa hii benki kuwepo hapa Zanzibar ni jambo muhimu sana, kwa sababu nchi bila ya kuwa na Benki Kuu au Vyuo Vikuu bado itakuwa haijakaa vizuri, tunacho chombo kama hiki ambacho kinatumika kwa faida ya nchi zetu zote mbili hizi Tanganyika na Zanzibar kwa kupata Jamhuri hii. Kwa hivyo, ni vyema tuitumie lisiwepo jengo ambalo limekaa tu pale. Jengo lipo na la thamani kubwa sana na lina mambo mengi kama tutaweza kulitumia.

Kwa mfano, wafanyabiashara pale waweze kuitumia vizuri ile Benki Kuu ya Tanzania Tawi la Zanzibar kwa kuweza kushirikiana na serikali pale kuweka dhamana za serikali na hati fungani, walitumie wafanyabiashara ili iweze kupatikana tija zaidi. Pamoja na hayo chombo hiki ili kiweze kufanyakazi vizuri ni vyema kutoa taarifa vile ama kujulikana kwake, kwa sababu watu wengi wapo jengo lile wanaliona hawajui matumizi yake. Kwa hivyo, naomba sana Benki Kuu iwe na vipindi maalum ili kuona ni namna gani inavyofanyakazi hapa Zanzibar kwa faida ya Tanzania nzima, ili na wananchi wetu wa Zanzibar waweze kuitumia na hata nje ya Zanzibar. Nawaomba sana wahusika na taasisi hii ya Benki Kuu ya Tanzania, waweze kulitumia na kutumia fursa hii ya kujitangaza, kwa sababu biashara itangazwayo ndiyo itokayo.

Vile vile kwa sababu ya chombo hiki kinatumika kufanya tafiti mbali mbali, ndio miongoni mwa umuhimu wake, tafiti zinasaidia sana katika nchi ili kujua ni kitu gani kifanyike na faida yake na hasara yake. Chombo hiki kinafanya tafiti mbali mbali ambazo na baadae huzitolea matokeo yake, kwa hivyo tuzifanyie kazi zile

tafiti ambazo zinatoa zisibaki kwenye makaratasi, huo ndio ushauri wangu wa ziada.

Mhe. Mwenyekiti, katika changamoto ya Benki Kuu moja wapo ilisema kwamba, zilioneshwa hapa na maoni yetu tulitoa katika kamati hii, lakini na mimi natoa ushauri wangu kwamba kuna taarifa muhimu ambazo tulipokwenda kutembelea tawi hili la *BOT* Zanzibar, kuna mambo mengine ukiuliza yanakuwa hayapatikani hapa. Kwa hivyo, ni vyema hii Benki Kuu ya Makao Makuu kukitumia ikijua kwamba ni sehemu yake. Hata baadhi ya kumbukumbu kutoka Makao Makuu zikawepo hapa kwa usalama zaidi, kwa sababu linaweza likatokezea lolote katika Makao Makuu kule, lakini kumbukumbu zile zikiwekwa katika jengo lake lile zitakuwa ziko salama. Badala ya kuendelea kuziweka tu pale pale ikitokezea hatari hatuna pakukimbilia. Kwa hivyo, maoni yangu ya zaidi ni kwamba baadhi ya kumbukumbu nazo ziwekwe katika jengo lile pale kwa faida yetu sote.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika suala zima la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Mfuko huu ulipoanzishwa mwaka 1998 ilikuwa ni kwa faida ya wananchi ambao watafikwa na mambo mbali mbali kama majanga ambayo yatahusisha wananchi wa Zanzibar, kufikia hadi kupata wanachama wasiopungua 81,477. Lakini mfuko huu umekuwa ukijitahidi sana kufanya miradi ambayo kwa lengo la kupata faida, ili wale wananchi watakapoutumia mfuko huu uweze kufaidika. Lakini sasa wameonesha kwamba kuna changamoto mbali mbali tulipopita zinawakabili, ikiwemo kukosa watu wengine wa kufanya ubiya nao katika miradi yao.

Kwa hivyo, mimi nishauri kwamba wanapofanya miradi hii kwanza waiangalie je, italeta faida gani kwa nchi hii, isiwe ni miradi tu ambayo inafanywa na baadae tukatafuta kusema, kama hivi sasa majumba yanajengwa, unasema bado wanunuzi hawajatokezea ni kidogo sana na mpaka kufika kukodishwa kwa

bei ya chini kabisa, ukitizama gharama za ujenzi huo ni mkubwa sana kuliko faida inayopatikana. Kwa hivyo, nawashauri sana wanapofanya miradi yao waangalie ni mradi upi utaweza kuleta faida kwa wananchi wa Zanzibar ambao ndio walengwa wakuu hapa.

Changamoto nyengine ambayo niliiona katika Mfuko huu wa Hifadhi ya Jamii, ni pale waliposema kwamba wanakosa mtaalamu msimamizi wa miradi ya uendeshaji. Kwa nini wanafanya miradi na baadae wakakosa msimamizi, hili ni tatizo. Kwa hivyo, ni vyema sana waangalie miradi yote ambayo wanaianzisha ina usimamizi. Kwa mfano, kama mradi ule wa Kiwanja cha Kufurahishia Watoto. Imefika pahali wao ndio waliojenga na wao ndio wanaendesha wenyewe, wafanyakazi ndio wanafika pale kwenda kufanya kazi za uendeshaji wa kiwanja kile, hilo ni tatizo. Kama ule mradi pale basi wawekeze, wamtafute mwekezaji wamkabidhi. Leo inafika pahali wafike Jumamosi na Jumapili waende wakafanye shughuli zile pale watendaji watoke maofisini, hili ni tatizo, hatuwezi kufikia hatua ya namna hiyo. Hili ni jambo ambalo ni vyema tutafute wawekezaji kwa baadhi ya miradi ambayo tumeshafanya, ili waweze kuiendesha.

Mhe. Mwenyekiti, maoni yangu zaidi ni kutokana na kwamba mfuko huu ujaribu kutoka, viongozi watoke nje ya nchi wakaangalie mifuko kama hii inafanya vipi. Nadhani hivi karibuni nilipata taarifa kwamba Mkurugenzi aliwahi kutoka kwenda nchi za jirani huko, ili kuwaona wenzetu wanafanya vipi katika mifuko hii na kuweza kupata faida. Kwa hivyo, ni imani yangu kwamba safari yake hii italeta mabadiliko, ili kuona kwamba wapi tumepiga hatua na wapi tumepungua hatua, ili na sisi tuone kwamba tunafaidika na mfuko huu.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la miradi ambayo inaendeshwa na mfuko huu ni pale wanapokula hasara miongoni mwao, ni pale inapotumia ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kawaida. Kwa kweli roho za binadamu ziko tofauti, ikifika msimu kama huo kama sherehe za skukuu hizo au Jumamosi na Jumapili, wengine wanaona ndio wakati wao ndio msimu wa kupata kutia mfukoni. Ni vyema huu mfumo ubadilike wa kukusanya mapato kwa njia ya kawaida, tutumie mfumo wa mashine ili kuweza fedha zile moja kwa moja kama ilivyoshauri katika kamati yangu hapa iweze kuingia katika mfuko husika moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika suala zima la Tume ya Pamoja ya Fedha ya Muungano hii. Mhe. Mwenyekiti, kwa nia njema kabisa Serikali ya Muungano ndani ya katiba yake hii iliweka kwamba kuwepo na tume ya pamoja kwa mujibu wa katiba yetu kifungu cha 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Hii iliweka kwa nia njema kabisa kukilinda chombo chetu hiki kikubwa ambacho kilikuwa cha Muungano, chombo ambacho kilianzishwa kwa faida ya nchi mbili hizi. Chombo ambacho sasa hivi kuna watu bado wanakikodolea macho kivunjike tu, ili wapate kufanya mambo yao kwa sababu ukivunjika hapa wanasema wachawanye uwatawale na hiki kitu ambacho hakitakuwepo kwa nguvu za Mwenyezi Mungu. Tukilinde na tukitetee kwa nguvu zote.

Mhe. Mwenyekiti, sasa tume hii ya pamoja ilipoundwa, iliundwa kwa kusimamia mambo haya yaliyotajwa humu haya yaliyotajwa humu mpaka kuundwa *secretariat* ya tume, ambayo ndio chombo kitakachosimamia ushauri wa kitaalamu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kwenda kwetu, tume hii kuitembelea tuliona mapungufu ambayo tumeyaonesha humu lakini zaidi

kwamba, kama tume tumeipa kazi na leo ninafanya kazi inatumia juhudi kubwa sana kuwatafuta wadau wengine kupata ushauri, na kuona kitu gani kitaweka vizuri katika malengo yetu tuliyokusudia, leo ushauri ule unaachwa haufanyiwei kazi. Hivi ni kuwapunguza nguvu watendaji ambao tumewaweka pale kuona kwamba hawana maana na chombo kinakuwa na gharama na jengine ni kutokana na hata bajeti yao imeanza kupunguzwa, kama ulianza na 3,000,000 au 5,000,000 sasa wanaendelea na 1,000,000 hili ni jambo litapunguza nguvu ya kufanya kazi. Ushauri wangu kwamba iongezwe bajeti yao ya tume hii ya pamoja ili wafanyakazi vizuri. Lakini na yale mapendekezo yao yafanyiwe kazi ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naona nikifikie hapo nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na kuweza kutoa mchango wangu Ahsante sana.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi nikiwa na mimi ni mjumbe wa kamati hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na utangulizi, kwamba sisi wajumbe wa Kamati ya Bajeti, au hii kamati ya bajeti ni miongoni mwa kamati nane ambazo za Baraza la Wawakilishi na tupo chini ya kifungu cha kanuni ya 106 ya kanuni ya Baraza la Wawakilishi ya mwaka 2016.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tuna masikitiko kidogo hususan mimi mjumbe, kwa sababu tukitizama Baraza, Wenyeviti wa kamati, nikitazama kwenye Baraza katika kamati 8 wanafika wenyeviti 3 tu, ikiwemo Kamati ya Bajeti lakini sisi tumo tuko katika kanuni hii, lakini pia tuna majukumu ambayo yameorodheshwa kwenye kanuni.

Mhe. Mwenyekiti, kati ya majukumu hayo nitazungumzia; kwanza ni kufuatilia na kusimamia na utekelezaji wa mwaka 2017/2018 na nyenginezo. Lakini pia kuna kutoa ushauri wa ujumla kuhusu bajeti ya serikali kwa Baraza na katika kamati za kudumu.

Mhe. Mwenyekiti, nilianza na utangulizi kwa sababu, sisi ni wajumbe wa Kamati ya Bajeti, hatuna Wizara maalum ya kufanyia kazi katika zetu, tuko katika wizara zote pindipo pale tutakapoona au tutakapohitajika kuenda kuhoji kitu, na kukitazama utekelezaji wake ukoje, tunapangiwa na tunakwenda kuufanyia kazi na baadae tunashauri Baraza zima au tunashauri kamati ambayo husika ya Wizara ile. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Baraza lako tukufu wafahamu kwamba kamati hii imeundwa kwa mujibu wa kanuni, lakini pia na majukumu yake yake kwa mujibu wa kanuni hizi.

Mhe. Mwenyekiti, la pili nije kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kati ya majukumu yetu tuliyoyatekeleza tumeenda kuupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na tukakuta changamoto mbali mbali ambazo amezungumzia Mhe. mwenzangu Mhe. Shehe Hamad Mattar. Lakini mimi nije kwenye Miradi hii ambayo wameianzisha kwa kweli nimeona kwamba mfuko huu unatumia fedha za wanachama kwa ajili ya kutekeleza miradi na ambayo, miradi hii inaweza kukusanya mapato mengi, na kuweza kuendesha mfuko huu. Lakini cha kusikitisha kwamba tumeona, tulipokwenda kutembelea mfuko huu, tumeona kuna Mradi wa Mnara wa kumbukumbu wa miaka 50 pale uliopo Michenzani.

Kwa kweli tumesikitishwa sana tulipoona mapato na matumizi. Tukiangalia mapato, toka kuanza mradi ule ukitazama kiambatanisho kwenye ukurasa wa 51, utakuta mapato ni kidogo

lakini matumizi ni mengi. Naomba sana serikali kupitia Mfuko huu wa Hifadhi ya Jamii, itafute au ibuni mbinu ya kutafuta Wawekezaji kufunga nao ubiya ili kuhakikishwa kwamba unaendeshwa mradi uli ili tuweze kupata mapato zaidi.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini nije kwenye changamoto nyengine; Mfuko wa hifadhi umejenga Viwanja vya kufurahishia watoto, vikiwemo Kariakoo na kwengineko, lakini kwa sasa sote ni mashahidi, Fumba kumejengwa majumba lakini pia kwa sasa kila inapofika siku ya Ijumaa, Jumamosi, Jumapili watoto mpaka watu wazima wanakwenda Fumba. Katika viwanja vyetu hivi kwa kweli kwa muda ambao kwa miaka iliyopita ikifika siku ya jumamosi na jumapili utakuta watoto wengi wapo katika viwanja vile lakini kwa sasa tunaona kwamba watu wote wanakimbilia Fumba. Naomba sana Mfuko huu wa Hifadhi ya Jamii na serikali kwa ujumla ikae itizame mbunu mbadala na kuona kwamba ile hali ya mwanzo inarudi kama kawaida katika viwanja hivi vya kufurahishia watoto.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye kiwanda cha Makonyo, tulitembelea katika kiwanda cha makonyo kilichopo Pemba na tukakitembelea kiwanda kile tukaona changamoto nyingi, lakini baadhi yake ya changamoto hizi tumeona kwamba mashine zilizofungwa toka kipindi kilichoanza kiwanda kile toka mwaka 1982 kama hivi, kwa kweli mashine zile ndizo zinazotumika mpaka sasa lakini tumezikuta zile mashine chakavu, na inafika pahala kiwanda kinasimamisha kazi zake kutokana na uchakavu wa baadhi ya mashine. Kwa hivyo naomba sana taasisi husika ambayo inashughulikia masuala mazima ya kiwanda cha Makonyo basi kione kwamba kinakwenda kukagua zile mashine na kuona kwamba kufanya ukarabati baadhi ya mashine zile, ili kiwanda kiweze kufanyakazi zake ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine, kuna baadhi ya wafanyakazi tumekuta kwamba wanafanyakazi lakini inafika pahala wanazalisha mafuta, na baadae mfanyakazi akitoka anaiba mafuta anaondoka nayo kwa kweli inafika pahala mpaka ikifika mwezi, mafuta yale ukijagundua ni mafuta mengi ambayo yameibiwa katika kiwanda kile. Naomba sana sana wafanyakazi pamoja na wizara husika ambayo ni Wizara ya Biashara na Viwanda, basi iende ikachunguze na ikichunguza ikigundua kama upotevu huo wa mafuta upo, basi ihakikishe kwamba inatafuta mbinu mbadala na kupanga mikakati, na kuhakikisha kwamba kile kinachozalishwa pale basi nakibakie na kiendeleze katika kiwanda kile.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye changamoto katika Hospitali ya Abdalla Mzee. Kwa kweli tumekwenda kutembelea katika Hospitali ya Abdalla Mzee lakini pia cha kusikitisha kwamba, katika Hospitali ili nzuri kubwa, lakini wafanyakazi wake ni kidogo, kwa sasa hospitali ile kuna wafanyakazi 196, na tuliambiwa kwamba mahitaji ya wafanyakazi ni 500, kwa kweli upungufu uliopo ni wafanyakazi wengi hawapo. Na changamoto kubwa kama tulivyotangulia kusema hapo mwanzo kwamba baada kuajiriwa hawa wanapopelekwa katika hospitali ile baada ya kukaa muda miezi 2 au 3 wanaomba uhamisho wanarudi Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana serikali pamoja, na kupitia Wizara husika ikufanye mchakato na kuweka mikakati kwa wale ambao wanaajiriwa na kupelekwa katika Hospitali Abdalla Mzee, basi madamu wamefunga mkataba ya uajiri, basi waweze kufanyakazi eneo ambalo wanapangiwa kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia tumevikuta vifaa ambavyo vipo, vifaa hivi vimekaa kwa muda mrefu na baadhi ya wafanyakazi wa Hospitali ile, wametwamia kwamba vifaa vile vikikaa kwa muda

mrefu sana vinaweza vikaharibika. Lakini hali ambayo itaweza kupelekea kwamba vifaa vile vitakapoharibika, matengengezo yake yatakuwa makubwa sana. Naomba sana serikali iwapeleke wataalamu ili viweze kufungwa vifaa vile na viweze kutumiwa na wananchi wa maeneo ya Pemba waweze kufaidika na huduma za afya.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa haya machache nimalizie kwa kusema kwamba, nawaomba sana wajumbe wa Baraza hili tukufu waweze kuchangia ripoti hii na waweze kuinga mkono kwani wafahamu kwamba sote ni wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, lakini pia na kamati zote zimeundwa kwa mujibu wa kanuni.

Mhe. Mwenyekiti nikushukuru sana sana naiunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nichukue fursa hii kwa kumpongeza sana sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa jitihada zake kubwa anazozichukua kuona kwamba siku hadi siku mapato yanaongezeka.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende moja kwa moja katika ukurasa wa 5 unaosema Tathimini ya kamati juu ya taarifa juu ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali Robo ya Nne April Juni, 2016/2017 lakini katika namba 5 iliyopo ukurasa wa 6.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tulibaini kwanba umuhimu mkubwa wa kuwepo kwa kodi wa miundo mbinu. Kwa vile ukusanyaji wa kodi unaridhisha kwa kipindi cha miezi 3 kodi ilikusanywa ilifikia jumla ya Tzshs. Bilioni 6.18 sawa na asilimia 98 la lengo. Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana sana Mhe. Waziri lakini pia na watendaji wake wote ambao wameweza kukusanya mapato haya.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea niende kwenye maoni na ushauri wa kamati. Kwa kuwa mapato yanakusanywa na serikali ni madogo ukilinganisha na matumizi inaashiria serikali kuweka vipaumbele katika matumizi yake ili kuweza kuwa na bajeti yenye uhalisia na yenye kuweza kutekelezeka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naishauri sana serikali kwamba tuangalie bajeti zetu na hasa katika zile wizara ambazo zina matumizi makubwa kwa mfano, kwenye bajeti ya Wizara ya Afya. Mhe. Mwenyekiti, kipindi kilichopita Wizara Afya tuliipa asilimia mia moja na Mhe. Waziri alitwambia kwamba yeye zinamtosha, lakini kwa bahati mbaya fedha ili haitoshi kulingana na zile kazi ambazo zimo katika Wizara Afya. Lakini vile vile katika Wizara ya Mawasiliano matumizi yao ni makubwa kulinganisha na yale mambo ambayo wanayo katika Wizara zao. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Waziri wa Fedha mara hii katika bajeti yao hawa tuwangalie sana ili tuwakuzie kidogo ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea niende moja kwa moja katika maoni na ushauri wa kamati ambao unatoka katika tathmini ya robo ya kwanza ya utekelezaji wa bajeti ukurasa wa 9. Mhe. Mwenyekiti, hapa tulitoa maoni na maoni haya tulisema kwamba katika nambari 6 kuhusiana na mwenendo wa uchumi wa Zanzibar.

Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuangalia kwa karibu viashiria vya uchumi kama vile pato la taifa *GDP*, mfumko wa bei, mwenendo wa biashara, mauzo ya ndani na ya nje. Ukuaji wa deni la taifa na ukuaji katika sekta mbali mbali za uchumi. Kwa kuwa viashiria hivyo ndivyo vinavyotoa sura halisi ya ukuaji wa uchumi na kuyumba kwa viashiria hivyo kuna athari kubwa katika maendeleo ya jamii hasa katika kupunguza mapato

ya serikali. Kwa hivyo, kuongeza nakisi ya bajeti na hatimaye kushindwa kutekeleza vipaumbele vya miradi ya maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana serikali sasa hivi tuangalie jinsi gani ambayo ile miradi yetu tutaweza kuitekeleza. Kwa sababu tumeona kwamba siku hadi siku tunakuwa na miradi mikubwa lakini hatima yake hatuimalizi miradi ile na tunaanza miradi myengine. Vile vile tunaongeza deni kwa wenzetu walio karibu na sisi kutukopesha zile fedha zao.

Mhe. Mwenyekiti, ni vyema tunapoanza miradi tukamaliza na badala yake ndio tukaanza miradi mwengine, kuona kwamba wale wenzetu watafurahishwa sana na kuona kwamba wametupa fedha ile ya mkopo lakini fedha zile zimetumika vizuri na mradi ule ambao tumekusudia umemalizika.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika maoni yetu ambayo maoni haya tunaipongeza sana serikali kwa kuweka kiwanda cha kusarifu mazao katika Wilaya ya Chake Chake eneo la Pujini. Mimi naipongeza sana serikali kwa jambo hili, jambo hili ni jema. Lakini pia naomba na wilaya nyengine waweze kuwekewa kiwanda kama hiki ili wananchi na wao waweze kufaidika zaidi na pia kuongeza ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika changamoto ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Mheshimiwa tunaomba sana kwamba changamoto hii ambayo hivi sasa inaendelea changamoto yenyewe ni kwamba kukosekana kwa utaalamu, usimamizi na uendeshaji wa miradi iliyowekezwa na Mfuko hali inayopelekea mradi kama wa Kiwanja cha Watoto Uhuru kuendeshwa na wafanyakazi wa kawaida wa Mfuko ambao kimsingi si weledi katika kuendesha miradi ya namna hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali ichukue jitihada za makusudi ili kuona kwamba changamoto hii imeondoka kwa haraka, lakini vile vile tunaomba kwamba kuna changamoto ambayo ni nambari 5 kutokuwepo kwa mfumo wa kisasa katika ukusanyaji wa fedha kutoka katika miradi ya viwanja vya kufurahishia watoto Kariakoo na Tibirinzi kule Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, mapato yanapotea na yanapotea kiasi kikubwa sana katika viwanja hivi kutokana na ukusanyaji mbovu ambao unakusanywa na baadhi ya wafanyakazi. Tunaiomba serikali ifanye jitihada zake kuona kwamba hawa wanakusanya mapato haya kama ilivyo mfumo wa sasa hivi, mapato ni mengi unapofikia wakati lakini utakuta mwisho wake kinapokuja kuharibika kiwanja tunataka zile fedha ambazo tutengenezee kile kiwanja basi zitakuja kutushinda na baadae itakuwaja kuwa kama Meli ya MV. Mapinduzi II hatima yake tuongeze deni hadi deni kutoka kwa wenzetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende moja kwa moja katika changamoto ya Mamlaka ya Uwekezaji, Ukuzaji Vitega Uchumi. Hapa kuna changamoto nambari 2 ambayo tumeiweka, Mamlaka kukosa usafiri wa gari kwa muda mrefu ambao unahitajika kwa shughuli za ufuatiliaji wa maendeleo ya miradi mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, hili si jambo jema kama wenzetu hawa wanafanya kazi lakini hawana usafiri. Naiomba serikali watu hawa wapatiwe usafiri ili waweze kufanya kazi zao ziende vizuri na tija iweze kupatikana katika uwekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, nikimalizia kamati imebaini kwamba, kwa miradi mingi ya uwekezaji katika sekta ya uvuvi hali inayorejesha nyuma wawekezaji wa ndani na nje katika sekta hii. Kamati imepatiwa taarifa hiyo na Mamlaka ya ZIPA, kuwa jumla ya

miradi nane inayohusiana na shughuli za uvuvi iliripotiwa kukwama.

Mhe. Mwenyekiti, miradi hii nane naomba sana ishughulikiwe ili vijana wetu waweze kupata ajira. Miradi hii nane siyo miradi kidogo, kama ingalikuwa miradi hii ingeweza kufanya kazi vizuri basi tunaamini kwamba vijana wengi wangeweza kujiajiri na wengine vile vile kuajiriwa ni vitega uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa vile mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii naunga mkono ripoti hii ya Kamati ya kudumu ya bajeti ya Baraza la Wawakilishi kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, nakushukuru Mhe. Bahati Khamis Kombo kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Abdalla Ali Kombo atafuatiwa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na Mhe. Miraji Khamis ajiandae.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako nakushukuru sana, kwanza naiunga mkono ripoti hii mia kwa mia na ku-*declare* kwamba mimi ni Mjumbe wa kamati hii lakini kuna mambo tu kidogo nitaongezea.

Mhe. Mwenyekiti, naanza kuzungumzia habari ya Mangapwani, Mangapwani kunatakiwa kujengwa *Depot* na ZURA kitu ambacho ni kizuri na kitatusaidia sana kuondosha hii adhabu ya mafuta na vitu vingine vyote. Lakini kidogo nina wasiwasi kwamba tayari sasa hivi Mangapwani kuna makampuni katika maaeneo hayo ingawaje wenyewe wanasema kwamba hayataathiri, lakini mimi wasiwasi wangu kwamba yataathiri. Makampuni haya tayari yameshapewa hati na serikali hii hii, sasa sijui Waziri akija atatwambia nini kama kutakuwa na uwezekano wa kutanua eneo letu kwa watu hawa ambao wamewahi na wako

kisheria. Lakini pia mimi ningeliomba tuwe na mipango ya baadae wakati mwingine hata kama hatuna pesa kwa kuepukana na haya, si kwa hili tu na kwa mengine yote hilo ni la mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la pili katika mazungumzo yetu na kamati tofauti tulikuwa na kamati ya hawa hawa ZURA na bahati nzuri tulikuwa na Wajumbe wa Bodi, katika mazungumzo yetu likatajwa neno la kununua meli ya mafuta, lakini kama nilivyozungumza mapema tayari tunajitayarisha kwenda kujenga *depot* huko Mangapwani ningeisihi tu serikali kwa nia nzuri, tujenge *Depot* lakini pesa za kununulia meli tukajengee *depot*. Tusifanye mambo mawili ambayo uwezo nayo hatuna na baadae tukaja tukakwama njiani. kwa hivyo, naisihi tu serikali hizi pesa za kununulia meli wacha twende Mangapwani tukaongezee kujenga *Depot*. Huo ndio ushauri wangu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kuna ununuzi wa karafuu hapa kidogo kuna watu wanaweza wakasema huyu bwana vipi, lakini pia na ushauri hali ya ununuzi wa karafuu hasa Pemba kidogo una matata matata. Pesa zimetumika nyingi lakini hii *system* haifahamiki vizuri, mimi nigeshauri kwa misimu ambayo inakuja wakulima sasa tufate wenzetu kama Bara wale wa korosho, walipwe kupitia benki. Ili angalau mradi serikali na wananchi wenyewe wajue zile pesa zimekwenda wapi na hii pia itasidia wananchi wenyewe kuwa akiba yao ambayo iko salama.

Kwa hivyo, nashauri tu kuanzia msimu unaokuja sasa pesa za ununuzi wa karafuu tuna benki ya PBZ benki inayoaminika wanaweza wakaamua zende kwenye uislamu wale wachapa nanihii wakaamua twende huku kwenye riba lakini angalau zipitie kwenye akaunti za benki. Kuliko kupiga foleni na mikoba ya ukili na kapu mwisho wa msimu pesa haifahamiki iko wapi nani kapata wakulima wanaanza kulalamika, wengine wamepita huku. Kwa hivyo, hiyo nainasihi serikali ama naiomba wizara tufanyeni

hivyo kwa manufaa ya wananchi wenyewe lakini na kwa manufaa ya serikali yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni takwimu, nimeshaulizia siku nyingi sana kwa wizara hii na kumwambia Mtakwimu Mkuu atusaidie angalau tujue kwa msimu ukisha tumepata nini sisi serikali na wananchi wamepata nini. Kwa maana hiyo wanasema kuwe na *cost benefit* hizi gharama zifanyike, tunatumia vitu vingi tunakopesha wakulima, tunatumia magari, kila kitu kinafanyika sasa gharama ambazo zinatumika mwisho wa msimu inakuwa hatuzijui. Sasa naiomba serikali hasa Mtakwimu Mkuu atusaidie gharama ambazo zinatumika kwenye uzalishaji wa karafuu tufahamu kwa tani moja mpaka tunakwenda ughaibuni tukirudi serikali imepata kiasi gani, mkulima amepata kiasi gani, tuna akiba gani ya msimu unaokuja kuanzisha tena? Isiwe hadithi ya goa faida juu kwa juu lakini hakuna kinachofahamika.

Mhe. Mwenyekiti, nazungumza haya kwa sababu tayari tumeshatumia zaidi ya bilioni mia moja na kumi na mbili bilioni na nadhani wananchi wakati mwengine wangekuwa wanajua hizi wakisikia bilioni ngapi wangesema duu kumbe bilioni moja maana yake milioni elfu, sasa kwa mwananchi wa kawaida atajua kumbe pesa nyingi zimetuka. Sasa tumeshatumia zaidi ya bilioni mia moja na kumi na mbili kwa msimu huu, lakini je serikali imepata nini? sasa Mtakwimu Mkuu miye ningemuomba atufanyie hizi hesabu na atupe kutwambia tumepata faida hii na tumepata hasara hii. Naiomba sana serikali itusaidie kwa hili.

Mhe. Mwenyekiti, jengine katika kukaa na wizara au Shirika la ZSTC kuna kitu kimoja kidogo kinanipa mashaka, tunazungumzia *project* au mradi wa bilioni ambazo tumeshazitoa kwa msimu huu tu, lakini huko ughaibuni ambako tunakwenda kuulizia masoko kuna wafanyakazi watatu wa kihindi mmoja Dereva mmoja Muhudumu na Mmoja Muhasibu. Sijui nitumie lugha gani ya

kwamba nisije nikakashifu au kutukana lakini wafanyakazi watatu wako ughaibuni ndio tunawategemea hawa kututafutia *information* za karafuu zetu. Mmoja Mhudumu mmoja Dereva na mmoja Muhasibu.

Mhe.Mwenyekiti, Zanzibar sasa hivi tuko 1.5 milioni kuna watu nina uhakika hawapungui kumi Unguja na Pemba wenye aidha *Certificate Diploma* za mambo ya uchumi. Tunachokosa nini kwenda kuweka watu wetu ughaibuni wakatupa *information* za uhakika za kweli, kweli tumekosa serikali kwenda kutafuta watu kukaa ughaibuni wakafanya kazi ya nchi yao, biashara ambayo inakwenda bilioni bilioni kwa msimu tunakwenda kuweka wahudumu, sitaki kutukana kwa sababu uhudumu nao ni kazi lakini sote tunaifahamu kazi yake, dereva tunaifahamu kazi yake, huyo mhasibu tunaosema mhasibu wetu, serikali mengine kidogo tubadilike. Zanzibar tuna watu milioni moja na laki tano, tutafuteni watu wetu waende huko. Hii ndio ile bwana nna mtoto yuko huko kazaliwa lakini miaka mitano hujenda ndio haya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba serikali na hapa itusaidie, tumetembelea tena Pemba tumekwenda skuli ya Madungu kuna mradi wa skuli nane hivi bilioni thamanini na nne zimetolewa mkopo, katika walipaji wewe umo mwenyekiti na mimi nimo humu Barazani tumo themanini na sita jumlisha zile pesa tunazokatwa kila mwezi inabidi tuzilipe.

Maana wengine labda hua hamjui, sasa katika skuli hii yalofanyika na niliyoyaona maana yake ni kwamba yamefanyika na naomba mwenyekiti kama kuna uwezekano mwanasheria anaweza akatusaidia siku hizi TV iwekwe ioneshe yale tulokwenda na wananchi waone, tumekwenda Madungu skuli imejengwa juzi hizo taa unazoziona ndio matundu ambayo yako kwenye skuli. Hivi unavyoziona taa ndiyo Madungu yale matundu

yalivyo. Tumetumia 84 bilioni pesa ambazo na mimi nalipa na wewe umo.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali tuwe wasimamizi wazuri, lakini hii hotuba kwamba tuwe wasimamizi wazuri haitoshi mimi ningewaomba ZAECA wanatutangazia kwenye radio hebu waende kule Pemba wakatizame hali halisi ikoje, maana kuna mambo mengine fitina ndio nikasema kwamba sasa Mwanasheria kama kuna uwezekano tubadilishe mambo tukizungumza mambo kama haya yaoneshwe kwenye *screen* sote tuone na wananchi waone hali mbaya. Kwa hivyo, ningeomba wale ndugu zetu ZAECA lakini pia wizara ya Elimu ndio wasimamizi wakubwa wa majengo haya, lakini cha kushangaza kuliko yote huyu huyu Mkandarasi sijui nani huyu, tumetembelea Wizara ya Kilimo tukamkuta tena kule Saateni, jamani hivi ile nyimbo moja inasema siyo bure labda umerogwa. Tokea juzi hapa watu wanazungumzia habari ya meli, sitaki kusema mengi kuhusu meli lakini kama umeuziwa baiskeli haina mnyororo wala tairi tuyaache.

Mhe. Mwenyekiti, tunazungumzia habari ya Uwanja ya ndege *one twenty million dollar* na juzi tumetoa nyingine zimeshakwenda, na masuala mengine jamani hatukomi bakora hizi? Mtu yule yule anapewa tena kazi nyingine sasa mimi ningeomba kama kuna mtu anawapenda watu wa namna hii wakajenge nyumba ya kwake. Kama ana kwao mjini ajenge mjini na kama ana kwao shamba akajenge kwao shamba lakini asituingilie kwenye mambo ya serikali aibu. Kwa hivyo Mwenyekiti, nazungumza haya kwa unyonge sana, sasa kuna masuala mengine nayo kidogo yanaudhi tumekwenda Pemba tena Madungu kwenye eneo la skuli ya Madungu humo humo ni serikali hiyo hakuna mtu mwingine wala hakuna mtu anaeweza akenda akajenga mle, kuna mtu akenda akajenga sasa serikali au wananchi wanamlipa.

Mhe. Mwenyekiti, wanafunzi wetu wanalala mle, wanasoma mle sasa analipwa jamani niliwahi kusema safari moja hii ni kibafta maana kibafta mnatafuna mihindi hivi kibafta mbili futa sijui nini futa, unampa ndo tayari hapo keshakufuta. Kinaitwa nini Kibafte sasa ndio mchezo huu jamaa hii serikali tufikeni pahala hizi pesa hizi kule kwetu tunasema Mchanga na checheche pesa hizi hazina hesabu. Serikali tuwe macho tunaumia tumekwenda tena Mbweni hapa tunazungumzia uchumi ZSSF inajenga majengo ya kisasa ya kukopesha huku kuna majengo ya skuli ya Mbweni katikati kuna maeneo tayari watu weshachukua, maana yake huku ujenge jengo huku ujenge majengo katikati kuwe na ma-*gap* ukiuliza Mheshimiwa anakutania tu Sheikh Rashid, sasa itakuwa mbaya hiyo jamani tujitahidini hali si nzuri ya matumizi tumekaa hapa viongozi tumechaguliwa hizi tai tukienda huko Mheshimiwa vipi uheshimiwa maana yake ujiheshimu na wewe. Kwa hivyo jamani tuheshimuni wananchi tunaopewa madaraka ya kuongoza wananchi wetu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Abdalla Ali Kombo kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na atafuatiwa na Mhe. Miraji Khamis na kama muda utaruhusu basi Mhe. Suleiman Sarahan ajiandae.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kunipa nafasi hii. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa asubuhi hii kuchangia ripoti hii muhimu sana ya Bajeti katika nchi yetu ambayo inalenga mambo mengi sana na dira na mpango wa nchi yetu.

Lakini kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kazi yake nzuri sana kwa kujitahidi sana kuongoza katika wizara hii mama ambayo inaendesha mambo mengi sana katika nchi yetu.

Lakini niipongeze Kamati yetu ya Bajeti na nimpongeze sana Mhe. Mwenyekiti Mohammed Said Mohammed kwa kazi yake nzuri na ripoti yake nzuri aliyotutelea hapa. Lakini pia niwapongeze Wajumbe wote wa kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianzie hapa katika ukurasa wa 61 changamoto yetu ya mradi huu wa *Airport Terminal II.* Lakini katika maelezo mengi katika ripoti yetu imeeleza kuwa changamoto hii kwa kweli inasikitisha kidogo, fedha nyingi sana serikali imeongeza katika mradi huu karibu bilioni 58 zimengezeka. Kwa hiyo, mimi niombe sana Mheshimiwa kwa sasa hivi kupitia Wizara ya Fedha na serikali yangu tujitahidi sana tumalize *Airport* hiyo, ili tuweze kupata maendeleo makubwa na tufanikiwe katika mradi ule hasa kwa upande wa maduka na madege mengine makubwa kuja ili tupate kodi kubwa tuweze kuendesha nchi yetu na maongezeko ya thamani ya pesa izidi.

Lakini niendelee kwenye huu ukarasa wa 8 wa ripoti ya kamati hii upande wa *ZIPA* Mheshimiwa. Upande wa *ZIPA* kwanza niwapongeze sana *ZIPA* kwa jitihada zao kubwa na kwa kujitahidi sana kuwakaribisha wageni. Kwa sababu wageni wanapokuja Mheshimiwa wanafikia hapa *ZIPA* na hichi kitengo kiko chini ya Wizara ya Fedha lakini niseme wawekezaji wakija wanaweza kufikia hapa na kuangalia wanaendea kuekeza nini.

Lakini ukiangalia kwenye ripoti ya kamati inasema wawekezaji *ZIPA* kubaini kuwa kipindi cha Januari hadi Juni 2017 miradi imefikia kumi na moja yenye thamani ya dola za Kimarekani milioni mia moja thamanini na sita milioni. Mhe. Mwenyekiti, hili sio jambo dogo hawa wawekezaji wametuamini sana kwa serikali yetu kuja kuwekeza fedha kama hizi dola milioni mia moja na thamanini na sita, ni fedha nyingi sana. Kuna nchi zinatafuta wawekezaji kama huu waende watu lakini wawekezaji wanakuja

Zanzibar kwa imani yetu, utamaduni na amani iliyokuwepo mimi nashukuru sana.

Niipongeze sana serikali yetu kupitia wa Rais wetu Mhe. Dkt Ali Mohammed Shein kwa kujitahidi sana kuimarisha amani, utulivu na umoja wa Wazanzibari wote. Kwa hivyo, nimpongeze sana kwa juhudi hizo na wageni hawa wanakuja kwa kuonesha kuwa Zanzibar ni huru na amani iliyoendelea katika kisiwa hichi. Kwa hivyo, nipongeze. Lakini kuna miradi sita Mhe. Mwenyekiti, ya dola za Kimarekani milioni ishirini na tisa, jambo sio dogo milioni ishirini na tisa kwa miradi sita fedha nyingi sana. Lakini Mheshimiwa kuna tatizo moja hapa wametwambia ndugu zetu hawa wa Kamati ya Bajeti changamoto kubwa ya wawekezaji kukuza kitega uchumi Mheshimiwa inakuja hapa kutokamilika kwa huduma hii *One Stop Centre* hii muhimu sana kwa wageni wetu. Kwa sababu hapa ukiangalia huduma hii kama haipo Mheshimiwa kuna watu wanakuwa kama *agent* wa nchi hii kutaka uwekezaji. Ukitaka kuekeza lazima uwaone wao na ukiwaona wao wanatia kamisheni zao mambo mengi wanaongeza wakati jambo hapa linakuwa dogo tu kupewa kiwanja na muekezaji akaekeza.

Mheshimiwa Mjumbe aliemaliza pia kasema suala hilo hilo na ukiangalia wanatoa mwanya pia kutoa rushwa kwa ajili hii ya *One Stop* kwa nini hii tusifungue hii *One Stop* ikawa *open*, kwenye mitandao ukawa unaona muwekezaji akishuka tu tunajua anakwenda Afisi fulani nimalize kazi yangu haina haja ya kupitia kwa mtu yoyote, iwe *very simple* maana yake. Sasa naomba hii nia nzuri na nia njema ya *ZIPA* kuanzisha hii *one stop centre* kwa nini tunachelewa mimi naomba ifanyiwe haraka vyombo vya habari kuwapa taaluma wananchi, mitandaoni wakiwekezaji wakishuka waende pale wakitoka *Airport* tu wende pale wasihangaishwe naamini kuna wawekezaji wanataka kuwekeza lakini bado *process* hazijakamilika. Kwa hivyo mimi naomba

Mkurugenzi wa *ZIPA* ujitahidi sana kuweka wazi sisi tunahitaji wawekezaji waje ndio kodi yetu tunapata hawa wanachangia karibu asilimia arubiani ya pato la taifa letu uwekezaji huu kama utafanyika.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia ukurasa wa kumi na nane wa ripoti hii ya Kamati hapa nisikitike tena sana kama mimi Muwakilishi wa Jimbo la Mtoni nisikitike kwa upande wa Zanzibar kuwa na tatizo kama hili Mheshimiwa, ukiangalia hapa muwekezaji kaja hapa Zanzibar anataka kuekeza bilioni mbili dola, si masihara bilioni mbili kuzitia hapa katika uwekezaji wa mredi mkubwa huu wa hoteli, niseme muwekezaji huyu anataka kidogo aongezewe kipande kidogo cha eka karibu eka 220 aongezewe tatizo liko hapa. Ukiangalia hapa muwekezaji huyo akiweza kuwekeza kwanza ajira itafunguka kwetu, wananchi wetu watapata ajira.

Sisi shida yetu kubwa ni ajira na shida nyengine kubwa tumeshapata mapato kwenye uwekezaji huu, lakini ukiangalia pia nisikitike sana Mheshimiwa ukiangalia huyu muwekezaji anaambiwa alipe mnazi mmoja shilingi milioni nne, mnazi mmoja shilingi milioni nne fidia gani Mheshimiwa umesikia wapi? Kitu cha kusikitisha sana huu mradi kama huu wa *Penny Royal* hawa wametuandikia utakuwa mradi *best* katika Zanzibar lakini unaambiwa mnazi mmoja tuulipe milioni nne fidia mnazi wa dhahabu huo.

Hebu tukae chini tujiulize jamani huyu muwekezaji anatufikiria sisi vipi, sasa kama kuna minazi mia pale itakuwa milioni nne mara mia milioni ngapi hizo, sasa mimi nashangaa vitu kama hivi ni aibu, wako watu wataalam wa kilimo wanajua mnazi thamani yake. Mimi najua mnazi mmoja sana shilingi elfu arubaini, hamsini alipwe, minazi yake mingapi, kumi ilipwe kwa sababu huyu muwekezaji hamsaidii mwananchi tu, mpaka sisi ajira tutapata kuwapatia wananchi wetu. Sasa mimi nasikitika sana

mradi kama huu ukiondoka ni hasara Mheshimiwa tuangalie, *ZIPA* naomba waangalie Wizara ya Fedha waangalie kuna watu hawana nia njema na nchi hii.

Sasa watu kama hawa Mheshimiwa wachukuliwe hatua Serikali iingilie kati, hapa hapa fidia ukitizama *Airport* walipolipwa fidia watu mimi nilikuwa mjumbe wa Kamati fidia inapangwa nyumba hii thamani yake milioni ishirini, nyumba hii thamani yake milioni kumi, huwezi kuandika fidia yake milioni mia nne nyumba yako haifiki . Wako wataalam wa ujenzi, wako wataalam wa mazao ya kilimo, milioni nne mnazi gani hebu mimi nataka nifahamishwe leo mnazi huo uko vipi Waziri anifahamishe. Inasikitisha sana milioni mbili mtu anakuja kuwekeza, mradi *East Africa* nzima pengine utakuwa upo hapa sie tunauwacha mradi kama huo. Hata Rais wetu ana nia njema anataka wawekezaji waje kuja kuwekeza na wanakuja mungu katujaalia neema hii anatupa.

Kwa hivyo mimi naomba sana Mheshimiwa tuangalie kwa huu mradi *best of Zanzibar Penny Royal* tusiwaache wawekezaji tuwape nafasi hizi ekari mia mbili sisi tuwape wajenge na hii minazi Serikali a watu walipwe waondoshwe wananchi ili mradi uje tutafaidika sote kutoka Pemba, kutoka hapa Zanzibar kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watakuja wananchi kwenye mradi huu. Kwa hivyo mimi naomba tuendeleze haraka Mheshimiwa ripoti hii ya kamati mmetuletea lakini tuifanyie kazi kwa haraka sana.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye mfuko huu wa Hifadhi ya Jamii *ZSSF* ripoti ya kamati ukurasa wa kumi na tatu Mheshimiwa, kukosekana kwa soko la majengo ya uwekezaji Mheshimiwa mfuko huu. Hizi pesa za wananchi zinakusanywa kufanyiwa biashara leo inakosekana masoko vipi, mimi mpaka leo sifahamu hii ripoti mmetuletea lakini ukisema thamani yamajengo au nyumba mpaka leo thamani yake kubwa tena wananchi wanataka

sana.Sasa hapa tuangalie tuweke nafuu kupitia benki wananchi wakopeshwe nyumba hizi kidogo kidogo ili waweze kulipa kwa muda wa awamu, ukisema *International Housing* mimi nilikuwa mjumbe wa kamati hapo Tanzania Bara nilikwenda nilipelekwa katika Wizara ya Mawasiliano na Ujenzi, tumekwenda kuangalia lakini wanakopesha nyumba hata mimi nimekopa nyumba. Mimi nimekopa nyumba Ilala Mchikichi nilikwenda na Mheshimiwa alikuwa na Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Makame Mshimba, tulikwenda mimi nilikwenda Mhe. Marina alikuwepo, Mhe. Hassan, Mhe. Subeit kamati ile ya zamani ikawa inajengwa nyumba ile Mkurugenzi akatwambia ilikuwa Suzan Omar kipindi kile akasema Zanzibar wanataka kukopa nyumba hiie nani atakopa na nyinyi kamati unatoa milioni kumi nyumba haikujengwa mimi nimetoa milioni kumi katika kamati yote, mimi ndio niliyenunua nyumba ile nikatoa milioni kumi nyumba hata bado ndio kwanza msingi lakini tumekopeshwa, tumepewa fursa ya kamati mimi nikachukua Kigamboni sijachukua.

Lakini pale Ilala nimechukua mpaka leo ninayo milioni mia moja na tisini na nane lakini tumemaliza juzi deni Mheshimiwa kidogo kidogo nilikuwa nalipa, mpaka juzi nimemaliza nyumba ile kupitia benki. Sasa hiyo fursa ingekuwa pesa hizi kuwa *cash* mimi nisingeweza kununua lakini kama mkopo mimi naamini wananchi wengi wangeweza kununua nyumba hiz, kupitia benki kwa kukopa nyumba hizi hata mimi nitakopa, hata wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pia watakopa nyumba hizi tutanunua. Sasa kusema kwamba hamna soko fedha hizi zipotee bure nyumba zimejengwa hasara bado hatujakaa na wataalam na elimu hatujakuwa nayo uzuri tukajifunze hapo Tanzania Bara kwa wenzetu *National Housing*, wanajenga vipi majumba yao kila siku wanajenga nyumba za mkopo nafuu na wananchi wananunua.

Lakini Mheshimiwa nije kwenye suala hili la uwanja wetu wa Kariakoo wa Uhuru hapa ripoti ya kamati ukurasa wa kumi na

tatu umetuandikia, Kiwanja cha Watoto cha Uhuru cha Zanzibar. Mheshimiwa kiwanja hichi ninavyojua mimi kimetumia karibu bilioni tano katika kujenga uwanja huu kuimarisha kwa kuwafurahisha watoto wetu, lakini leo unaambiwa katika ripoti kiwanja kinakuwa hasara hata ukitizama wafanyakazi wanatumiwa hao hao wa Wizara au wa ZSSF, kwa nini asitafutwe muwekezaji akakodishwa. Kwa sababu ukitizama sisi wenyewe tunafanya mambo mengi uchakachuwaji mwingi utafanyika hapa hichi kiwanja si cha kwenda hasara leo Leo unaambiwa Fumba kunajaa watu pale hawajai kwa nini tujiulize watoto wamekosa nini pale wasije? Kuna mambo mengi yaangaliwe biashara ushindani. Leo Fumba wikiendi kumejaa watu kule kuna nini kule watu wenye magari wachome mafuta wende kule wakakae mpaka usiku warudi mimi, kitu hicho siamini kama uwanja huo mzuri kama ule wa Kariakoo, mimi nimeshaenda mara mbili mpaka tatu naupenda, lakini kuna tatizo pengine hapa ya huduma au ya vipi.

Ukitizama hata hapa mambo ya tiketi sasa hivi dunia inakwenda kwa *electronic ticket,* unakwenda kununua tiketi unapewa kadi ndogo kama hivi, unatia pesa zako kama elfu hamsini unatumia kwa pembea zote hutoe *cash.* Hiyo dunia nzima inafanya hiviyo, lakini hapa utaambiwa kalipe *cash* pale dirishani unapewa risiti na tiketi zile pesa nasema wazi zitaliwa tu, lakini utafute kadi utaalam unanunua kadi unatia pesa zako kwenye kadi kama elfu kumi unatumia kwenye pembea zile ukimaliza kadi imeisha.

Tufanye utaalam huo hichi kiwanja si cha kwenda hasara au apewe muwekezaji, apewe mtu anayetaka kukodi akodishwe itolewe tenda ifanywe kazi hapa mara moja wageni wanakuja kutoka Tanzania bara kwenye kiwanja kile leo. Lakini pesa zinaingia zinaambiwa pesa. Mimi ninayo hapa takwimu tokea 2014/2015 tumekusanya bilioni karibu mia sita. Lakini gharama zake milioni mia moja na tisini na saba, tumepata mia sita milioni lakini gharama tu milioni karibu mia mbili, ukitizama 2015/2016

tumepata milioni mia nane, ukitizama gharama milioni mia tatu arubaini Mheshimiwa.

Ukenda mwaka 2016/2017 tumepata bilioni moja na lakini ukitizama gharama milioni mita tatu arubaini na nane, ukitizama hata Pemba mimi napongeza Uwanja wa Pemba wanakusanya kingi gharama yao inakuwa ndogo, wamekusanya milioni mia moja hamsini na saba Pemba lakini gharama yao milioni arubaini na tisa. Kwa hivyo hili ni jambo la kuangaliwa huu ni mfuko wa jamii unatakiwa kuingiza faida hapa sio hasara. Sasa kwa nini tuingize hasara huu mradi ni pesa nyingi na tumefanya historia ya nchi yetu kwa sababu ya kuwaenzi wazee wetu aliyejenga kiwanja kile Mzee wetu Abeid Amani Karume baba yetu kajenga kiwanja kile kwa nia njema.

Leo tumekiboresha lakini sisi kuendesha kile kiwanja Mhe. Mwenyekiti, kitakufa na hasara kwa sababu yatataka matengenezo mapembea yale baada ya muda itabidi aje *engineer* kuyatengeneza. Kama hatujakuwa na fedha za kutosha tutakifunga na kitakuwa kiwanja cha mambo mengine, kwa hivyo naomba sana tuangalie tufanye nini kiingize pesa kile kiwanja kisiwe hali kama hii kusema hamna hamna, tutafute kadi za *electronic* mtambo mdogo tuufunge ili mwananchi alipe pesa kwenye kadi yake ili aweze kutumia.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie haraka haraka kwenye ripoti ya kamati, nije hapa kwenye changamoto kwenye Hospitali yetu ya Abdalla Mzee ukiangalia changamoto kwenye ukurasa wa ishirini na saba kifungu cha tatu kinasema, kutokuwemo mazingira rafiki kwa wafanyakazi ikiwa pamoja na kukosekana kwa nyumba za daktari. Juzi nimesema hawa madaktari wetu wako hali mbaya wana shida daktari tumemsomesha miaka saba pengine nje kusoma kamaliza kaja hapa lakini unakuta leo hana hata nyumba au anakaa nyumba hairidhishi, au hana hata usafiri wa kuja

hospitali kazini. Nimesema kupitia Benki tuwakopeshe wafanyakazi wetu, *PBZ* wanakopesha dhamana iwe Serikali nafikiri huyu daktari ukimtafutia nyumba ya mkopo kama hizi za *ZSSF* ukimkopesha huyu miaka mitano, miaka mingapi atachukua atakopa. Akichukua utakua umeshamfunga hawezi kwenda Tanzania Bara kufanya kazi nyengine.

Sasa leo Daktari hana hata nyumba ya kukaa atamtibu mtu kweli, atamuokoa mtu maisha yake kweli, shida itakuwa kwa sababu akili yake haipo kuna familia yake nyumbani hajui iko vipi, watoto wake hajui wako vipi wanaishi vipi wanakaa wapi, hawezi kumtibu mtu akili yake haiko sawa inatakiwa akili yake iwe nzuri imetulia Mheshimiwa atafanya kazi kwa kumtibu mgonjwa kwa raha na furaha kabisa. Kwa sababu daktari anataka akupe moyo wewe mgonjwa uponde lakini daktari wenyewe kanuna utapona vipi wewe, huwezi kupona utaona huyu daktari na anataka kuniua sasa.

Kwa hivyo naomba sana tuwaangalie sana Mheshimiwa hali zao duni, mimi nimeshaona kuna siku daktari alikua anatakiwa aje hospitali ya kuzaa, lakini kumpa dawa ile nusu kaputi yule mgonjwa alale daktari yuko Bububu kule anaataka aje pale, mimi nipo pale kwa kweli usafiri hana daktari apande dala dala aje huku. Huku anataka kum-save mgonjwa mwanamama mjamzito leo apande daladala mimi nikatoa *ambulance* hebu mchukue mara moja mlete hospitali.

Sasa lazima tuangalie hawa madaktari ni muhimu ku-*save* maisha yetu leo daktari hana hata usafiri hana hata vespa, hana hata gari apande daladala, saa nne za usiku gari hiyo ataipata wapi. Kwa hivyo mimi naomba tuangalie Mhe. Waziri, tuangalie madaktari wetu hawa ni watu muhimu sana katika maisha yetu.

Mhe. Mwenyekiti hapa mwisho nimalizie katika mgawanyo huu wa fedha, Muungano na msaada wa bajeti, kwanza mimi niipongeze sana Serikali yetu ya Muungano kwa kazi yake kubwa sana inayofanya na Muungano wetu huu kudumisha wa kidugu na kidamu kwa pamoja, naamini siku hadi siku Muungano huu utakuwa na manufaa zaidi zaidi kwa Zanzibar kama ulivyokusudiwa hapo mwanzo. Kwa hivyo changamoto nyingi sana tunaanza kuzibadilisha. Nipongeze sana mambo mengi hasa ule wa 4.5% kupata, niipongeze sana Muungano kwa kazi hiyo kubwa sana wanayoifanya kwa Zanzibar.
Lakini pia niseme ukurasa huu wa ishirini na moja kifungu namba tatu, hapa inaeleza kuwa kuna changamoto hii bado Mheshimiwa inasikitisha kidogo, hii changamoto ambayo kwa wafanyabiashara wa Zanzibar wamekuwa wakilipa kodi mara mbili kwa upande wa Tanzania bara, hii inasikitisha lazima changamoto hii tuifanye kila njia imalizike. Kwa sababu ukiangalia sasa hivi katika ripoti hii ya Kamati nafikiri niliiweka pahali hapa ukiangalia sasa hivi thamani ya vitu au bei ya vitu, mfumko wa bei unaongezeka kwa Zanzibar, asilimia nane au tisa imeshaongezeka tayari na jana nilisema.

Kama hali itakwenda hivi itakuwa Zanzibar hata wafanyabiashara watashindwa kujimudu. Sasa mimi naomba changamoto hii tuiangalie kwa undani kwa sababu Zanzibar ni kisiwa hapa tuna biashara ukiangalia karafuu, ukiangalia utalii, ukiangalia na hawa wafanyabiashara, ni ajira kubwa imekamata hawa wafanyabiashara wetu wadogo wadogo ambao wanauza bidhaa ndani na kupeka Tanzania Bara.

Kwa hivyo hapa tuangalie hizi kodi kama mara mbili mbili mtu alipe hapa kodi ya *VAT,* ende kule alipe kodi ya *VAT* aje huku alipe tena kodi ya *VAT*, huu mzigo utakuwa haumlipi thamani yake itakuwa kubwa. Anahitaji mfanyabiashara yoyote kwanza kupata faida hakuna mfanyabiashara anayetaka kupata hasara. Kwanza jambo analoangaliwa ni faida akishapata faida atalipa

kodi, akipata faida atalipa *ZRB* atalipa kodi ya pango yake ya duka, atalipa umeme, atalipa mfanyakazi, atalipa ajira. Sasa kama hapati faida atamlipa nani kama ana wafanyakazi wanne atabakisha wawili, kama atakuwa na wawili atabakisha mmoja Mheshimiwa sisi tunahitaji ajira, ajira ni kitu shida. Kwa hivyo hii sekta hii imebeba watu wengi kwa ajili ya ajira kwa ajili ya watu wa nchi ya Zanzibar na pia inakusanya kodi karibu asilimia thalathini kodi ya taifa la taifa kutokea kwa wafanyabiashara hawa.

Sasa mimi naomba hii kodi vya *VAT* na mimi kama Mbunge kupitia Baraza la Wawakilishi ninakwenda kwenye Bunge la Jamhuri, naomba sana Mheshimiwa hizi changamoto basi tupewe tuandikiwe tukazitetee kule ndani ya Bunge la Jamhuri au kuna sehemu husika tutakwenda mimi Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, lakini naogopa leo kwenda Bungeni kusema maneno yaliyokuwa hayana maana tukaja tukauchafua Muungano huu, naomba sana tupewe kazi mtupe kazi mliyotupa….

Mhe. Mwenyekiti: Malizia Mheshimiwa.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante Mheshimiwa namalizia kwa hivyo naomba tupewe changamoto kama hizi tukazihusishe kule tukaziwakilishe upande wa Zanzibar kuna moja mbili tatu, kwa utaratibu mzuri. Mimi niipongeze sana ripoti ya Kamati hii niipongeze Serikali yangu kwa bajeti hii, na naomba sana hizi changamoto zilizokuja mara hii mwakani Mheshimiwa naomba zisiwepo. Mhe. Waziri upo makini, Mhe. Makamu wa pili najua uko makini kabisa tuondoshe changamoto hizi mwakani ije ripoti nzuri changamoto haina, itakuwa tumepiga hatua kwa asilimia karibu thamanini kwenye nchi yetu ya Zanzibar.

Mheshimiwa nakushukuru sana na mimi naunga mkono asilimia mia kwa mia kwa ripoti hii ya kamati. Ahsante sana. (Makofi)

Mhe. Mweyekiti: Ahsante nashukuru Mhe. Hussein Ibrahim Makungu sasa naomba nimuite Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia ripoti hii ya Kamati ya bajeti ya mwaka 2017/2018 kwanza naomba nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati brother wangu Mhe. Mohammed Said Mohammed amefanya kazi kubwa sana kwa kushirikiana na wajumbe wa kamati, nimekipitia kitabu hichi nimeyaona mengi lakini ushauri wangu naupeleka moja kwa moja kwa Mhe. Mwenyekiti.

Nilipokuwa nikiangalia changamoto hizi ambazo baadhi ya nyengine ameziainisha zilikuwa zinawahusu moja kwa moja Wanyeviti wa kisekta nipendekeze tu pale ambapo hajamaliza mzunguko wa kamati, kwa sababu kuna nyengine zinahitaji kufuatiliwa basi sisi wenyeviti wengine aweze kukaa nasi, pamoja na kuwa tunapita lakini yapo mengine ambayo anaweza akayakuta baada ya kuwa zile kamati zimepita katika eneo lile. Kwa hivyo kwanza nimpongeze sana kwa sababu aliyoyaibua ameyaibua katika mfumo wa bajeti na utekelezaji lakini pia ameziibua nyengine ambazo pia zinafanyiwa kazi na kamati nyengine.

Kwa hivyo nimuombe sana mimi mara nyingi alikuwa akininong'oneza baadhi ya mambo lakini naamini na wenzangu anawanong'oneza lakini ni vyema basi hata siku moja akaandaa utaratibu mzima wa kuwaona wenyeviti kwa yale ambayo yanahisi kufuatiliwa katika mfumo wa kamati za kisekta basi wakaweza kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo za Mhe. Mwenyekiti, kwa kazi nzuri naomba niende ukurasa wa kumi kunako eneo la

tathmini juu ya taarifa ya utekelezaji wa robo ya pili Oktoba hadi Disemba, nikisoma katika mpango wa maendeleo taarifa ambazo ameziandika Mhe. Mwenyekiti na nikisoma mapato na matumizi wenzetu wa Serikali hususan Wizara ya Fedha inayosimamia mapato ya Serikali, pia na mgawanyo ule wa matumizi ya Serikali umefanya kazi kubwa sana. Kwa maana hiyo naomba nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mhe. Waziri wa fedha pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote ambao wanashirikiana nao.

Asilimia iliyoandikwa hapa ni asilimia tisini na tatu ni hatua kubwa sana katika utekelezaji wa ukusanyaji wa mapato haya, lakini pia ukiangalia kunako matumizi unakuta asilimia thamanini nukta tisa unahisi hasa ule mgawanyo ulivyokwenda katika utekelezaji wa bajeti kwa Wizara na Taasisi za Serikali katika shughuli za kawaida na zile za maendeleo ni hatua njema sana, naomba tena nimpongeze Waziri huyu na Katibu Mkuu na Mwenyezi mungu awajaalie kuwa na kasi nzuri kama hii ya utekelezaji ili kuisaidia Serikali yetu kusogea mbele zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika changamoto za mamlaka ya uwekezaji na vitega uchumi changamoto namba nne. Kwanza niishukuru kamati kwa kuliona hili kwa kuwepo kwa madalali ambao mara nyingi wanawatumia wale wawekezaji wanaokuja kutaka kuwekeza hapa nchini. Changamoto hii mimi nikubaliane nayo Mhe. Mwenyekiti, ipo na wakati mwengine ni sahemu ya kusababisha ile migogoro isiyokuwa ya lazima. Sasa nakubaliana na mapendekezo ambayo umeyatoa lakini na mimi niendelee kushauri mara tu wanapotokea wawekezaji hao wenye nia nzuri pamoja na kuwa lazima wapokewe na Wazanzibari au Watanzania walioko hapa, lakini mara wanapokwenda katika utaratibu nzima wa kwenda kupeleka maombi katika sekta zetu au katika Wizara zetu basi Wizara zile ziweke utaratibu mzuri wa kuzungumza na hawa wawekezaji moja kwa moja, isiwe utaratibu huu wa

kuwatumia hawa madalali ambao wakati mwengine unaweza ukazorotesha utaratibu mzima wa uwekezaji hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, naomba tena niende katika eneo la *Penny Royal* kuna changamoto imewekwa ambayo wanaonyesha mahitaji yao ya hekta 220, lakini kuna taarifa ambazo ziko rasmi na mimi pia ni mjumbe wa bodi ya kamisheni ya ardhi naomba ku-*declare* interest. Sasa katika utaratibu wa kawaida wawekezaji hawa wameshapewa hekta 411 hadi sasa, ukenda katika utaratibu wa wastani wa ekari zile za kawaida ni karibu 1100. Ni hatua kubwa sana ambayo wawekezaji hawa wamepewa na serikali kwa nia njema. Tukiendelea kuwapa maeneo bila ya ule uwekezaji kuonekana hatuwezi sisi kusogea lakini nakuamini ule utekelezaji.

Tukirudi katika muwekezaji ambae tumempa Fumba Bakharesa tumempa hekta 100 tu lakini utekelezaji tumeuona katika ile ile mia tuliyowapa. Lakini leo aliyepewa 411 maana yake yeye kakushanya tu ukisha unaomba tena 220 aendelee kukushanya tu, lakini ile azma na ule utekelezaji hauwonekani. Mimi hapa sihesabu changamoto nasema tu hii ni sehemu ambayo taarifa imetoka, lakini katika sura ya changamoto kama muwekezaji mzuri lazima atumie kwanza angalau kuonekane.

Kwa hivyo mimi niishauri serikali kwenye azimio hili au changamoto hii basi naishauri kile alichopewa 411 aanze nacho tuone ile hatua ya utekelezaji, maana yapo maeneo mengi wawekezaji tumewapa na wengine wameshindwa wameyajengea makuta hakuna utekelezaji namna ya kuyafuta sasa hivi serikali inatafuta huo mpango wa kuonekana vipi watafanya ili hatua hiyo iendelee. Kuendelea kumkusanyia muwekezaji mmoja ardhi yote bila ya kuonekana hatua ya utekelezaji na mfano nimetoa, Bakharesa tumempa 100 lakini utekelezaji kwenda hekta 100 zimeonekana, huyu uliyempa 411 haujaonekana, ikisha tunaandika changamoto anataka 220, Serikali ikiendelea kufanya

hivi kuna wengine wanaweza kuwa wasiwafahamu mmoja mimi. Sasa niishauri tu kama ana azma nzuri ya uwekezaji basi aonekane kunako zile 411 baadae zile nyengine zitafuata hata kama ukitaka 400, au 600 unapewa tu, kwa nini mwanzo upewe 411 mwanzo ushindwe kupewa 220. Sasa kwenye changamoto hii mimi niko tofauti kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ziara ya Kamati Mamlaka ya Kuendeleza Maeneo ya Uzalishaji Mauzo ya Nje. Kamati imeona na mimi niliwahi kulipendekeza hili kuwa Kamati pia ilijifunza namna ya kituo cha *Stop Center*. Kwanza niipongeze serikai Kamati ilikwisha pita katika kituo hichi, huu ni utekelezaji nzuri na tunaomba zile changamoto ambazo Mwenyekiti wa Kamati ameziona na ameziainisha serikali ichukue jitihada za makusudi ili kuweza kutatua eneo hili ili mambo yaende vizuri.

Pia niipongeze Kamati ilipokwenda katika Mamlaka ya Mapato kwenye utaratubu ule wa kushauri mashine zile EFD ni kweli tumeipongeza serikali, tumeipongeza Wizara ya Fedha imefanya kazi kubwa, mapato yameonekana, lakini tukienda katika utaratibu mzima wa kuanzisha mashine hizi za EFD basi mapato yetu yatakuwa kwa kiasi kikubwa sana. Sasa na mimi niungana na Kamati jambo hilo wameliona zuri, basi kama walivyoshauri serikali iharakishe kuingia katika mfumo huu ili ile mianya midogo midogo ambayo tunaweza baadaye kuizuia kupitia mashine hizi za EFD itakapoanza, naipongeza sana Kamati kwa kuliona hili.

Niende kwa ujumla Wizara ya Kilimo na Mifugo wameizungumzia Sekta ya Uvuvi lakini mimi nachanganya na kilimo pia. Katika sekta hizi mbili katika kukuza uchumi wetu tukizitumia vizuri tunaweza tukafika kwa haraka zaidi. Sekta ya Uvuvi ina uchumi mkubwa sana, tukiitumia vizuri basi tunaweza tukafika kwa uharaka. Lakini Sekta ya Kilimo pia nayo niiombe

serikali basi tuwekeze pia katika Sekta ya Kilimo. Mara zote tukiagiza chakula basi fedha yetu tunayoitumia kwa kuagiza chakula chenyewe, tukichenji pesa tukenda kununua chakula na kurejea hapa basi sehemu kubwa ya uchumi pale kati kati unaweza ukaona uharaka unavyouangusha. Lakini tukiwekeza kwenye kilimo tukilima vizuri katika kilimo cha *irrigation* tukizalisha chakula chetu nchini, tukiuza ndani na wananchi wetu wakapata mahitaji yao hawatakuwa na mpango ule wa kuagiza chakula, basi fedha yetu itakuwa na itaimarika katika utaratibu mzima wa kukuza hili pato la nchi na la mtu mmoja mmoja pia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwenye kitabu hichi sina mchango mkubwa wenzetu Kamati wamefanya kazi kubwa lakini naendelea kushauri eneo zima la Mwenyekiti kwa yale ambayo utakayoyaona basi wenye viti wenzio tuainishie changamoto zile iwe ni sehemu ya *assignment* zetu ambazo tunaweza kwenda kuzifanyia kazi pamoja na kuziripotia serikalini, hii ni wajibu wako kama Mwenyekiti lakini na sisi kwenye maeneo mengine hasa wale wanaomiliki sekta waweze kuzitumia kwa utaratibu mzuri.

Mwenyekiti, naomba kukushukuru na niwapongeze Wanakamati wote kwa kazi nzuri waliyoifanya na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na kumi (110%).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Miraji Khamis Mussa, sasa naomba nimwite Mhe. Suleiman Sarahan Said.

Mhe. Suleimna Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia machache katika kitabu chetu cha Bajeti. Awali ya yote kwa bajeti hii tunayokwenda nayo napenda kumpongeza sana Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti, wa Baraza la Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika jitihada zake za

kuliongezea Zanzibar pato pamoja na kuwaimarisha wananchi wake katika sekta mbali mbali na kuweza kuionesha Zanzibar ikipata mafanikio katika hali ya juu kwa kipindi kifupi sana cha uongozi wake.

Mhe. Mwenyekiti, si jambo dogo sana ambalo Rais wetu alilolifanya kupandisha mishahara kwa asiimia mia moja ni jambo kubwa sana na ni jambo la kupigiwa mfano kwa nchi nyengine, lakini pia kinataka ujasiri kutokana na hatua ambayo amefanya mbinu gani mpaka akaweza kufanikisha na suala hili linakwenda kama alivyolitarajia wala halina kupinda pinda.
Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ni nchi mojawapo iliyokuwa inafanya mambo yake katika uhalisia wa kibinaadamu. Kwa sababu huduma nyingi zinazofanyika katika nchi hii ambazo ni za lazima kama afya, elimu ni vitu muhimu sana kwa binaadamu na Zanzibar asilimia kubwa ikiwa ni bure kwa huduma hii. Lazima nimpongeze Rais kwa jitihada zake anazozifanya kwa kuwapatia wananchi wake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nizungumzie habari chache chache zilizokuwemo katika bajeti humu, kuna kitu kama uchumi. Uchumi ndio kila kitu ndio unaotufikisha hapa na ndio unaoendesha wananchi kwa kupitia serikali, kwa hivyo ni kitu muhimu sana tukaupima uchumi wetu, tukauangalia zaidi uchumi wetu tunaupima kwa kuangalia unatoka wapi. Kuna nchi ambazo uchumi wake unatoka katika maumbile ya ardhi ambao wengine wanapata mafuta, wengine wanapata gas, wengine wanapata vitu gani. Wengine uchumi wa nchi yao unategemea kwa kuutengeneza nchi yao katika viwanda na vitu mbali mbali ambavyo vinasaidia uchumi. Sisi tumeshakaa katika kipindi kirefu ambacho uchumi wetu tunategemea sana mazao kama zao la karafuu, labda sasa hivi tunaingia kwenye utalii na mambo mengine ambayo yanatusaidia kupata pato letu kupitia mitaala hiyo.

Ningeiomba sana serikali, ikachukua juhuzi za makusudi katika kuangalia mambo ya miradi mingi ambayo tunakusudia kuifanya na inaweza ikaleta mapato kwa njia mbili. Kwanza tunapata ajira kwa wananchi wetu, lakini pia tunapata mapato kwa kuisaidia serikali na pesa zile zikafaa wananchi wetu. Ningeomba muda haupo tena kila kitu kinahitajika kwa muda, serikali ifanye jitihada za kuhakikisha katika nchi yetu katika upande wa ardhi ni madini gani ambao yanaweza yakatusaidia kwa muda wa haraka ili kuweza kutusaidia kipato chetu ukiachia mapato ya biashara, ambayo tunayakisia ndiyo ya msimu na utalii una msimu unataka usalama wa nchi na kuna mambo mengi ambayo yanaboreshwa mpaka kupatikana kwa uchumi huu. Ningeomba sana serikali kwa kupitia wataalamu wake tukaangalia tena na njia nyengine za kupata mapato yetu kwa kupitia uchumi na masuala mengine.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala la biashara. Biashara nayo inasaidia wananchi, inapata mapato serikali, lakini bado hatujajiingiza sana katika viwanda bado tumejiingiza katika biashara ndogo ndogo ambazo tija yake ni ndogo pia. Serikali ina matumizi makubwa sana, kwa sababu inataka haja ya kukidhi matakwa ya wananchi lakini bila ya mapato serikali haiwezi kufanya kitu kwa sababu itakuwa haiwezi kukidhi haja ya mambo yale. Mimi ningeomba sana tuongezeni njia za kutafuta mapato ili serikali yetu iweze kusaidia wananchi na kuweza kujiendesha kwa sawiya kuliko mambo mengine.

Nije kwenye Sera za kodi, katika Sera za Kodi bado nchi yetu inafanya sera zake za kodi lakini kodi bado vyanzo ni vile vile. Ningeomba tukaangalia utaratibu wa kwamba tunaweza tukashusha kodi lakini vianzo vikawa vingi ili wananchi wetu wakapata urahisi katika kupata mapato na kujiendeleza katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala la Utalii, bado Zanzibar tunasema tuna utalii lakini bado utalii hatujaufanyia kazi, bado tunakwenda katika mwendo ule mdogo mdogo. Zipo haja za makusudi za kuendeleza utalii wetu ili tukahakikisha sasa utalii unatia tija, sasa utalii unaleta utalii ili tukapata fedha kwa sababu tumeshaweka na kuegemea katika Sekta yetu kwamba Utalii ni moja ya pato letu la kutuingizia fedha. Ningeomba sana utalii na watu ambao wanahusika na utalii wakaweza kupunguza baadhi ya mambo wanayoyaona yanaweza kuwa hayaleti tija, lakini pia kuutangaza utalii kwa Zanzibar tukatumia fedha kwa kuitangaza Zanzibar kiutalii na tukayafufua maeneo ya utalii ili tukapata fedha zaidi.
Mhe. Mwenyekiti, masuala mengine kama nilivyozungumza nilizungumzia kwamba utalii kwa asilimia naweza kusema 80 inayokwenda sasa hivi bado utalii ni wa Unguja tu ndio unaofanyika. Utalii wa Pemba haujafanyika kabisa. Ningeomba sana na jambo ambalo nalisemea utalii kwa Pemba bado usafiri wa Pemba haujakuwa kamili, bado usafiri una matata, bado usafiri una shida. Sisi wenyewe raia wa ndani tu tunajua kwamba usafiri wa Pemba na Unguja ni wa shida hatusemi mtalii ambaye na yeye atalihangaikia hilo, unaweza ukafika Pemba ukakwama *one week* unataka safari ya kuja Unguja haipatikani, ndege zimejaa, masuala hayaendi.

Kwa ulimwengu wa sasa siku moja ni kubwa, maisha yenyewe ni machache mtu akifika miaka 30 tayari sukari, unga, keshachanganya kila kitu, akipata uhai wake ni miaka michache. Sasa tunataka mtu angalau ajione katika kipindi chake ya uhai amefanyaje. Ni lazima maisha ya usafiri yawe na *speed* kweli kweli. Ningeshauri sana sekta za usafiri zikafanyiwa utafiti wa kutosha ili kule Pemba nako kukaonesha utalii wake na ikaweza kuongezea mapato. Mhe. Rais wetu wa Zanzibar anazungumzia kwamba utalii Pemba haujafunuliwa na bado zipo nafasi nyingi tu za kuweza lakini tatizo kubwa ni usafiri, tulikuwa tunasema mahoteli yanajengwa lakini bado usafiri.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye sehemu ya Uwekezaji. Sehemu za uwekezaji zipo nyingi sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba umalizie.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante Mheshimiwa basi namalizia naunga mkono hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana, Mhe. Suleiman Sarahan Said najua ulikuwa umebakisha dakika zako kama tano, lakini kutokana na muda kama utaweza jioni kumalizia dakika zao naweza nikakupa nafasi. Lakini pia na Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil ajiandae kwa jioni.

Waheshimiwa Wajumbe naomba niahirishe mpaka saa 11:00 jioni.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Hapa Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alikalia kiti

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa tunaendelea tulibakisha mjumbe ambaye alikuwa na muda wake Mhe. Suleiman Sarahan Said, kwa hivyo nakupa dakika tano umalizie katika mchango wako wa leo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa tena ya kumalizia muda wangu. Labda niendelee tu Mheshimiwa mimi katika mchango ambao

naendelea kuchangia ni kwamba kuna mambo ambayo miradi, majengo ambayo serikali huyaanza kwa kasi yakimaanisha kwa kuwa ni *target* fulani, lakini majengo yale yanaweza kuchukua tena zaidi ya miaka kumi bila kufikiwa malengo yaliyokusudiwa na fedha ile ambayo ilishakwenda pale basi thamani yake huwa imeshaanguka kwa kipindi na faida huwa haipatikani.

Kwa hivyo, ningeiomba serikali sana katika jumla ya mambo ambayo wanatizama mapema ni kwamba jengo au miradi itakayoanzishwa basi ihakikishe inamalizika ili kutimiza haja na tija ambayo serikali ingeweza kufaidika na kuongeza mapato.
Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana serikali iondokane sana na tatizo la kukodi maofisi kwa sababu ni pesa nyingi sana za walipa kodi zinapotea katika kukodi majengo ya maofisi. Ingawa serikali imejitahidi sana hivi sasa lakini bado kasi yake isipungue na iweze kumaliza kabisa tatizo la maofisi ili fedha zinazopatikana ziweze kusaidia wananchi.

Lakini Mheshimiwa niende kwenye fedha za misaada. Mhe. Mwenyekiti, huwa tuna mpango wa kupata misaada lakini ufuatiliaji au umalizikiaji wa ule msaada unakuwa haufikii malengo, sisi tuna barabara ya Wete - Chake Chake imeshatimia miaka kumi inakwenda kila siku haijajulikana barabara ile itamalizia vipi. Kwa hivyo, ningeomba sana misaada ifuatiliwe na mambo ambayo yamekusudiwa yamalizike ili tuweze kutafuta jambo jengine ambalo linaendelea.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kuna suala moja ambalo linaipunguza nguvu sana serikali katika malipo yake. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi ni lazima tufike pahala ardhi yetu tuweze kuipima na kuigawa vizuri sana ili kujua malengo ambayo tunataka kuifanyia na maeneo ambayo yanaonekana yatakuwa vitega uchumi ya barabara na kila kitu.

Mhe. Mwenyekiti, serikali inapoteza pesa nyingi sana katika kulipa watu gharama za kwenye barabara, hili limekuwa ni tatizo kubwa. Ningeiomba sana serikali kupunguza mzigo huu ni kutafuta fedha na kuipima ardhi yetu tuliyonayo ili tukaweza kuweka alama pamoja na maeneo ambayo yanahitajika kuja kuweka vitega uchumi au kuweka maeneo maalum yaliyokuwepo. Lakini pia itakuwa na mpango maalum wa kuweza kuweka miundombinu yake katika maeneo yale ili lile suala liweze kumalizika kwa haraka kama patakuwa pana mwekezaji kama ni kiwanda, basi suala la umeme na maji iwe tayari miundombinu imekwenda katika maeneo yale.
Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nizungumzie suala la Kisiwa cha Pemba kidogo. Mhe. Mwenyekiti, kwa mpango maalum unahitajika serikali itizame Pemba kwa jicho la huruma sana kuhusu suala la mfumko wa bei katika vitu vyake. Pamoja na kwamba Mheshimiwa mpaka sasa hivi Pemba ikifika saa 12:00 basi huoni gari hata moja kutembea tena unaweza ukalala barabarani, bado inahitajika Pemba kufufuliwa na kuweza kuangalia inakwenda wapi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kitu kilichopo Pemba ukenda Dar es Salaam au Zanzibar unakinunua mara mbili, huu ni mfumko wa bei ambao unawakandamiza sana wale watu wake kule kwa misingi wanakwambia kwamba labda usafirishaji pamoja na kodi nyengine ambazo wanasema zinakuwa sio za lazima. Kwa hivyo, ningeomba changamoto nyingi kwa sababu umoja wa Zanzibar ni Kisiwa cha Unguja na Pemba, bado Kisiwa cha Pemba kinahitaji kuboreshwa kuweza kutoa mapato ili kusaidia katika miradi yetu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie suala la...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika moja.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante Mheshimiwa, nizungumzie kipato cha mtu. Mhe. Mwenyekiti, tunazungumza sana suala la kipato cha mtu kimeongezeka lakini kwa mtazamo wa karibu hakionekani. Utakuta sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, hata ukiuliza utaambiwa bwana Pemba kwa nini wafanyabiashara hawaji juu. Ni sababu iliyopo Mheshimiwa anakuwa katika ukoo mzima anayejiweza ni mmoja waliobakia wote ni maskini. Sasa inakuwa yule mmoja akifungua kiduka waliobakia wote wanamuandama yule mpaka wanamuangusha.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa namwita Mhe. Ahmada Yahya akifuatiwa na Mhe. Hamza Hassan Juma ajitayarishe.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona na napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu alaasiri ya leo kuwa mchangiaji wa pili katika hotuba au katika ripoti ambayo inahusiana na bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba kwa hakika tumeipokea na mimi nimepokea kikamilifu na nilikuwa nikipitia dondoo hadi dondoo. Mimi katika mchango wangu utakuja katika ukurasa wa 16 na 17 kwenye changamoto za Maeneo Huru ya Uwekezaji Amani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hakika hapa ni pahala penye tija sana kwa uchumi wa nchi yetu na serikali haikukosea kuanzisha *zone* ile ya Viwanda Vidogo Vidogo katika miaka ya thamanini. Katika miji yote duniani ardhi ni kitu muhimu sana na ni mali ya mwanzo kabisa katika uwekezaji. Kwa hiyo, suala la kuwa na ardhi kama ile na kamati ikiwa imeona kama kuna majengo ambayo yamechakaa na yanavuja, hili suala serikali ingilie kati. Ni kweli kuna majengo ya maana mle ndani na ni majengo ambayo

yamejengwa kwa umadhubuti mkubwa na miaka mingi. Ikiwa mwekezaji akija kutaka nafasi ya kutaka kuwekeza na majengo yenyewe hali ile ni jambo la kuvunja moyo.

Kwa hiyo, mimi ushauri wangu kuna changamoto au maoni ya kamati iliyosema kwamba kunahitajika milioni thamanini kujenga ule uzio, hili jambo ni jepesi kwa serikali. Mle ndani tunavyosikia kuna mwekezaji wa *ZANTEL* ambaye kwa miaka saba sasa yeye anakuwa ndio *champion* kwa kulipa kodi. Ikiwa uzio ule umeshindikana kujengwa na ikapatikana usalama wa eneo husika jambo hilo haliingii kwenye mizani. Kwa hiyo, Wizara ya Fedha na Mipango kuhusiana na hawa *ZIPA* washirikiane zipatikane hizi milioni thamanini na ule uzio ujengwe wa kisasa.

Tumezowea kujenga uzio kwa matofali lakini kadri siku zinavyoendelea mimi nasema hizi milioni thamanini ni kidogo, tuige mfano wa uzio wa Uwanja wa Ndege ambao ule *guarantee* yake si chini ya miaka hamsini kwa sababu ni ujenzi wa kitaalam wa uzio na wala hauhitaji gharama kubwa lakini unaweza ukadumu hata miaka sabini na kuendelea. Kwa hiyo, hii ni changamoto lakini imo ndani ya uwezo wetu tunaweza tukajenga ukuta ule tukahifadhi na majengo yale tukaanza kuyafanyia *repair* kidogo kidogo, yale majengo ni ya thamani na ardhi ile kwa leo kwa mji huu huwezi kupata ardhi nzuri pahala pazuri katika uwekezaji kama pale.

Kwa hiyo, nia ya serikali ilikuwa ni *Small Scale Industries*, ile nia ya mwanzo wakati wa uanzishwaji naikumbuka ilikuwa ni *Small Scale Industries* yaani Uwekezaji wa Viwanda Vidogo Vidogo. Kwa hiyo, ipo haja serikali kuliangalia suala hili na uzio ule ukashughulikiwa na *inshaallah* ikawa tatizo hili limeelekea hatua nzuri.

Kuhusu *ZIPA.* Mhe. Mwenyekiti, hapa ni pahala muhimu sana ni kitovu baina ya ukuaji wa uchumi na wawekezaji wanaokuja. Mimi ushauri wangu nasema wakati umefika kwamba *ZIPA* isizingatie wawekezaji wa nje tu, lakini kuna wawekezaji wa ndani ambao wana uwezo wa kuwekeza ila tu wanakosa mbinu za kufahamishwa na kuelekezwa na kushajihishwa wakaweza kushiriki katika uchumi wa nchi yao. Mimi naamini kama inavyotaka kuzungumzwa iwe *One Stop Centre* basi kitengo hiki kiimarishwe, na hata kwenye *Zanzibar Business Council (ZBC)* imeshawahi kuzungumzwa kwamba iwe ni ya *One Stop Centre* ya kweli.

Kwa nini nikasema. Leo ikiwa anakuja mwekezaji anaanza kuja uhamiaji aende kwake, akija kwenye miundombinu aende kwake, akija kwenye hiyo *staff* yenyewe *ZIPA* aende kwake, ikiwa *One Stope Centre* basi taasisi zote zenye kuhusika na uwekezaji wawe na ofisi moja, hiyo ndio nitaamini kama ni *One Stop Centre.* Wenzetu wa Rwanda kweli wapo *One Stop Centre* ndani ya siku thalathini mwekezaji ameshapewa *lease* na anaanza kazi serikali inachukua mapato yake.

Kwa hiyo, kitengo hiki cha *One Stop Centre* cha *ZIPA* kiimarishwe na kiwe kweli *One Stop Centre* si kama ilivyo. Leo nimeshawahi kushuhudia anakuja uhamiaji anachukua mwezi mmoja, anakuja kwenye taasisi nyengine anachukua mwezi mmoja, unafika mradi mpaka anaamua kutaka kuondoka bado *lease* hajapata. Kwa hiyo, ipo haja *One Stop Centre* hii imarishwe. Lakini mkazo zaidi umefika wakati nchi yetu iwape fursa na iwashajihishe wawekezaji wazalendo wapate kuwekeza. Mimi naamini mabenki yamejiandaa kuwasaidia wawekezaji wazalendo, kuna benki ya *NMB,* kuna benki *PBZ* na benki mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, mabenki haya yaliyokuja yanachukua juhudi binafsi kuwafuata wateja kusudi wawape mikopo na fursa mbali mbali. Sasa mfumo huu huu wa benki kuwafuata wateja mimi naamini na *ZIPA* wanao uwezo wa kuwafuata wawekezaji wa ndani wakawapa mipango wakaweza kushiriki katika uchumi wa nchi yao. Hao wawekezaji wa ndani kwa hakika wana nia sana nzuri ya kuwekeza lakini wanakosa mbinu za kufahamishwa. Kwa hiyo, wakati umefika naishauri serikali kupitia *ZIPA* wawashajihishe wawekezaji wa ndani ili waweze kutumia fursa hizo.

La mwisho kuhusu uwekezaji wa maeneo huru ya Fumba. Mimi naamini kwamba serikali kwa nia safi kabisa ina nia ya kuendeleza mji wa Fumba ili uwe mji wa kisasa. Lakini ukiangalia hasa mpaka sasa hivi hakuna mpango mahsusi na unaojulikana kwamba sasa mtu akitaka kwenda kuwekeza aanzie wapi, apite wapi, apate ruhusa wapi, kwa mujibu wa mradi ambao anataka kuwekeza. Mimi nasema tena na nashauri serikali wawekezaji wapo wa ndani na wanaweza kushiriki kuwekeza katika uchumi wa nchi yao lakini wafahamishwe na iwe *easy* ukianzia hapa, unakuja hapa, unapeleka *proposal* yako, *capital* yako *investment* iko vipi na unaweza ukaingia ubia nao.

Suala la uwekezaji. Mhe. Mwenyekiti, kuna nchi za Falme za Kiarabu wao wana mpango wa kuwawezesha wazawa au wazalendo, kampuni inapokuja wanakuwa na *list* ya wazalendo ambao wanaweza wakashirikiana na wale wawekezaji kwa mujibu wa uwekezaji wenyewe husika. Sasa mimi naamini wakati umefika *ZIPA* na wao kuwatambua, kuwaita na kuzungumza nao fursa zile za uwekezaji wanapokuja wageni na wazalendo wanaweza wakafanya *join ventures*, kwani nia ya *ZIPA* ni *promotion* yenye kukuza uchumi kwa kila siku. Kwa hiyo, mzalendo anayo haki ya kutumia fursa zile akishirikiana na wageni kusudi uchumi uende mbele na serikali ipate mapato yake.

Mhe. Mwenyekiti, nasema Wazanzibari wanaweza kushiriki uchumi wakishirikiana na wageni watakaokuja kusudi uchumi uende mbele.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa jumla naikubali kwa asilimia mia juu ya mia ripoti hii ni nzuri na ifuate misingi hiyo, ili tuondokane na kuwa wageni wanaweza lakini na wenyeji pia wanaweza. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil. Sasa anafuata Mhe. Hamza Hassan Juma Mwakilishi wa Jimbo la Shaurimoyo, akifuatiwa na Dkt. Makame Ali Ussi na Mhe. Rashid Makame Shamsi ajitayarishe.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nakushukuru pia na wewe kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi iliyosomwa na Mhe. Mohammed Said Mohammed, mheshimiwa makini sana katika jengo letu hili la Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, naungana na wenzangu kuipongeza kamati hii iliyojaa wajumbe makini sana, wasomi waliobobea, kwa hiyo wametuletea vitu ambavyo kwa kweli kama tutavifanyia kazi basi kwa kiasi fulani tutaweza kuisaidia sana serikali yetu kuweza kuboresha uchumi wake, kuongeza ajira, lakini vile vile kuipatia mapato makubwa serikali yetu. Kwa hiyo, naomba sana kwa sababu Kamati ya Bajeti haina tofati sana na Kamati ya *PAC* ni kamati ambayo haina mipaka katika utendaji wake, inagusa wizara zote baada ya kuleta taarifa na wao wanakwenda kuzifuatia utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze moja kwa moja katika ukurasa huu wa 12 ambapo Mwenyekiti ametuelezea changamoto za Benki Kuu Tawi la Zanzibar. Ameeleza hapa kwamba baadhi

ya wananchi kukosa uelewa mzuri kuhusu kazi za majukumu ya Benki Kuu Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nilisema nilipokuwa nachangia Ripoti ya Kamati ya Fedha na Uchumi na leo narejea tena kusema kupitia Ripoti hii ya Kamati ya Bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, *BoT* sio wananchi tu wa Zanzibar wengi hawajui majukumu yao, lakini naamini karibu zaidi ya asilimia sabini ya Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi basi pia hawajui majukumu hasa ya *BoT* kwa wananchi wa Zanzibar.

Kwa hiyo, narejea tena wito wangu kupitia Wenyeviti wa Kamati hizi mbili, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi lakini pia Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa kweli mnayo nafasi ya kumtaka Gavana wa *BoT* aje ndani ya Baraza la Wawakilishi atuelezee madhumuni ya kuanzishwa *BoT*, ilianza anzaje, hisa za Zanzibar katika uwezeshwaji wa *BoT*, lakini vile vile lengo na madhumuni ya uanzishwaji wa *BoT*.

Mhe. Mwenyekiti, bado Zanzibar *BoT* hatujaitumia vile ipasavyo. Ukiacha ule ushauri wanaoutoa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar lakini *BoT* kazi yake vile vile kuweza ku-*regulate* uchumi wa nchi zetu hizi mbili.

Lakini bado wakifanya kazi wao peke yao bila na sisi kuelewa majukumu yao kuna mambo mengi ambayo yanaleta changamoto sasa hivi ndani ya bajeti yetu ya serikali kwa kifupi ilikuwa inatakiwa *BoT* lazima waingize mkono wao ili kuweza ku-*stabilize* uchumi wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni kuna matukio yamejitokeza ambayo yanaweza yakavuruga mpaka makusanyo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nafikiri nitakapoendelea mbele nitakapofika kwenye eneo la *TRA* nitajaribu kuelezea maeneo yake.

Kwa hiyo, sisi kipindi cha nyuma kwa kweli tulifika pahala mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi na tulimwita hapa Gavana Profesa Benno Ndulu alikuja hapa akatueleza na sisi tukamueleza yetu, kimsingi tulipata kujua nini hasa kazi za *BoT*. Kwa hiyo, ndio maana nikasema kwa kuwa wajumbe zaidi ya asilimia 70 ni wapya katika Baraza hili inahitaji na wao waje wapate hiyo dozi ili wafahamu hasa nini majukumu ya *BoT*. *BoT* sio kazi yao kushauri serikali tu, pia kusaidia sekta binafsi *small and medium enterprise* kuweza ku-*boost* kiuchumi na kuweza kupata mitaji kwa ajili ya kuanzisha biashara zao.

Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, *BoT* ni chombo muhimu kwa taifa letu tunaomba sana wenyeviti mfanye jitihada kumtaka Gavana wa *BoT* aje hapa, na sio atuletee wasaidizi wake aje yeye mwenyewe kwa sababu kuna mambo mengi yeye anakuwa ndie muamuzi wa mwisho. Kwa hiyo, ni vizuri tumpate hapa ili tuweze kupata uelewa mzuri ili na sisi aweze kuelewa changamoto za uchumi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nikija ukurasa wa 13 wameelezea Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Mhe. Mwenyekiti, tumeona maelezo ya kamati, kwa kweli kuhusu miradi ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wametueleza katika changamoto zake. Moja, hapa katika changamoto wametueleza kwa kipindi kirefu mfuko umekosa wabia wa kushirikiana nao katika uwekezaji mbali mbali kwenye miradi mikubwa kwa lengo la kugawana tija na athari za miradi inayowekezwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa sababu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti yeye anakwenda kukagua na kuangalia na kutoa ushauri, lakini kwa kweli Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi yeye ndie anayewajibika kabisa na Wizara ya Fedha na Mipango na

mashirika taasisi zilizokuwepo chini yake. Tuwatake sasa *ZSSF* hii changamoto ya kukosa wabia kuingia katika miradi hapa inatokana na kwamba miradi wanayoibuni inaonesha tija yake ni ndogo, lakini vile vile pengine itachukua muda mrefu kuweza kurejesha ile *Capital Investment*. Kwa hiyo, sasa hivi kama tunavyofahamu kwamba nchi yetu inategemea zaidi uchumi katika sekta ya huduma ya biashara.

Kwa hiyo, kitu ambacho ninachokiomba *ZSSF* tumeona miradi yao wanayoifanya, hapa imeelezwa na kamati kwamba ukiangalia sasa hivi katika uendeshaji wa Kiwanja cha Kariakoo tokea ulipoanza shughuli za sherehe hasa katika masuala ya *weekend* na mambo mengine, kuanzishwa kule Fumba kwa kweli soko la kiwanja chetu cha watoto hapo Kariakoo mapato yake yameshuka. Pia nimesikia katika vyombo vya habari jana na leo tayari wamejaribu kupunguza mpaka kiingilio cha uwanjani ili kuweza kuwavutia.

Mhe. Mwenyekiti, lakini sasa *issue* sio kiingilio kuna mambo mengi mle yanahitaji kuboreshwa. Mimi nadhani wakae *ZSSF* kuna baadhi ya wajumbe waliwahi kuchangia asubuhi hapa kama tunahisi ni tatizo kuendesha sisi wenyewe, basi tukodishe tuangalie tutaweza kupata kiasi gani. Tukodishe kwa masharti maalum ili vile vifaa vyetu viweze kutunzwa. Vile vile utaratibu wa kukusanya pesa mkononi mambo haya kwa kweli yameshapitwa na wakati nafikiri sasa hivi turudi katika ile *electronic system* ya kuweza kukusanya fedha.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kitu ambacho ninachokiomba *ZSSF* watafute mchumi akae pale aweze kubuni miradi ambayo italeta tija kwa sababu zile ni pesa za walipa kodi, ni pesa za wastaafu, ni pesa ambazo wenyewe wanahitaji kwamba kuwe na *liquidate* pale unapofika muda wa kustaafu waweze kupata pesa zao, vile vile ile miradi iwe na tija. Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti,

ZSSF miradi ambayo wanaibuni wasipate sana *pressure* kutoka kwa watu mbali mbali. Waweze kubuni miradi yao wao wenyewe na wakimpata mchumi mzuri pale naamini kiwanja kitakwenda, kama sio hivyo basi ni vizuri viwanja wakavikodisha ili kuweza kuleta tija na wao kuondokewa na *pressure*.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu nakuja katika ukurasa wa 14 Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi *ZIPA*.

Mhe. Mwenyekiti, moja katika changamoto Mwenyekiti ambayo ameieleza ni kutokukamilika huduma kwa *One Stop Centre*. Mhe. Mwenyekiti, hili narejea tena kusema juzi nilipokuwa nachangia Kamati ya Fedha na Uchumi nilizungumza kwamba Waziri wa Fedha aliyepita kipindi kile alikuwa Mhe. Omar Yussuf Mzee tulizungumza sana kuhusu *ZIPA* kwamba wanafanya maamuzi halafu bado miradi inakuwa haitekelezeki. Na tulitegemea *ZIPA* iwe ni *One Stop Centre* ili pale Wajumbe wa Bodi ya *ZIPA* wawe ni watu ambao wenye maamuzi, na kipindi kile Mhe. Waziri wa Fedha alitueleza kwamba pale watakuwepo Makatibu Wakuu, kwa sababu Makatibu Wakuu katika wizara zao wale ndio wanakuwa ni waamuzi wa mwisho baada ya mashauriano na waziri. Lakini sasa leo Mwenyekiti bado anatuletea changamoto hili inaonesha lile donda bado ni ndugu halijapata dawa tunaomba sana *ZIPA* iwe *One Stop Centre* kweli.

Mhe. Mwenyekiti, wawekezaji hapa wakati mwengine wanakuja kutokana na urasimu inawezekana *ZIPA* tayari wameshatoa kibali ardhi hawajatoa *lease*, wakati mwengine ardhi wameshatoa *lease ZIPA* hawajatoa kibali, wakati mwengine watu wanataka kufanya mradi unaambiwa ramani ya mipango miji na vijiji bado haijakaa sawa. Kwa hiyo, hii bado inakuwa ni usumbufu na wawekezaji wanakimbia.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu wa Rwanda sasa hivi ndani ya siku mbili mradi tayari mwekezaji ameshapata sehemu ya kuwekeza, tena wenzetu wanajaza *online*. Unajaza wewe kule unakokwenda unakwenda ku-*sign* mikataba unapewa eneo kwa ajili ya uwekezaji. Sasa tunaomba sana *ZIPA* iwe kweli *One Stop Centre* ili iweze kufanya kazi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, tuliwahi kwenda Dar es Salaam namshukuru sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko aliwahi kunialika katika ziara yake moja tulitembelea *EPZ* Dar es Salaam. Kwa kweli kule tulipokwenda tumeikuta ile taasisi ya uwekezaji kule Jamhuri ya Muungano wenzetu wako *sharp* kweli kweli, na ndio maana sasa hivi katika huu uanzishwaji wa viwanda leo Mkoa wa Dar es Salaam una viwanda karibu mia tatu na zaidi. Kwa sababu wakienda pale katika kituo cha uwekezaji mara moja wanapata vibali, mara moja wanapata *facilitation*, na yule Mkurugenzi wa *ZIPA* yeye mwenyewe ndio anahangaika katika taasisi nyengine kuweza kukwamua wale wawekezaji waweze kuwekeza kwa haraka haraka. Sasa naomba sana *ZIPA* na wao kwa kweli wawe *aggressive* waweze kuhakikisha kwamba miradi inayokuja pale haikwami.

Mhe. Mwenyekiti, suala la changamoto ya gari ni kweli, hili kwa kweli lazima tulivalie njuga, katika bajeti ya mwaka huu lazima *ZIPA* wahakikishe wananunua gari ili kuweza kushughulikia masuala ya uwekezaji. Kwa sababu uwekezaji haukai ofisini, uwekezaji unakwenda katika maeneo tofauti tofauti na maeneo mengine yanakuwa ni mbali kama hawana usafiri itakuwa ni vigumu kuweza kupatikana uwekezaji kwa haraka.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile changamoto nyengine imeelezwa kukosekana kwa *master plan* hasa katika miradi ya uwekezaji wa ujenzi wa nyumba.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nilipokuwa nasoma ripoti yangu nimeelezea na hili kama serikali haijalifanyia marekebisho kwa kweli *master plan* itakuwa ni nyimbo. Leo ukiangalia Kamisheni ya Ardhi inaingiziwa *OC* moja, *OC* zile zinagawanywa kwa idara nne, idara moja wapo ni Idara ya Mipango Miji. Leo utegemee kwa kutegemea *OC* moja ya Kamisheni ya Ardhi ambayo msimamizi ni Katibu Mtendaji ikagawanywe kwa idara nne, Idara ya Mipango Miji, Idara ya Usajili wa Ardhi *just* tunacheza. Kwa hiyo, mimi kitu ambacho ninachokiomba katika bajeti ya mwaka huu inayokuja na safari hii serikali wanaponiletea bajeti ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira sitokubali Kamisheni ya Ardhi ikawa inatengewa fungu moja kwa *OC*. Nataka kila idara iweze kupangiwa fungu lake ili iweze kutekeleza majukumu yake.

Leo ukienda hiyo Idara ya Mipango Miji hata Mkurugenzi gari hana, anaendesha gari yake mwenyewe, idarani hapana gari, Mipango Miji watakwenda kuipanga nini kwa miguu. Kwa hiyo, sio kitu rahisi lazima tuandae utaratibu wenzetu tunawapa majukumu tuhakikishe tunawapa na nyenzo ili waweze kwenda kufanya kazi. Kwa hiyo, *ZIPA* wataendelea kukwama katika hii miradi kwa sababu wenzao ambao wao ndio wanatakiwa watengeneze *master plan* fedha hakuna, *OC* ni chache kwa hiyo utakuta na *ZIPA* itabidi lazima watakwama katika hii miradi mengine ya uwekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto nyengine imeelezwa hapa Mradi wa Uvuvi kukwama. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana, hapa Mwenyekiti ametueleza kwamba kuna baadhi ya watendaji wamefika mpaka kwenda Korea kwa ajili ya kuona jinsi gani miradi ya uwekezaji hasa katika Sekta ya Uvuvi wapo tayari wenzetu kuja kuwekeza. Lakini mpaka leo bado wawekezaji hawa hawajaweza kufuatiliwa.

Kwa hiyo, mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti hebu andaa safari nyengine, katika hii safari ya Korea mara hii hebu na mimi nichukue, halafu twende pamoja na Waziri wa Fedha na Mipango tuangalie kwamba uwekezaji utakuwepo au hautokuwepo. Kwa hiyo, mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu vitu vyengine vinatakiwa uone *physical* halafu sasa uje ujenge hoja, lakini sasa ukiwa unaangalia tu kwenye makaratasi, kwenye mambo gani haya huwezi ukahakikisha kwamba mambo yanakwenda sawa. Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, tunataka uwekezaji uje, na kama alivyosema mwenzangu alizungumza pale Mhe. Miraji Khamis Mussa, uwekezaji katika sekta ya uvuvi kama tutausimamia vizuri hii nchi itapiga hatua sana za maendeleo.

Kwa sababu nchi yetu imezungukwa na bahari, visiwa vyote vimezungukwa na bahari, leo hatuna mradi hata mmoja wa uvuvi, kwa kweli hii ni aibu, lazima tuhakikishe kwamba miradi hii ya uvuvi inakuja hapa Zanzibar na kwa kuwa wawekezaji wapo tuwape moyo ili waweze kuwekeza. Tena kwa bahati nzuri wao walitaka kujenga bandari eneo la Fumba, na bandari ile wangeitumia wao kwa shughuli za uvuvi lakini mpaka na wananchi wengine. Lakini mpaka leo sijui mradi huu umekwama wapi, pamoja na kwamba ripoti hizi jawabu zake tutazipata mwezi wa tisa, lakini naamini mawaziri wajiandae wakati wa bajeti tutayarejesha haya ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inapata maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, nishakuona dakika zangu tano zilizobakia naomba nimalizie haraka haraka.

Mhe. Mwenyekiti, eneo la uwekezaji Amani maeneo huru. Mhe. Mwenyekiti, hapa pana changamoto mimi mwenyewe pale huwa nakwenda sana vijana wetu wanalalamika na hili naomba Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti utakapofanya ziara zako nyengine uende pale *Amani Industrial Park* uzungumze na

wafanyakazi. Wafanyakazi wanalalamika lile agizo la serikali la kima cha chini cha mshahara bado wawekezaji katika *Amani Industrial Park* halitekelezwi vijana wetu tunahitaji walipwe kwa mujibu wa serikali inavyotaka.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie kwa haraka haraka suala la *Penny Royal*. Mhe. Mwenyekiti, hapa mimi kidogo sikubaliani na ripoti ya Mwenyekiti alivyoieleza. Hii changamoto iliyokuwepo hapa kwa kweli sio suala kwamba wamezuiwa *Lease Penny Royal*. Kwa sababu mimi sio mdau wa *Penny Royal* lakini ni mshiriki mkubwa sana tokea jinsi walivyokuwa wanakwama tulikuwa tunasaidiana.
Mhe. Mwenyekiti, mimi namshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kulikuwa kuna tatizo kweli katika suala zima la ile *tax holiday*, kwa sababu wale walikuwa kwa ile sheria ya mwanzo ilikuwa *tax holiday* ni mwaka mmoja na nusu. Lakini baada ya kupeleka *claim* Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango nashukuru wamekaa nao, tayari Mhe. Waziri wa Fedha amerekebisha kanuni ambayo wale wanaweza wakapata *tax* ya *five years* kwa ajili ya uwekezaji. Lakini bado ile kanuni ambayo Mhe. Waziri aliyorekebisha kupitia Wizara ya Fedha kuna sheria nyengine ya ardhi bado inabana. Na hapa Mhe.

Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa bahati mbaya hayupo hili suala lipo kwa Mhe. Waziri wa Ardhi. Mimi nimejaribu pia kufanya mawasiliano na watendaji wa Kamisheni ya Ardhi suala lililokuwepo Mhe. Mwenyekiti, sheria ya ardhi mpaka sasa hivi bado haijakubali ile *tax holiday*. Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Ardhi walete marekebisho ya haraka haraka ya ile sheria ya ardhi ili mwekezaji wa *Penny Royal* aweze kupata uwekezaji wake.

Kwa hiyo, *Penny Royal* waliwahi kupata *lease* ya mwanzo, lakini ile *lease* ya mwanzo kuna marekebisho ambayo waliomba kufanya na tayari marekebisho yale yamefanywa. Lakini kama hakijaondoka kikwazo cha kisheria basi itabidi Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira atoe dokezo awape Kamisheni ya Ardhi ili waweze kuwapatia *lease*. Lakini ile *lease* ya Marina pia kuna mapendekezo ya kitaalam kwa sababu eneo lile linatumiwa na wavuvi wote wa upande wa Kaskazini na wakati upepo unapokuwa mkali sehemu ile wanakimbilia kwa ajili ya kwenda kujificha.

Sasa *Penny Royal* wameomba *square kilometer* 40. Mapendekezo yaliyokuja *at least* waweze kupewa kama *square kilometer* 25 au 30 lakini na wananchi waweze kupata *access* ya kuweza kutumia eneo lile. Wataalam wanasema kwamba wakiwapa eneo lile lote ina maana wananchi watakuwa hawana tena *access* ya kuweza kutumia eneo lile jambo ambalo kimazingira vile vile linaweza likatuletea tafrani. Sasa mimi kitu ninachokiomba mawaziri wakae pamoja na wataalam pamoja na wenyewe *Penny Royal* ili kukubaliana katika suala hili, kwa sababu ule mradi ni mkubwa utaweza kutangaza uchumi wetu, utaweza kutangaza utalii wetu na utaongeza ajira nyingi, lakini mradi umekwama na wale sasa hivi kila siku watatumia fedha.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa dakika moja nazungumzia eneo la Mangapwani. Mhe. Mwenyekiti, eneo la Mangapwani sasa hivi imekuwa changamoto kubwa na hizi foleni foleni za mafuta zilizokuwepo sasa hivi hazitoweza kumalizika kama hatujaweka miundombinu ya matenki ya mafuta kule Mangapwani. Mhe. Mwenyekiti, meli yoyote hata hiyo meli tuliyotengeneza sasa hivi ya mafuta ya serikali haiwezi ikafunga gati kwenye bandari ya Mtoni, itakuwa sawa sawa tumenunua chombo lakini tunashindwa kukitumia.

Eneo la Mangapwani lina kina kirefu cha maji ma-*investor* wapo tayari kujenga matenki wakae pamoja. Juzi nilizungumza Tume ya Mipango ikae na wale wadau, wadau waliokuwepo Mtoni lakini na wale waliopata *lease* kule Mangapwani wakae washauriane namna gani waweze kuboresha miundombinu. Wawekezaji hata kesho wakiambiwa waanze kujenga matenki ya mafuta pamoja na bandari ya kuingiza mafuta wapo tayari. Leo tunaambiwa sijui kamati wanashauri, sijui wakachukue mafuta Mtwara, wakachukue mafuta Tanga bado tunacheza tu, tengenezeni kwetu fedha zipo, watu wapo wapewe *go ahead* watengeneze ndani ya mwaka mmoja tutaweza kupata uwekezaji mzuri pale.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ripoti hii ni kubwa na nzito lakini muda mchache, lakini pia nakushukuru kuweza kunivumilia kunipa nafasi hiyo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa. Sasa namwita Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi akifuatiwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi pamoja na Mhe. Omar Seif Abeid nae ajitayarishe.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi niwe mmoja kati ya wachangiaji katika ripoti yetu hii adhimu ya bajeti. Kwa kweli kwanza nianze kwa kuwapongeza Wizara ya Fedha na Mipango kwa namna wanavyoendesha majukumu ya kifedha ambapo hali ya uchumi inaonesha kukua ukilinganisha na vipindi vilivyopita.

Pili, niipongeze Kamati hii ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Mohammed Said Mohammed kwa kazi nzuri sana waliyoifanya kupitia haya waliyoyapitia wakatuletea ripoti hii ambayo kwa kweli inafahamika. Hongereni sana kamati.

Tatu, niwapongeze wana kamati wote kwa kweli kwa sababu mambo yote yaliyoelezwa katika kamati yanahusu bajeti na wao wameeleza kwa njia moja au nyengine mambo yanayohusu bajeti. Kwa hiyo, wote nawapongeza kwa kazi nzuri waliyoifanya na nategemea kwamba mapendekezo yaliyotolewa na hii ripoti ya bajeti pamoja na mapendekezo yaliyotolewa na kamati nyengine yatafuatwa kwa lengo la kuleta mustakabali mwema katika kuendesha nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naingia moja kwa moja kwenye mapato na matumizi kama yalivyoainishwa hapa. Hapa tumeambiwa kwamba katika kipindi cha Januari-Juni, 2017 ingawa hatukuoneshwa malengo yalikuwa kiasi gani lakini mapato yaliyokusanywa yalikuwa ni bilioni 142.15, ukitizama matumizi yalikuwa bilioni 171.10, hii inaonesha kwamba tunatumia zaidi kuliko tunavyopata. Sasa ukichukua kwamba dunia nzima sasa hivi inatakiwa iende kijasiriamali kila kazi inayofanywa basi iwe angalau inalipa hata kama si kazi ya kutumia fedha, kazi hiyo iwe inalipa. Kama unafyagia basi ufanye kazi ya kufyagia ilingane na mshahara wako. Sasa kama mapato yetu yanakwenda namna hii tunapata mapato madogo lakini matumizi yetu makubwa, nadhani hata kibiashara hii haikubaliki.

Kwa sababu kama ni biashara ita-*collapse* tu haiwezi kuendelea, itakufa biashara. Kwa hivyo, mimi nashauri katika hili kwamba ule utaratibu mliouleta Wizara ya Fedha wa *Smart Budgeting* hapa sasa ufanye kazi. Pamoja na kwamba kuwe na *Smart Budgeting*, lakini pia kuwe na *long* na *short term planning*. Hii *short term planning* pengine miaka mitatu, *long term* pengine ichukue miaka mitano mpaka kumi. Sasa hii itatusaidia kila mara ku-*review* ni wapi tumeteleza, ni wapi panahitaji kuongezeka, ni wapi panahitaji kufanywa nini, ili twende mapato yawiane na matumizi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda kwenye ukuaji wa pato la taifa ambao tumesema kwamba, pato la taifa limekua kwa asilimia 6.3 kwa mwezi huu wa Januari - Juni ikilinganishwa na asilimia 5.2 kwa mwaka 2016. Sasa ukuaji sawa kuna ukuaji mzuri sana hapa ni sawa kabisa tunakua, lakini ukiangalia ile *purchasing power parity* ya watu, ule uwezo wa kununua bidhaa watu wenyewe kwa kweli umeshuka lakini bei imepanda. Sasa hapa tunalazimika tuwe na *price control mechanism* ambayo kwa kweli itakuwa inasimamia biashara, inajua nje wananunua kiasi gani wakileta hapa wauze kiasi gani, bila ya hivyo tutawaachia wafanyabiashara wengine walisema hapa mfanyabiashara hana dini yeye dini yake ni mapato zaidi, akipata zaidi basi yeye ndio furaha akikosa anaona tabu. Kwa hivyo, ukiwa na *price control mechanism* najua ipo lakini ifanye kazi basi itakuwa huu uuzaji bei kubwa kiholela utapungua sana.
Halafu kuna mfumko wa bei sasa. Katika hili ndio huo mfumko wa bei ambao nimeusema hapa kwamba bei zinapanda katika soko. Mambo yote yanategemea *market process* tunasema, na *market process* inategemea sana na *demand and supply. Supply* ikiwa kubwa basi bei zitashuka, *demand* ikiwa kubwa basi *supply* inaweza ikapungua, kwa sababu watu wanataka mengi lakini hayapo. Tukilinganisha sasa biashara zetu sisi Wazanzibari na ndugu zetu wa hapo Bara utaona sisi tunanunua vitu vingi zaidi kuliko tunavyouza kwao.

Sasa hii kidogo inashangaza kwa sababu sisi kinchi kidogo tuwe tunanunua zaidi, wao nchi kubwa kabisa kama ile inanunua kidogo. Iko haja ya kuangalia kuna matatizo gani ya kibiashara yarekebishwe sisi hapa tuonekane tunauza kingi kwa sababu kule ni kukubwa kuna mikoa isiyopungua 32 na kila mkoa pengine Zanzibar hizi zinaweza kutoka tatu, kuna mikoa mingine hata nne. Kwa hivyo, kama tutafanya biashara zetu kweli kila mikoa kule tukasambaza biashara vizuri zinakwenda, kuna maelewano mazuri basi lazima tunachopeleka sisi kitakuwa kingi kwa sababu kule ni

kukubwa. Kwa hivyo, hapa iko haja kabisa kuangalia namna ya biashara zetu hapa ndani zinavyokwenda.

Sasa niingie kwenye *ZSSF*. Naeleza kwa kifupi sana kwa sababu nasema karibu kila kamati imeeleza mambo haya yanayohusu mapato na matumizi na uadilifu katika kufanya kazi. Kwa hivyo, nikizidi kusemea tutakuwa tunarudia, pamoja na kwamba hatupotezi muda tunachangia lakini itakuwa tunarudia yale yale.

Niingie kwenye *ZSSF*. Hapa wamesema jumla ya wanachama 81,477 wamesajiliwa pamoja na uwekezaji wa miradi minane mikubwa. Ninachotaka kusema kwenye *ZSSF* ni kwamba, kuna mambo mengi sana ya kuyafanya. Kwanza wafanyabiashara binafsi na watu wengine hao wadogo wadogo na wakubwa bado *ZSSF* haijawachukua wakawa ni wanachama ambao nao wana-*contribute* kwenye Mfuko wa *ZSSF*. Nadhani iko haja kama wamechukuliwa basi wachukuliwe na wale hata wafanyabiashara wadogo wadogo.

Mimi nadhani niliwahi kushauri siku moja, *ZSSF* tuna bandari zetu kama pale Mkokotoni na kwengineko, pale *ZSSF* ikafanya kujenga kigati kidogo watu wakapata pa kuegesha zile boti wananchi wetu wakaweza kupata mapato, hata kama ni shilingi mia kwa boti moja kwa siku watu wataweka. Kuna watu wengine wanaweka maboti yao asubuhi anakwenda limeshapwerewa hawezi kwenda hata kazini. Sasa wakijengewa wakafunga gati wakaweza kwenda kazini kwao kwa urahisi basi nadhani *ZSSF* inapata mapato na wakati huo huo itakuwa ni rahisi wananchi kuweka pahala pa usalama, vyombo vyao wakati wowote wakitaka kwenda baharini wanaweza wakenda.

Sasa niingie tena kwenye mradi wa *Penny Royal*. Huu kwa kweli ni mradi mkubwa sana na naipongeza *ZIPA* sana wanajitahidi, lakini wanadai kwamba mashirikiano baina ya wao na wizara

nyengine za kutoa *decision*, wana *decision makers* wengine wanachelewesha maamuzi ambayo wanatoa *ZIPA*. Kwa hivyo, nashauri wale wote wanaohusika na kutoa vibali kwa kuharakisha vibali hivyo vipatikane. Kwa sababu mwekezaji anakuja na pesa zake hapa anataka afanye kitu mara moja kiwe, aweze kuendeleza biashara zake apate yale mapato aliyokusudia, ukimcheleweshea ina maana fedha zake zinapotea bure kwa muda wote atakaowekeza. Kwa hivyo, tukifanya bidii tukawapatia vibali vyao kwa wakati sisemi kwamba hata kama ana matatizo apewe aa, mwenye matatizo awekwe pembeni, aliyekuwa ana matatizo asipewe lakini aliyekuwa hana matatizo iharakishwe apewe aendeleze biashara zake.

Sasa hapa kwenye hii *Penny Royal* nadhani kuna tatizo la kutoa *specification* kama *Penny Royal* kaja akakubali kupewa eneo halafu baadae hajamaliza anataka eneo jengine, nadhani kama nimefahamu hilo ni tatizo. Tatizo tangu mwanzo hatukumwambia kwamba wewe tunakupa eneo hili na ulitumie hili hili. Sasa anakuja anataka eneo jengine la kilomita si chini ya 220 kama sikosei, hizi zinatoka wapi. *Okay* kama zipo sawa, lakini kama hazipo tutafanya nini. Ni kwamba bora anapokuja mwekezaji aseme vile anavyotaka na sisi tuweke *specification* zetu kwamba sisi ukitaka kuongeza utakuwa na hivi na vile. Kwa hivyo, mtu anakuja anajua kwamba mimi hapa nikitaka kuongeza kutakuwa na ugumu fulani, hivyo najipanga kufanya hapa hapa au najipanga kukabiliana na hayo nitakayoambiwa kwenye mkataba.

Sasa pia kuna matatizo ya wananchi kwa maeneo haya ya kuwekeza, wananchi wanadai. Mwananchi akishaona pana pesa basi atataka zile pesa azipate kwa wingi kama inavyowezekana, mnazi atataka apewe shilingi milioni kumi au tatu, eneo lake dogo atataka apewe pesa nyingi ili ajiokoe na umaskini. Sasa kutokana na hayo nadhani iko haja wananchi waelimishwe umuhimu, kwa sababu inapokuja miradi kama ile wao wenyewe ndio wanapata

ajira pale tena ajira zenyewe zitakuwa za kudumu hasa wale wa maeneo ya jirani. Kwa hivyo, waelimishwe juu ya umuhimu wa mradi ili wasiweke vikwazo, kwa sababu hawa wakiachiwa wanalalamika wananyimwa mwisho wake itakuja kuwa matatizo ya kupigana.

Jambo jengine ni uvamizi sasa. Wananchi wanaweza kuwa wanavamia maeneo na haya pia yachukuliwe hatua. Mahala kama panawekezwa pawekewe ulinzi wa kutosha ili maeneo yale yasivamiwe ikaja ikasababisha tena wananchi wakaja wakaanza kudai fidia nyengine.

La mwisho ambalo nitapenda kupendekeza hapa ni kwamba huu utaratibu wa mipango miji mbona upo kwenye karatasi kwa muda mrefu sana, kwa nini tusianze kuutekeleza. Nadhani iko haja sasa huu utaratibu wa mipango miji ufanyiwe haraka haraka ili hawa wawekezaji nao wajenge kwa mujibu wa mipango miji inavyotaka.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi sitaki niendelee tena kwengine zaidi kwa sababu wenzangu wamechangia na kwenye ripoti nyengine yamechangiwa hayo hayo. Kwa hivyo, narudia kuwapongeza sana wana kamati hawa kwa busara zao za kuleta bajeti hii na naipongeza Wizara ya Fedha na Mipango yenyewe kwa kuweka mikakati mizuri ya kuendeleza suala la uchumi. Baada ya hapo pia nipende kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi kwa mchango wako. Waheshimiwa Mawaziri ripoti iliyopo mbele yetu inahusu wizara nyingi au takriban zote, lakini watendaji wenu siwaoni hapa, sijui ripoti hii itakuwa anapewa na nani. Naomba utulivu, kwa hivyo, niwatake watendaji wenu wafike haraka ili

haya tunayozungumza yaweze kudhibitiwa. Tunaendelea. *(Makofi)*

Anayefuata sasa ni Mhe. Rashid Makame Shamsi akifuatiwa na Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi ili niweze kuchangia juu ya ripoti hii ya Kamati ya Bajeti ya Baraza iliyowasilishwa na Mwenyekiti Mheshimiwa makini Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae ndugu yangu Mohamed Said Mohamed.

Kwanza nimpongeze sana Mhe. Mwenyekiti na kamati yake kwa ripoti nzuri ambayo wameileta, lakini vile vile kwa kufuatilia kwa kina katika sekta mbali mbali hususan kuhusiana na masuala ya kibajeti. Vile vile nichukue fursa hii kuweza kuwapongeza wenzangu wote ambao wamenitangulia kwa kuitendea haki, kuichangia hotuba hii muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kibajeti ni suala moja muhimu sana, kwa hivyo, wenzetu wana kazi kubwa sana kuweza kuona kwamba bajeti ambayo imepitishwa na Baraza hili inatumika kwa yale malengo ambayo yamekusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu wenzangu wengi wamechangia mimi nikazie kazie tu. Kwanza nianze ukurasa wa 13 wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ambapo wenzetu wameweza kuonesha changamoto mbali mbali zihusianazo na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa huu wa 13 pamoja na maendeleo ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na nipongeze sana uongozi wa mfuko kwa juhudi zao katika kuona kwamba fedha hizi za wananchi na hususan wafanyakazi wanazifanyia maarifa

mbali mbali ili kuweza kuendelea kuwepo ili pale wanapostaafu waweze kupata haki zao.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kuanzisha miradi katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa fedha za michango ya wafanyakazi ni suala muhimu na sio suala geni katika mifuko ya aina hii. Lakini kutokana na changamoto ambazo zimejitokeza na hapa nimpongeze sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwa ufafanuzi wake mzuri lakini inatia wasi wasi kwa sababu lengo la mfuko kuweza kuwekeza ni kuweza kuukuza ule mfuko wenyewe kwamba uwe unazalisha faida kwa ajili ya sisi wafanyakazi kwa sababu na mimi ni mmoja wa wanachama. Sasa itakapokuwa miradi ambayo wenzetu wanaibuni lakini inaonesha viashiria ambavyo pengine inawezekana ikawa haina tija au ikakosa ile tija ambayo inakusudiwa, hii inawezekana ikawa ni hatari kidogo.

Sasa niwaombe sana wenzetu mfuko kama ushauri uliotolewa na kamati naungana nao, vile vile ushauri wa Mhe. Hamza naungana nao, lakini mfuko lazima uwe makini katika kuwekeza. Kwa sababu vyenginevyo fedha hizi za mfuko ambazo zimewekezwa pale ambapo hazitorudi au hazitoleta tija maana yake wanaoathirika au watakaoathirika ni sisi wafanyakazi na hususan katika muda wetu wa kustaafu. Kwa hivyo, niombe sana, niuombe sana mfuko kuweza kujitahidi katika kuwekeza ile miradi ambayo itakuwa na tija na mfuko huu ili sisi wastaafu wa baadae tukija tukitaka haki zetu iwe zinapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Shirika la *ZSTC* katika ukurasa wa 24. Katika ukurasa huu wenzetu wameweza kuelezea juu ya shirika hili maendeleo yake na changamoto zake, lakini nilipongeze shirika hili kwa juhudi zake kutokana na majukumu yake mbali mbali na hususan katika kushughulikia biashara ya zao la karafuu ambalo ni muhimili mkubwa wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika changamoto kuna changamoto ya uchakavu wa maghala. Hivi sasa maghala ni sehemu ya chanzo kikubwa sana cha mapato. Wafanyabiashara au watu mbali mbali wenye uwezo hivi sasa wanawekeza katika kujenga maghala ili kuweza kuyakodisha kwa wafanyabiashara mbali mbali. Kodi za maghala hivi sasa ni kubwa sana, kwa hivyo kuweza kushuhudia kama *ZSTC* ina maghala na yanaendelea kuvuja au kuendelea kuchakaa bila ya kuleta tija nafikiri sio suala zuri katika mtazamo wa kuipatia serikali mapato. Ningelishauri sana shirika hili na mimi ninavyoona kwamba kutokana na biashara ambayo wanafanya uwezo wa kuweza kuyafanyia ukarabati maghala haya inawezekana. Kwa hivyo, wayafanyie ukarabati maghala haya ili yawe ni sehemu ya chanzo cha mapato ukiacha vile vyanzo vyengine vya karafuu.

Vile vile imetajwa changamoto ya mashine ya kusafishia karafuu ambayo kwa mujibu wa maelezo ya kamati mashine hii ni ya kizamani haiendani na wakati uliopo. Kwa hivyo, ningeishauri sana kwa sababu kila mara shirika hili linajaribu kuweza kupanga mipango yake ya kuwa na ubora katika zao la biashara ili kuweza kupata soko zuri ulimwenguni, basi ni vyema kuweza kufikiria kuwa na mashine ambazo zitakuwa zinaendana na wakati katika suala zima la kusafisha zao letu hili muhimu la biashara hapa nchini. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nimeingia wasi wasi kidogo na changamoto ya ukosefu wa huduma za kibenki katika Shirika hili la *ZSTC* hususan katika vile vituo vya uuzaji wa karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Rais wetu wa Zanzibar kwa kuweza kuimarisha na vile vile kupandisha ile bei ya zao la karafuu. Kwa tunakotoka hivi sasa bei ya karafuu kwa kweli ni nzuri na ni kubwa mno, lakini itakapokuwa inatokezea katika vituo vya kuuzia karafuu hakuna huduma za kibenki. Hii inaonesha kwamba wafanyabiashara wa zao hili wanapokwenda kuuza maana yake wanaondoka na fedha mikononi. Na kutokana

na thamani nzuri ya karafuu kuna wafanyabiashara wengine wanauza magunia kwa magunia na inawezekana wanaondoka na fedha kwa mamilioni.

Kwa hiyo niombe sana Shirika la *ZSTC* moja kati ya haya, aidha, wale ambao wanauza bidhaa hii au karafuu na mapato yao yanakuwa ni makubwa basi labda wawe na utaratibu wa kuweza kutoa cheki ili kuweza kuwahakikishia usalama wa fedha zao pale ambapo wanauza karafuu.

Lakini jengine nafikiri ni suala la kuzungumza na taasisi za kifedha na hususan benki yetu ya Zanzibar katika vituo mbali mbali katika zile siku za mauzo basi kuwe na ile *mobile bank,* ili kuweza kuwarahisishia wenzetu kuweza kuzihifadhi fedha zile baada ya kukabidhiwa pale wanapouza karafuu, ili kuweza kuhakikisha usalama wa fedha zao. Vyenginevyo wale wenye njia za mkato kuna hatari ya kuja kuwavizia njiani na kuweza kuwanyang'anya fedha zile ambazo wameuza karafuu na pengine wakati mwengine ni wale wale ambao wamechukua mkopo katika mashamba ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, nije na changamoto ya mamlaka ya *ZURA* ukurasa wa 38. Mhe. Mwenyekiti, katika kikao chetu hiki tumekuwa tukipiga kelele sana juu ya suala zima la mafuta na Mhe. Hamza Hassan Juma amelizungumza hivi punde nimpongeze sana na niunge mkono sana mawazo yake.

Lakini pamoja na mawazo yake hayo mazuri ambayo inawezekana yakachelewa kwa sababu yanahitaji mipango, yanahitaji mtaji lakini ukweli tumefikia pahala ambapo sio pazuri katika lile lengo la kukuza uchumi wa nchi. Kwa sababu tunapoathirika katika Sekta ya Usafiri maana yake unakuwa unaharibu zile harakati zote za mwanaadam za maisha zikiwemo zile harakati za kiuchumi. Juzi tulizungumza juu ya kadhia

wanayoipata watalii na kuathiri Sekta ya Utalii pale yanapoadimika mafuta.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mpaka hii leo nakuja huku Barazani bado kuna foleni za mafuta katika sheli mbali mbali. Waziri alitoa tamko lakini mpaka leo nchi hii ina tatizo la mafuta. Sasa hii ni hatari kwa maendeleo ya uchumi wa nchi yoyote ile duniani, kama tunaadimikiwa na mafuta wiki moja kwa sababu uadimikaji wa mafuta ulianza toka Ijumaa iliyopita mpaka Ijumaa hii ya leo. (*Makofi*)

Sasa na mafuta tunayachukua Dar es Salaam ni mwendo wa masaa kidogo tu. Lakini sasa inawezekana kunahitaji mipango mizuri, kunahitaji utaratibu nzuri wa kuweza kuona kwamba kwa hizi hizi *facility* ambazo tunazo ufinyu wa *storage* zetu, basi tuweze kuona kwamba mafuta hayaadimiki. Lakini hii ikiendelea hivi kwa kweli yale malengo ya kukuza uchumi wetu yatakuwa yanaathirika. Lakini vile vile kipato cha mtu mmoja mmoja kwa sababu tunategemea sana sekta ya usafiri katika miradi mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, nimesikitishwa kidogo kukosekana kwa kifaa hiki cha kupimia mafuta *flow meter* katika *depot* yetu. Mimi nafikiri wajanja wanaweza wakaitumia fursa hii katika kuweza kupunguza kile kiwango ambacho wanaingiza mafuta kikaonekana kidogo kwa hiyo serikali ikakosa mapato. Kwa hiyo, kama kifaa hiki hakipo basi niombe shirika au wizara inayohusika kuweza kuhakikisha kwamba kifaa hiki kinapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie mchango wangu katika Uwanja wa Michezo wa Mao Tse Tung. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze wizara inayohusika, lakini nimpongeze Mhe. Rais kwa kuweza kulitizama suala zima la miundombinu ya viwanja vya michezo katika nchi yetu. Nimpongeze vile vile Mhe. Waziri na

watendaji wake katika kusimamia vyema Sekta hii ya Michezo na hususan hivi sasa ambapo serikali ina miradi mbali mbali ya viwanja vya michezo katika mawilaya. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, suala la Uwanja wa Mao Tse Tung kwamba katika michoro yake hakuna eneo la *parking* ya magari. Mimi nafikiri tunarudi katika mwaka 49, hivi sasa tupo mwaka 2018, kama tunavyoelewa hivi sasa nchi yetu ina magari mengi na maeneo ya *parking* yamekuwa finyu. Nitoe mfano mmoja katika benki pale ya Mpirani pana *parking* ambayo sio rasmi kwa sababu *parking* ile ipo barabarani. Sasa kama tunataka uwanja wetu uwe unapata wateja, unapata watazamaji basi suala la *parking* ya magari lilikuwa lina umuhimu wake na hili lilikuwa litazamwe toka katika michoro yake. Inawezekana tukawa na viwanja vizuri lakini tukawa na kasoro hiyo kwamba wale ambao wanataka kuingia katika uwanja na tayari wana vyombo vyao vya usafiri wakawa wanakosa eneo maalum.

Kwa hiyo, maoni na ushauri wa kamati naupongeza sana kwa sababu kamati vile vile imetoa ushauri mzuri mbali mbali katika kuangalia fursa za kibiashara na kiuchumi kwa kutumia uwanja ule. Kwa hiyo, ni vyema taasisi inayohusika kuweza kuzitazama au kutazama ushauri ule wa kamati ambao unaweza ukasaidia hata katika kukuza sekta nyengine za kibiashara kwa kuutumia uwanja na viwanja vyengine ambavyo vinajengwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya michango hiyo na mimi niungane na wenzangu katika kuunga mkono ripoti hii na niwapongeze sana wanakamati wakiongozwa na Mhe. Mohamed Said Mohamed kwa maelezo na ufafanuzi wao wa kina. Niwaombe tu wenzangu na wao waichangie ripoti hii na tuiunge mkono kwa maendeleo ya nchi. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi ambayo ni hotuba muhimu sana lakini wenzangu waliotangulia maeneo mengi ambayo nilikuwa niyazungumze tayari wameyazungumza. Kwa hiyo, mimi nitaboresha tu kidogo kidogo nitakazia kazia. Maeneo mengi Mhe. Hamza Hassan Juma ameyazungumza, Mhe. Rashid Makame Shamsi kanimaliza kwenye mafuta, Mhe. Hamza Hassan Juma kayazungumza na Mhe. Rashid Makame Shamsi kazungunza kwenye karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba pamoja na changamoto zilizoelezwa, baadhi ya changamoto zilizoelezwa muelekeo wa ukuaji wa uchumi wa nchi yetu ni mkubwa sana na ni mzuri sana. Kwa hiyo, nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa dhati kabisa kwa usimamizi wake bora na utekelezaji wa majukumu ya nchi hii.

Mimi naamini Rais anajua kwamba yeye ana jukumu na anatekeleza lile jukumu ambalo amelikubali na ndio maana mpaka leo tunajisifu kwamba tumepiga hatua ya maendeleo hasa kwenye mpango huu wa bajeti zetu za serikali. Mimi nakumbuka tulipoingia hapa Barazani mwaka 2015 tulikuwa na karibu bilioni mia tano sabini bajeti yetu. Lakini hadi kufikia leo inakaribia trilioni moja nukta moja ni *indication* kubwa na nzuri. Kwa hiyo, ni kitu cha kujipongeza.

Lakini pamoja na hayo nachukua fursa hii kuupongeza uongozi mzima wa Baraza ukiongozwa na Balozi Mhe. Seif Ali Iddi, Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa usimamizi wake wa mawaziri kwa serikali hii. Mimi naamini ndio uliosababisha mpaka leo tukawa tunajigamba hapa, vyenginevyo ingekuwa

hatuyazungumzi haya maendeleo na mambo mengine tuliyokuwa tunayazungumza. Mhe. Mwenyekiti, huo ndio ukweli ulivyo.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo, napenda kuzungumzia baadhi ya mambo ambayo nimeyaona kama ni changamoto ili twende na kasi iliopo na tuweze kufikia leo tulilolikusudia ni vyema hizi changamoto ambazo zimezungumzwa tukaweza kuzipatia ufumbuzi. Mfano mimi naanza ukurasa wa 39 narudi nyuma, naanza kuizungumzia *ZURA.*

Mhe. Mwenyekiti, *ZURA* wana jukumu kubwa kutoa huduma kwa wananchi hasa kwa nishati ya mafuta na gesi. Leo tusiizungumze gesi tuzungumze mafuta ambayo tuko nayo. Leo ni wiki inaendelea mafuta hakuna, unakwenda kituoni unakuta kuna foleni iliyokuwa haisemeki, foleni kubwa sana. Mimi nimepiga foleni kutoka saa 5:00 hadi 7:00 ndio nimepata mafuta naambiwa nitapewa ya sh. 20,000/=. Tunakwenda wapi. Nchi tunayoitegemea twende kwa kasi na uchumi mkubwa kama nilivyoieleza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana na ushauri wa Mwenyekiti, Mhe. Hamza Hassan Juma, kwamba sasa iko haja ya kuweka miundombinu iliyo sahihi ambayo tutaharakisha kuleta maendeleo. Tukiwaza kumiliki lile eneo la Mangapwani tukalifanyia *plan* tukawapa wawekezaji wakaweza kuwekeza mimi nafikiri kwa asilimia kubwa sana tatizo la mafuta nchini kwetu halitakuwepo. Cha kusikitisha ni kwamba *ZURA* wapo Idara ya Ardhi, Idara ya Upimaji ni Idara ya Ardhi. Lakini inasemekana kutoka mwaka 1995 serikali ilipolitenga eneo lile kwa ajili ya uwekezaji mpaka leo halijapimwa miaka 23 sasa. Sijui hata tuseme nini. Maana yake ikiwa miaka 23 serikali imetenga eneo kwa ajili ya kuwekeza kitu fulani lakini mpaka leo halijapimwa likajulikana eneo hilo sijui tunafanya nini.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri akae na watendaji wake kwa sababu *ZURA* ipo na wizara yake na watu wa upimaji wapo anao katika wizara yake, waharakishe kulipima eneo lile lijulikane ili waweze kupanga mpango bora wa matumizi ya eneo lile, ili lile lengo lililokusudiwa lifikiwe, vyenginevyo tutakuwa kila siku sisi tunasema *ZURA* wee! *ZURA*. Niwaombe sana na nashauri jambo likishakusemwa sana ni vyema likatekelezwa isiwe tunalizungumza kila siku jambo hili litakuwa halipendezi. (*Makofi*)

Lakini si hilo tu tatizo la ukosefu wa mafuta kumesababisha foleni ambayo watu hawalipi kodi, kodi za serikali hazilipwi. Mwenzangu pale kazungumzia *flow meter,* hivi tutaweza kujuaje idadi ya mafuta yanayoingizwa ikiwa hakuna *flow meter* ambayo itakuwa inasoma kiwango halisi cha mafuta yaliyoingizwa nchini. Mimi sina hakika, ikiwa ni kweli naiomba sana serikali iharakishe kile kifaa kiletwe pale ili kiweze kufanya kazi. Kufanyakazi kwa kifaa kile ndio kitakachotoa muongozo wa kiwango halisi kinachohitajika kulipwa kwa ajili ya biashara ya mafuta yanayoingizwa nchini. Vyenginevyo kama alivyosema Mhe. Rashid Makame Shamsi kwamba kuna wajanja wataitumia nafasi hiyo waweze kudanganya kiwango halisi cha uingizaji wa mafuta na baadae wasilipe kodi na ile haki ya wananchi pia waichukue. (*Makofi*)

Niiombe sana wizara inayohusika naamini kwamba jambo hili lifanyiwe haraka kuletwa ili tuondokane na hiyo kadhia. Sambamba na uagizaji wa mafuta wakati tunasubiri huo ujenzi suala hili sasa limekuwa ni tatizo kila wakati mafuta yanakatika. Tuwaombe sana na naomba sana serikali kwamba kuliangalia jambo hili, hili ni tatizo.

Juzi au sijui ilikuwa jana waziri alitoa takwimu kwamba tunayo akiba fulani ya mafuta hapa. Lakini pamoja na maelezo aliyoyatoa

leo mafuta hakuna hayaonekani kabisa, pamoja na takwimu tuliyopewa jana kwamba *BP* wana kiasi fulani, *GAPCO* wana kiasi fulani cha akiba, lakini mafuta hakuna. Tuzungumzeni kwamba mafuta ni tatizo linalohitaji kupatiwa ufumbuzi wa kudumu. *(Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nirudi ukurasa wa 25 ambao tunazungumza suala la mashine za kusafishia karafuu. Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyojua kwamba karafuu ni uti wa mgongo wa taifa letu na ni moja katika biashara tunazozitegemea kutuingizia fedha za kigeni. Kwa hiyo, sasa hivi kweli wenzetu wana tatizo ulimwenguni mashine na bidhaa zao zote wanataka ziende vizuri. Ikiwa mashine tuliyonayo ya kusafishia karafuu ni ya miaka ya nyuma na serikali kupitia shirika letu la *ZSTC* linanunua karafuu kwa wingi. Niombe sana kwenye msimu utakaofuata wajitahidi *at least* zile mashine au ile mashine japo moja ya kisasa tuwe tumeshakuwa nayo kwa ajili ya kutengeneza biashara yetu kusafisha karafuu ziwe kwenye kiwango bora ambayo karafuu yetu kwa sasa hivi ina jina zuri. Tukiweza kupata mashine nzuri ya kisasa ambayo itaweza kusafisha karafuu zetu vizuri itaongeza sifa ya karafuu yetu na ninaamini kwamba ongezeko la matumizi na wateja kwa karafuu watapatikana wataongezeka.

Lakini pia mwenzangu Mhe. Rashid Makame Shamsi alizungumza suala zima la ukopeshaji wa fedha. Suala la ukopeshaji wa fedha kwa wakulima wa karafuu mara nyingi nimekuwa nikilizungumza mimi kwamba *ZSTC* walipaswa wawakopeshe wakulima wasiwakopeshe wanaokodi karafuu. Mtu anapoamua kukodi karafuu tayari ameshajipanga. Ni vyema na ni busara zaidi kwamba sisi tuna lengo la kuongeza uzalishaji kwa hiyo tuelekeze nguvu zetu zaidi kwa wakulima wale wenye mashamba kulikoni kuelekeza nguvu zetu kwa watu wanaokodi karafuu. Nasema hivi kwa sababu gani wenye mashamba

hawaondoki, lakini leo wenye kukodi mashamba ya mikarafuu baada ya kumaliza msimu wa karafuu wanaondoka na hii ndio sababu wanasema kwamba tumenunua karafuu za bilioni mia moja na kumi na mbili lakini pesa hazionekani katika mabenki yetu. (*Makofi*)

Huwezi kuziona fedha zile kwa sababu wanaokodi karafuu baada ya kumaliza wanachukua pesa zao wanaondoka. Hili nilimwambia Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwamba angalia watu wanaokodi karafuu, sio watu wa hapa angalieni, na leo nasema kwamba kama tunataka tuweze kudhibiti fedha hizi kwa wakulima wa karafuu utaratibu mzima ni bora watu walipe kwa kupitia benki. Watu wote wafungue akaunti zao benki na *ZSTC* walipe kupitia benki, mtu akachukue fedha zao, *transaction* itaonesha nani kachukua fedha, nani yupo, kwa sababu akaunti inatoa maelezo yote ya mtu yuko wapi, kazi anayofanya na kila kitu. Kwa hiyo, sisi ni rahisi kwetu kuweza kufahamu. Vyenginevyo itakuwa kila siku tunawapa watu baadae wanaondoka wengine hawatulipi matokeo yake ndio kama hayo. (*Makofi*)

Leo tumeambiwa karafuu zilizokodishwa karibu za bilioni mbili watu wana madeni hawajamaliza kulipa serikalini. Kwa nini hawajamaliza kulipa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika mbili.

Mhe. Omar Seif Abeid: Aaaa! Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo nimalizie hili.

Mhe. Mwenyekiti, wito wangu katika kukodisha karafuu serikali izingatie itoe kipaumbele kwanza kwa wenye mashamba kuwapa fedha za kuendeleza kilimo na wakati wa kukodisha waangalie watu wanaoishi katika maeneo husika.

Mwisho tuitumie benki yetu kwa sababu fedha zile zikirudi benki, benki ile kwanza watapata faida, ikisha pili na mwananchi yule atakuwa na uhakika na serikali yenyewe wizara itajua nani wa ku-*deal* nae. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mhe.Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Omar Seif Abeid, sasa anayefuata ni Mhe. Suleiman Makame Ali akifuatiwa na Mhe. Simai Mohammed Said.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi ya kuweza kuchangia ripoti hii ya kamati inayohusu masuala ya bajeti. Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabla ya kuchangia niwapongeze sana wajumbe wa kamati hii kwa kazi ngumu lakini inaonesha umahiri wao. Nimpongeze sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii kaka yangu Mhe. Mohammed Said Mohammed kwa uzoefu mzuri alionao na kuhakikisha kwamba kila kitu hapa ametuwekea wazi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukrani zangu hizo niende katika ukurasa wa 10. Mhe. Mwenyekiti, hapa kwa ruhusa yako nimpongeze sasa Mhe. Waziri wa Fedha kwa kusimamia mapato kuhakikisha kwamba ndani ya Oktoba hadi Disemba imefikia mpaka asilimia 93 ni jambo la kutolewa mfano kusema la ukweli. Lakini kwa yeyote yule anayebeza juhudi za Mhe. Waziri basi huyo itabidi apungwe ama azinguliwe.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anajitahidi sana mtu kweli yake anapewa. Kila siku Mhe. Jaku Hashim Ayoub anasema hapa kwamba mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Kwa hivyo, kilichobakia ni sisi kumuunga mkono ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inapata mapato na kupata maendeleo zaidi. Ama kweli hakika Dkt. Khalid Salum Mohammed anaweza.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende moja kwa moja kwenye masuala ya miradi. Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi kunakuwa na miradi ya kimaendeleo, miradi hii inapokuja kama ujenzi wa skuli, ujenzi wa barabara na mambo mengine huwa zinatengenezwa hizi tenda na kampuni kuomba. Mhe. Mwenyekiti, hubahatika kampuni za ndani na kampuni za nje zinazoshinda tenda zile. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nashauri sana kwamba wale wanaoshinda katika masuala yale ya tenda wanapokuja waje na vifaa vyao kwa sababu serikali siku nyengine inapata faida siku nyingine inapata hasara, mara nyingi inapata hasara.

Tunaona kwamba gari za serikali zinatumika kwenye kampuni. Mhe. Mwenyekiti, baadhi ya vile vifaa vinapotumika kwenye kampuni wanatumia wakiondoka hapa vifaa vyengine vinakuwa vibovu havifai. Kwa hivyo, siku nyengine kampuni nyengine zikija hapa zinakuja na vifaa huenda vifaa vyengine wakatuachia hapa hapa tukaendelea kuvitumia. Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, niombe sana kuhakikisha kwamba na suala hili nalo limeangaliwa.

Mhe. Mwnenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye Shirika la Biashara kwenye suala la kukusanya mapato. Mhe. Mwenyekiti, Pemba kuna wafanyabiashara wengi lakini hivi sasa wafanyabiashara wale kuna wengine wanakata tamaa kwa sababu wao wanachukua mizigo yao wanapitia Mombasa, Mombasa kule hakuna kulipia *TRA* au jambo jengine. Kama vile *TRA* mfano sijui wenyewe wanaitaje kule Kenya wanalipia *wharfage* tu pale bandarini wanauchukua mzigo wanauleta Mkoani ama Wesha. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hapa sasa hivi kumetokea tatizo kidogo wafanyabiashara wale ambao wanachukua mzigo wakauleta hapa Unguja halafu wakasafirisha Pemba gharama inakuwa kubwa.

Kwa hivyo, inakwenda wafanyabiashara wengine wakate tamaa na waache kufanya biashara na kukosesha mapato serikali.

Mhe. Mwenyekiti, unapoacha kufanya biashara na mapato yanakosekana. Kwa hivyo, niombe sana kwenye masuala haya ya biashara wahakikishe kwamba masuala ya karafuu, pia nayo Mhe. Omar seif Abeid amesema hapa kwamba mapato hapa tuliona yamevuja kidogo watu wamekopesha pesa za karafuu zile hawakurejesha ni mtihani. Ni mapato tumeyategemea kwa sababu pesa zile bilioni moja zingelipatikana sasa hivi zingelifanyiwa mengi ndani ya majimbo yetu na ndani ya mikoa na wilaya.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende moja kwa moja kwenye ukurasa wa 26 kuhusu suala la uvamizi wa shamba la wananchi katika maeneo ya Mtakata. Mhe. Mwenyekiti, wamesema katika hekta hizi hapa 230, lakini kuna maeneo mengine yamevamiwa na wananchi. Mhe. Mwenyekiti, hapo Mtakata penyewe ukipita unakuta mchaichai huku barabara shamba lote limekuwa pori sasa, wakati shamba lile haliendelezwi ni kweli wananchi watavamia watalima mihogo, mipunga na mambo mengine. Kwa hivyo, ulikuwa ushauri wangu kwa shirika hili kuhakikisha kwamba wale wananchi wanaolima pale wawape ushauri na wawape taaluma ya kulima hiyo miti wanayoihitaji ili kile kiwanda kiweze kuendelea.

Kwa sababu kama itakuwa hawana taaluma wanayowapa lakini pia na lile shamba wakaliacha likawa mwitu mwisho wake watakuwepo majambazi watajificha kwenye msitu ule itakuwa faida haipatikani. Lakini kama shamba lile wale wanaolima mle wakifahamisha kwamba hapa tunataka mlime lakini mlime mti huu na huu ili kwamba kile kiwanda kiweze kuendelea faida itapatikana. Kwa hivyo, mimi naomba sana sasa kuhusu suala hili la shamba lile la Mtakata wale wanaolima basi wapewe taaluma

ya ile miti inayotakiwa, la kama si hivyo wananchi wataendelea kulima muhogo wapate vijio wakila na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye ukurasa wa 29 kuhusu suala la mradi wa ujenzi wa Skuli ya Sekondari Madungu. Mhe. Mwenyekiti, sisi hapa tunapitisha bajeti na bajeti ndio roho ya serikali, bila ya bajeti hakuna kinachokwenda kwa sababu bajeti ni pesa. Mhe. Mwenyekiti, tunapopitisha bajeti pesa zinapopatikana zitumike zilivyo sio kufanya ubabaifu.

Mhe. Mwenyekiti, imani yetu sote inatupa kwamba Skuli ile ya Madungu na skuli nyengine zinazojengwa zidumu miaka 50 na kuendelea mbele. Leo kuna nyumba hapa zimejengwa tangu ukoloni ambapo babu zetu walikuwa hawajazaliwa nyumba zile zipo, leo nyumba mpya au linajengwa jengo jipya kesho unalikuta limeshachanika lote. Mhe. Mwenyekiti, hapo ufanisi haupatikani itakuwa sisi tunaimba nyimbo lakini kuimba nyimbo hiyo tunacheza wenyewe. Mhe. Mwenyekiti, kwanza naishauri sana sana serikali kuhakikisha kwamba tunasimamia vizuri kwenye miradi hii ya maendeleo ili kuhakikisha yale tunayoyajenga yawe ya kudumu sio kama kila siku turudie kujenga tena skuli hiyo hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika jimbo langu wanafunzi Skuli ya Ndagoni sasa hivi mabanda ni mabovu, ukienda Michungwani mabanda ni mabovu, leo inarudiwa tena skuli ile ile ya Madungu inajengwa tena. Sasa Mhe. Mwenyekiti, itakuwa tunajengewa skuli hiyo hiyo moja mpaka itafika kiama. Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana serikali kwenye masuala haya kuhakikishwa kwamba mambo haya kimaendeleo yasimamiwe vizuri na yajengwe, yakijengwa yawe madhubuti, ikiwa barabara, ikiwa hayo majengo chochote cha kimaendeleo kinachokuwa ni cha kujenga basi kiwe madhubuti na kisimamiwe. Kwa sababu zile ni pesa za wananachi, ikiwa ni pesa ya mkopo inalipwa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Abdalla Ali Kombo nilimsikia akisema hapa kwamba ninalipa mimi na wewe na mwananchi wa kawaida. Mwananchi wa kawaida analipa vipi yeye hajui, lakini analipa akienda akinunua umeme anakatwa *VAT*, akilipia maji analipa. Kwa hivyo, naomba sana ili kuzitunza hizi pesa za wananchi ni kuwaletea maendeleo wananchi, lakini tukisema kama kila mtu atie mfukoni mwake itakuwa hatufiki.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye suala la changamoto za bandari ya Mpigaduri. Mhe. Hamza Hassan Juma alisema na mimi naunga mkono suala hili ni jambo zuri sana kujenga bandari pale Mpigaduri. Lakini Mhe. Mwenyekiti, angalia ikikaa gari moja ya fusi kule Bububu skuli foleni inafika Darajani, leo inajengwa bandari Mpigaduri itabidi sasa ile barabara ya kwendea Bububu iwe haitumiki isipokuwa itumike magari yale ya makontena itakuwa ni usumbufu. Kwa hivyo, mimi naiomba sana na njia nyengine mbadala sijui kama itakuwepo ya kuweza kupita wananchi itabidi sasa azunguke apite huko aweze kwenda jimboni kwa Mhe. Miraji Khamis Mussa, Chumbuni. Kwa hivyo, naomba sana kuhakikisha kwamba bandari ya Mpigaduri nayo pia ingefikiriwa ikatafuta kama kuna eneo jengine mbadala ikawekwa kulikoni pale itakuwa ni usumbufu. Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono ripoti hii asilimia mia kwa mia.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Suleiman Makame Ali, sasa anayefuata ni Mhe. Simai Mohammed Said, akifuatiwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub na baadae Waziri wa Fedha nae ajitayarishe.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nianze kuchukua nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Lakini pia nichukue nafasi hii pia kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu kuhusiana na ripoti hii

ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi na mimi pia niseme kwamba ni mjumbe wa kamati hii pia.

Lakini pia nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mwenyekiti wetu Mhe. Mohammed Said Mohammed, Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae kwa uongozi wake juu ya kamati yetu na kazi nzuri aliyoifanya. Lakini pia kwa mashirikiano ambayo amekuwa akiyaendeleza yeye pamoja na Mhe. Waziri wa Fedha ambao sisi kama kamati tumefaidika sana katika kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika changamoto moja ambayo tumeipata katika kamati yetu ni watendaji wengi serikalini kutokuwa na ufahamu juu ya kamati yetu. Sasa ukisoma katika ripoti yetu ukurasa wa kwanza inasema:

"Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi inaundwa kwa lengo la kuliwezesha Baraza la Wawakilishi kupata fursa pana zaidi ya kuchambua, kushauri na kufuatilia kwa kina mchakato mzima wa bajeti ya serikali na hatimae kuishauri serikali ipasavyo".

Kimsingi kabla ya kuanzishwa Kamati hii ya Bajeti majukumu ya kamati hii yalikuwa yakitekelezwa na Kamati ya Wenyeviti wa Kamati ya Kudumu ya Baraza. Sasa nimekusikia Mhe. Mwenyekiti, leo ukizungumza kukosekana kwa watendaji wengi wa serikali kutokuwepo pale juu, hii inaonesha hata hao pia watendaji bado hawajawapa uelewa wa kutosha kufahamu hasa kamati yetu inafanya kazi gani. Mimi ningeshauri mawaziri husika ni vizuri wakatafuta njia nzuri pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi au watendaji wetu ili kuleta umoja mzuri na wapate kuelewa yale ambayo wajumbe wa hapa wanachangia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakwenda kwenye mchango wangu kwa haraka kutokana na muda ambao umenigaia. Nataka

nizungumze suala la uchimbaji wa mafuta na gesi. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilipata bahati pamoja na wajumbe wenzetu 11 mwaka 2016 baadhi ya Kamati ya Baraza hili tulifanyiwa semina na Bw. Yona Kilagani aliyekuwa Mkurugenzi Mstaafu wa *TPDC*.

Katika wajumbe ambao walishiriki walikuwa ni Mhe. Abdalla Ali Kombo, Mhe. Abdalla Maulid Diwani, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Hassan Khamis Hafidh na Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ambaye alikuwa ni Naibu Waziri pekee wa serikalini aliyekuja. Nafikiri wajumbe wengine wawili watatu walikuwemo nimeyasahau majina yao nikiyakumbuka nitayataja. Lakini moja katika jambo ambalo Dkt. Yona alijaribu kutufahamisha ni kujenga uelewa mzuri wa hii Sekta ya Mafuta na Gesi hasa ikoje, lakini kupata kufahamu hasa juu ya haya ma-*block* tuliyokuwa nayo kutoka 9 hadi 12.

Leo katika historia ya mafuta na gesi alitupeleka kutoka mwaka 1958 mpaka akatufikisha mwaka 2015 baada ya ile sheria kupitishwa ya mafuta na gesi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa moja ambalo sasa lililofanyika jipya ni kwamba Zanzibar tunapitisha sheria yetu na sasa hivi tupo katika harakati za kujipanga kwenda kuanza katika mchakato mzima wa kuanza kuchimba. Lakini katika sehemu moja kuu lazima wananchi na Wajumbe wa Baraza hili tufahamu vizuri, huwezi kuanza kuchimba mafuta au kuanza mpango wowote mkubwa kusaka mafuta na gesi ikiwa huna taarifa za mtetemo. Hivi sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar baada ya ile sheria kuipitisha na tuwapongeze sana wameanza harakati wameunda taasisi zote zinazohusika ili kuweza kusimamia mchakato huu.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia tuna pembe tatu, kuna *SMZ*, kuna hawa *BCG* ambao wao wanasimamia hiyo kazi, na kuna hawa Ras al Khaimah *(RAK)* ambao wanashirikiana na hawa *BCG* ili kupata

hizi taarifa za uhakika. Muda wake nafikiri unaweza kuchukua mwaka mmoja au miwili. Ninachoomba hapa sana nataka nikikazie kitu kimoja taarifa za mtetemo *ownership* yake ibakie ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa sababu mali yote, mambo yote yatakayoweza kupatikana katika yale ndio uchumi ambao Zanzibar unaotegemea katika vizazi vijavyo.

Kwa hivyo, Ras al Khaimah pamoja na *BCG* watakapomaliza mchakato wote wa kutafuta mpango mkuu katika maeneo yote ya uchimbaji wa mafuta na gesi pamoja na kuzipata hizi taarifa za mtetemo, basi tupate zile data ambazo ni *original* ya kila eneo kutoka Mashariki ya Pemba kule Kaskazini mpaka tunamaliza Kusini katika maji ambayo yametajwa katika Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, hili ninalolisema lina umuhimu wake, kuna mifano mingi ya nchi ambayo hizi taarifa za mtetemo palitokea migogoro tofauti. Kwa hivyo, *SMZ* pamoja na mawaziri wote kwa pamoja na watendaji wetu wajiendeleze kujipatia elimu na kufahamu katika Sekta hii ya Mafuta na Gesi ambayo ni ngeni kabisa. Leo tulikuwa tupo nyuma sote, miaka miwili nyuma wapo wametangulia mbele hawawezi hata siku moja wakawa mabingwa katika sekta hii. Tuendelee kujifundisha sote ili na sisi Wajumbe wa Baraza tuweze kuishauri Serikali. Naamini Mhe. Waziri wa Fedha na Mwanasheria Mkuu wamenifahamu vizuri kwa sababu wao ni watu wenye uelewa na wanafahamu umuhimu katika suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu nyengine nataka nizungumze *finance bill*. *Finance bill* ya mwaka 2016/2017 ilituumiza sana sisi watu wa Zanzibar hasa kwa wafanyabiashara. Leo tumeona kila mfanyabiashara anapotoka Tanzania Bara kuja Zanzibar wanalipishwa asilimia 18 imekuwa mara mbili, Bara watalipa waende kule viwandani kununua bidhaa, ukinunua *generator*

Tanzania Bara utalipa asilimia 18 *VAT,* ukileta Zanzibar *ZRB* wanakusubiri.

Mimi naomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa kushirikiana na watendaji wake hasa Katibu Mkuu, washirikiane na Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuelekea bajeti 2018/2019. Tuhakikishe yale yote yatakayokuwemo katika *finance bill* ya mwaka huu yaende sambamba yasije yakazorota na kuturudisha nyuma na wananchi wetu wakapata hali ngumu katika kufanya shughuli zao za kila siku, tukijua kwamba Wazanzibari wengi ni wafanyabiashara. Hadi leo tukitoka tukienda madukani Mlandege, Darajani, maeneo yote wananchi wanalalamika juu ya matozo ya kuchajiwa asilimia 18 Bara na Zanzibar ambayo mambo haya zamani hayakuwepo. Hasa katika *tax returns* wanazozifanya mwisho wa mwezi kuzipeleka pale *ZRB,* wakati zamani walikuwa wana-*enjoy facility* kwamba ukinunua bidhaa Tanzania Bara una risiti yako ya *VAT* mwisho wa mwezi ukipeleka katika *input* na *output tax* yako pale *ZRB* wanaipokea ile risiti yako wanaitambua, na Kamishna wa *ZRB* anampelekea Kamishna wa *TRA* na fedha zile zinarudishwa tena Zanzibar. Sasa mimi naomba jambo hili waliangalie sana.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni *issue* ya Micheweni Pemba. Mheshimiwa ukienda katika miradi mikuu ambayo wakati Fumba ilipokuwa inatayarishwa, ilipangwa mwanzo nafikiri ilikuwa iwe *Economic Free Zone,* lakini zaidi ilitegemea kujengwa katika masuala ya viwanda. Nampongeza sana Mhe. Rais kwa kumualika hasa pia kwa kumjali Mhe. Said Bakhresa na leo tunaona mradi mkubwa umefanyika Fumba.

Naomba nguvu zile zile ambazo zimetumika kwa upande wa kisiwa cha Pemba hasa katika eneo la Micheweni, tutafute kila njia tuweze kufungua miradi ya *assembling plans,* ili miradi hii

tuweze ku-*create* ajira kwa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba, lakini bidhaa zile pia ziweze kuletwa Unguja. Pia nashauri serikali tuangalie katika hali nzima ya lishe ya Wazanzibari kwa ujumla ni mboga mboga aina gani ambazo tunaweza tukapanda Pemba zikaja zikauzwa katika *market* ya Tanga pamoja na Unguja ili wananchi wetu waweze kufaidika.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nataka nizungumze Ofisi yetu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo ipo Dar es Salaam. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia Ofisi ya *SMZ* iliyopo Dar es Salaam ni kiunganishi kikubwa sana sio baina ya *SMZ* na *SMT*, lakini *SMZ* na dunia na mabalozi wote waliokuwemo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ukiangalia hali ya jengo letu, hali ya ile ofisi, hata mtu haijui ile ofisi pale inasimamia kitu gani. Lazima tujenge mazingira ya kwamba hata watu ambao wawekezaji wanapotaka kuja Tanzania, wanaishia Tanzania Bara wasiishie Serena Dar es Salaam, wasiishie Hyatt Dar es Salaam, waweze kwenda katika Ofisi ya Zanzibar ili kupata kujua miradi, biashara, fursa zilizokuwepo hapa Zanzibar za kiuchumi.

Ninasema hivi kwa sababu kesho kutwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wengi watendaji wao watahamia Dodoma, watakapokuwepo Dodoma watazidi kuwa mbali na sisi kwa upande wa Zanzibar, hivi vikao vitakuwa vinafanyika vipi vya pamoja. Mimi nashauri tuweze kuimarisha ofisi yetu Dar es Salaam ili kujenga ukaribu mkubwa wa dira kuu ya nchi ambayo inayosimamia ndani ya Mawaziri ambao wanamsaidia Rais wetu pamoja na Makamo wa Pili na watendaji.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kunipa nafasi hii nikushukuru sana sitaki kupoteza muda mwingi najua watu wengi wamechangia ripoti hii, mimi naunga mkono ripoti hii kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu mia juu ya mia. Nakushukuru sana

Mwenyekiti, nawapongeza Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, nawashukuru kwa kunisikiliza. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Simai Mohammed Said, sasa namwita Mhe. Jaku Hashim Ayoub na baadae Mhe. Waziri wa Fedha ajitayarishe kwa kumalizia ni mchangiaji wetu wa mwisho.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitakuwa mtovu wa adabu wa mwisho kama sikukushukuru wewe kwa umakini wako uliloonesha hii leo kwa kuliona suala la watendaji kutokuwepo juu nikupongeze kwa dhati kabisa. Inaonekana kila siku zikiendelea mbele hichi kiti kitakuwa hakiyumbi Mhe. Mwenyekiti, umeonesha umakini wa hali ya juu baada ya kuona watendaji hawapo. Siku zote nikisema mimi naonekana kama ni mbaya, kwa hivyo nikupongeze kwa dhati. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunachangia kitabu cha bajeti karibu wizara zote zimeguswa. Tumtafute Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko yuko wapi hapa, Kaimu wake yuko wapi hapa, Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, tunafanya nini, tunatwanga maji kwenye kinu, *serious* iko wapi. Tumekaa hapa wananchi wametutuma tueleze matatizo yao, tunaongozwa na Kanuni na Katiba ya Zanzibar. Sasa nisije nikafika pahala nikaja nikateleza. *(Makofi)*

Narudia tena tusije tukafika pahala tukateleza. Lakini Wizara nyeti ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira leo *issue* kubwa nchi hii mafuta. Mhe. Mwenyekiti, mimi ndio kwanza nafika hivi sasa jioni sitaki kusema nikataka kujisifu lakini najua ninakotokea kwenye suala la mafuta. Kama mtamuuliza Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira watakuambieni nilikuwepo wapi mimi kuhusu mafuta Zanzibar, sitaki kuzungumza mengi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimeondoka kwa gharama zangu mwenyewe asubuhi, lakini sitaki kusema tena mkono wa kulia ukatoa wa kushoto ukapata habari hapana sitaki kufika huko Mwenyezi Mungu anajua nia yangu. Lakini ukiwauliza hawa watakuambia leo tuna changamoto gani. Meli moja imeondoka hivi mchana *United Spirit* ya petroli. Pana mvutano ilikuwa kwa kutaka kuingiza Meli ya Ukombozi ambayo inapakia tani 3,000. Kwa ubishi mkubwa na mvutano wa hali ya juu sitaki kuzungumza mengi. Leo Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira yuko wapi, Naibu wake yuko wapi. Ndio yale ninayosema Mhe. Mwenyekiti, tunatwanga maji kwenye kinu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mafuta ni nguzo muhimu ya kila kitu, watoto wanataka kwenda skuli, kuna wazazi wanataka kuzaa kupelekwa hospitali, utalii. Gari sasa hivi ukienda *Airport* mtihani, kutoka hoteli kwenda *Airport* na kutoka *Airport* kwenda hoteli, huu utalii tunaouhitaji kwa kupata mapato, tunakuza mapato au tunarudi nyuma.

Mhe. Hamza Hassan Juma nikuombe sana wewe ni Mwenyekiti makini, suala la meli kutokufika pale Mtoni tani 3,000 ni kina kidogo. Sasa serikali iwe *serious* kuelekea Mangapwani. Mhe. Mwenyekiti, nikuombe sana, vyenginevyo tunajitakia wenyewe meli ingekuja moja kwa moja tusingepata shida hii, tuwe wakweli. Tufanye haraka njia ya Mangapwani tena mafuta Dar es Salaam ni rahisi kuliko Zanzibar kutokana na kodi zilivyokuwa kubwa, na maswali kutoka Bungeni ninayo sio kazi nyepesi, inakuwa ni mbuzi wa kafara wakati mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nije kwenye *ZIPA*. Uwekezaji *ZIPA* kuna matatizo makubwa sana. Kuna kitengo cha Kamisheni ya Ardhi, *ZIPA* walipokuwa wakijitegemea wenyewe ilikuwa hakuna mtihani huo, vibali vilikuwa vikitoka hata Ilani ya Chama

cha Mapinduzi kuna miradi mingi imefanyika. Ndio nikasema Mhe. Waziri Salama Aboud Talib hayupo hapa na Naibu wake pia hayupo. Kitengo cha Kamisheni kuna mitihani, kuna vibali vya wawekezaji zaidi ya vinane au tisa, kibali hakijapatikana karibu mwaka mzima, tunakwenda mbele au tunarudi nyuma.

Mhe. Mohammed Said Mohammed nikushukuru sana kwa umakini wako kwa kuiongoza kamati na umeiona hii changamoto kubwa sana iliyokuwepo pale. Hatuwezi kwenda, vibali vingetolewa tungepata ajira na serikali ingepata mapato. Vibali zaidi ya vinane au saba, nimezungumza mara ya pili hii na zimo katika ripoti karibu mbili. Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ripoti hiyo imo na Mhe. Dimwa kaliona hilo, vibali vimekaa tu pale hakuna kinachoendelea. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, *One Stop Centre* ni muhimu Mhe. Mohammed Said Mohammed nikupongeze, ni muhimu sana. Leo tunataka kuuza wawekezaji wanashindwa, miradi mingine inataka kuondoka. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye *Terminal II Airport*, huu ni mtihani mradi huu sasa unataka kulipwa pesa, pesa hazipatikani ziko wapi, mradi huu una miaka mingapi. Leo wenzetu Dar es Salaam wamejenga juzi Uwanja wa Ndege leo unamalizika, juzi tu kabla ya sisi, *serious* iko wapi, tuwe wakweli. Kule sasa ukienda sijui kama utakosa nyoka na mabuku kwenye *Terminal II*, pesa zinataka kulipwa sasa hivi, sijui aliyepewa kampuni ya mwanzo yuko wapi, sasa nafikiri atapewa kampuni nyengine ya pili. *Terminal II* kuna mitihani mikubwa, katika uwanja ghali duniani nafikiri ndio unaongoza wa *Terminal II* wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, *ZIPA* inastahiki pongezi, lakini kwa kuunda hivi tunavyokwenda pana mtihani.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Hospitali ya Abdalla Mzee, kuna changamoto hapa zimejitokeza nakubaliana na Mhe. Mohammed Said Mohammed hasa ya wafanyakazi Pemba kunahitajika hatua za dharura serikali kuajiri madaktari Pemba. Lakini kila kukicha changamoto iko kwenye Hospitali ya Abdalla Mzee, Hospitali yetu kubwa ya Mnazi Mmoja kuna changamoto kubwa, na Mhe. Waziri wa Afya simuoni hapa na yeye. Tunazisema hizi wizara, tunacheka wenyewe na tunasema wenyewe lakini watendaji hawapo, huo ndio ukweli.

Mhe. Mwenyekiti, katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kuna changamoto moja kubwa sana ya *lift* huu ni mwaka mzima sasa hivi. Sisi tushukuru angalau tuna kadi zetu tunakwenda hospitali yoyote, lakini kuna wavuvi na wakulima kule ndio wanaoumia. Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Mohammed Said Mohammed atafute njia katika bajeti inayokuja pesa zitengwe. Sisi tuna kadi zetu angalau tunakwenda hospitali yoyote, tunakwenda *Global* au *Al Rahma,* lakini wanyonge watakwenda wapi na wanahitaji matibabu, hawana pesa na hali ya maisha tunaijua. Hakuna *lift* mgonjwa utampeleka wapi, utambebaje kama mwili wake ni mzito. Naendelea kusema na nitaendelea kusema mpaka itakapofanikiwa. Narudia tena naendelea kusema na nitalisimamia mpaka litakapofanikiwa, likishakufanikiwa itakuwa basi. Kuna msemo unaosema "hoi hoi nacho kilindo", wanaoumia ni wanyonge. Matokeo yake ndio mtu anapelekwa kule anakatwa mkono.

Kwa hivyo, niiombe serikali, serikali ipo hapa, Waziri wa Fedha na Mipango na tena tunamuamini na ni makini, mimi nikuombe *lift* mpya haifiki shilingi milioni 150, wanyonge wanateseka jamani pale. Mimi nilisema jana, juzi na nitasema kesho na kesho kutwa na nitaendelea kusema, nilishasema nyuma na nyuma huko. Wagonjwa wetu wanaumia jamani, huzuni kubwa. Kuna *CT scan* ile nimepata harufu kidogo kuwa pesa zimeshatolewa

zimeshatengwa za kipimo kile, jitihada za Rais wetu zinakwenda wapi jamani kwenye Sekta ya Afya, hebu tuzienzini. Katika wizara iliyopata bahati hakuna kama Wizara ya Afya, tunachosema basi Mhe. Rais anatekeleza. Kuna huduma za wazazi hapa tulipiga kelele katika Baraza la Wawakilishi lililopita mpaka leo bure. Kipimo cha *CT scan* shilingi 250,000 ukienda hospitali nyengine utakayokwenda, lakini bure. Kwa hivyo, hizo ni juhudi kubwa sana za Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, lakini mengine ya *bulb* hayataki Mhe. Rais, ya sakafu tena kila kitu Mhe. Rais, *no*. Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huo nije kwenye skuli hii kidogo ya Sekondari ya Madungu na Wawi. Hii ni sekta muhimu sana, naiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali nafikiri waziri mwenyewe yupo sijui, na yeye nafikiri hayupo. Kaenda msikitini. Kwa hivyo, niwaombe waangalie kuna changamoto moja kubwa sana ya skuli hizi zimejengwa majuzi, miradi hii inakwama.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Sekta ya Kilimo na Uvuvi. Mimi nasikitika sana, tuna miaka karibu 54 hii wenzetu Mwanza wana ziwa tu na viwanda vitatu vya samaki karibu na sijui kama sio vinne, sisi tuna bahari karibu miaka 54 ya Mapinduzi, itakuwa hadithi hii kama ya watu wa Michamvi na maji.

Mhe. Mwenyekiti, niombe kuna soko lile linalotaka kujengwa pale Malindi kila siku tunaambiwa kesho, kesho kutwa tumeshaambiwa hadi ndani ya chombo hiki, chombo muhimu kabisa kwamba ujenzi huo utaanza kesho, kesho kutwa. Itakuwa hadithi ya mtoto wa kuku hiyo. Mhe. Mwenyekiti, lililokuwa haliwezekani mtuambie ili tusiwape watu tamaa. Mhe.Mwenyekiti, tumeambiwa alikuwepo Said Ali Mbarouk ujenzi utaanza Mji Mkongwe sijui wakaweka pingamizi, pingamizi Mji Mkongwe imeshakwisha. Juzi tulipewa kauli hapa na Mhe. Waziri hakuna kitu.

Mhe. Mwenyekiti, Uvuvi wa Bahari Kuu huu, kuhusu mpunga wa umwagiliaji maji, hakuna kitu ndani ni hadithi tu. Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana na mimi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa mchango wako. Sasa nimpe nafasi Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Khalid Salum Mohamed na yeye aweze kuchangia machache na baadae Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti aweze kuja kutoa maoni yao.

MICHANGO YA MAANDISHI

Mhe. Ali Suleiman Ali: Naipongeza Ripoti ya Kudumu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa mwaka wa Fedha 2017/2018.

Naupongeza Mfuko wa Jimbo, ombi langu fedha za Mfuko zitolewe kwa wakati.

Naipongeza Wizara ya Fedha na Mipango kwa juhudi zao nzuri ya ukusanyaji wa mapato. Aidha, napongeza kwa usimamizi mzuri wa matumizi mazuri ya fedha hizo.

Mwisho naipongeza kamati kwa kazi yake nzuri ya kufuatilia Mfuko wa Jimbo, hongera sana. Naiunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchangia changamoto za Ofisi ya *CAG*.

Kwanza naomba kuchangia suala la changamoto za uhaba wa wafanyakazi wa ofisi hiyo. Suala hili linachangiwa na wizara

kwani ofisi hii taratibu zote za uajiri zimeshakamilika, lakini bado wizara wamezuwia ruhusa ya ajira hiyo. Hivyo, naomba wizara nayo ikamilishe taratibu hizo ili vijana nao ambao mchakato wao wa ajira umeshakamilika waweze kuanza kazi ili changamoto hiyo iweze kuondoka.

Jengine ni changamoto ya wakuu wa idara na taasisi kushindwa kutoa ushirikiano kwa watendaji wa ofisi ya *CAG* kwa kutokuhudhuria katika mikutano ya kufungua au kufunga ukaguzi katika taasisi zao. Jambo ambalo linakwanza utendaji na ucheleweshaji wa kazi za *CAG* .Hivyo, naomba kuwekwe mikakati maalum kwa wakuu watakaoshindwa kutoa ushirikiano na ofisi hii, ili waweze kutekeleza shughuli zao ipasavyo.

Mhe. Ussi Yahya Haji: Awali ya yote naipongeza Kamati ya Kudumu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali, chini ya Mwenyekiwiti wake mahiri Mhe. Miraji Khamis Mussa pamoja na wajumbe wake.
Kazi waliyoifanya ni kubwa na nzuri kupelekea kupata taarifa iliyojaa ukweli na ushauri mzuri kwa Serikali, mimi mchango wangu kwa jumla ni kwamba yale majimbo ambayo hayakutoa ushirikiano wa kuweza kupata taarifa ya matumizi ya fedha za Serikali yasiachwe hivi hivi tu. Serikali ichukue hatua zifaazo.

Mwisho naipongeza Wizara ya Fedha kwa namna ilivyopania, kwa kuongeza makusanyo ya mapato ya Serikali kwa kiwango ambacho kwa miaka mingi hakijapatapo kufikiwa. Kwa hayo machache sana naomba kuunga mkono tarifa hii, ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia Ripoti hii ya Kamati ya Bajeti. Awali ya yote nimshukuru na kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati, Mhe. Mohammed Said Mohammed Mwakilishi makini wa Jimbo la Mpendae. Nimshukuru yeye

pamoja na Kamati yake na Wajumbe wote kwa kazi nzuri na kwa mashirikiano makubwa ambayo tunayo katika kamati na wizara zetu.

Pia nimshukuru na kuwapongeza kwa ripoti ambayo wameleta ripoti ya kina na imeonesha maeneo mbali mbali, imeonesha changamoto ziliopo na pia wametoa maoni yao. Walizungumzia suala la utekelezaji wa bajeti robo ya nne ya mwaka 2016/2017 kwa maana ya Aprili/Juni. Vile vile wamezungumzia utekelezaji wa bajeti kwa robo ya kwanza Julai hadi Septemba 2017/2018 na robo ya pili Oktoba hadi Disemba 2017/2018, pamoja na maeneo mengine ambayo waliyazungumzia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaomba nitoe ufafanuzi katika baadhi ya maeneo, pamoja kwa kwamba majibu tutayaleta katika mwezi wa Septemba, ni kwa sababu wizara zote *almost* zimeguswa na taarifa hii na ripoti hii. Kwa hivyo, kama serikali wizara zetu tutakaa pamoja ili kukusanya maoni na kukusanya majibu juu ya hoja mbali mbali zilizotolewa.

Nataka kutoa ufafanuzi katika baadhi ya maeneo ili *hansard* ikae vizuri kabla hiyo Septemba tutakapokuja na majibu kamili. Kwanza kuna hili suala la malipo ya ujenzi wa jengo la abiria *Terminal II*. Nilisema hapa katika maelezo kwenye jibu kwenye swali, wakati wa maswali na majibu, kwamba mradi ule awamu ya mwanzo ulikuwa na gharama ya jumla ya dola za Kimarekani milioni 70.4, lakini kutokana na mabadiliko ya *design* mradi ule ukahitaji fedha za ziada za dola za Kimarekani milioni 58.

Niliwahi kujibu katika kikao hiki Mhe. Mwenyekiti, kwamba tayari malipo ya mkopo wa mwanzo wa dola za Kimarekani milioni 70.4 yameshafanyika na ni taarifa sahihi yalifanyika mwezi wa Novemba, 2017. Kwa sababu mradi ule ulianza mwaka 2010 na *grace period* tuliopewa ndani ya mradi ule ilikuwa ni ya

miaka saba, kwa hivyo mwaka 2017 tayari mkopo wa mwanzo ulikuwa uanze kulipwa na malipo hayo yameshafanyika.

Kwa hivyo, hili nilitaka nilitolee ufafanuzi kwa sababu ndani ya taarifa hii ukurasa wa 32, imeeleza kwamba malipo hayo yataanza kulipwa mwaka 2019. Kwa hivyo, taarifa sahihi ni kwamba malipo yameshaanza na yameanza mwezi wa Novemba, 2017.

Mhe. Mwenyekiti, pia Waheshimiwa Wajumbe walizungumzia suala la utofauti baina ya mapato tunayokusanya na matumizi yetu, na walionesha hofu kwamba tunakusanya kidogo lakini tunatumia zaidi. Sasa hili nilitolee ufafanuzi Mhe. Mwenyekiti, kwamba ukichukua taarifa ya robo mwaka unaweza kukuta kuna tofauti, kwa sababu kipindi kinakuwa kidogo cha miezi mitatu, lakini ukichukua taarifa ya kipindi kwa mfano cha miezi sita, basi taarifa inabadilika. Kwa sababu ndani ya ukusanyaji wa mapato kuna miezi tunafanya vizuri, lakini kuna miezi *performance* inashuka kidogo kutokana na mwenendo mzima wa hali ya shughuli za kiuchumi katika nchi yetu. Kwa hivyo, hilo sio tatizo ukienda miezi sita taarifa inabadilika na ukienda ya mwaka mzima kwa sababu kipindi ni kirefu pia taarifa itabadilika.

Mhe. Mwenyekiti, nitoe mfano, mapato katika mwezi wa Oktoba/Disemba katika kipindi cha robo hiyo 2017/2018, mapato kama ilivyo taarifa yalikuwa ni bilioni 182.26 ambayo ilikuwa ni wastani wa asilimia 93.73 ya lengo. Lakini matumizi katika kipindi hicho yalikuwa ni bilioni 204.18, sasa ukitizama tofauti ni shilingi bilioni 21.896. Lakini ukichukua kipindi cha miezi sita Julai/Disemba 31, mapato yetu yalikuwa bilioni 460 na matumizi yetu yalikuwa bilioni 463, tofauti imepungua ni bilioni 3. Sasa kutokana na *performance* hii lazima tujipongeze kwa sababu *BoT* wenyewe wanatupongeza sana kwa usimamizi mzuri wa bajeti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hii bilioni 3 wala tusishtuke, hii tofauti huwa inazibwa kwa sababu ya *balance* ambayo tunaamka nayo, kwa sababu ya makusanyo mazuri basi huwa tuna *balance* ambayo inabaki, ile inafidia upungufu uliopo. Kwa hivyo, tuombe kwa Mwenyezi Mungu katika kipindi cha mwaka huu tukija tukizungumzia katika kipindi chote cha miezi 12, basi hapo ndipo tutajua uwezo wetu wa ukusanyaji na *performance* yetu katika ukusanyaji wa mapato, tathmini halisi itapatikana katika kipindi hicho.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala hili la mnara wa Michenzani, mnara wa kumbukumbu. Kama lilivyo jina lake, ule ni mnara wa kumbukumbu ya Mapinduzi matukufu ya Januari 12, 1964. Lakini pamoja na kwamba ni kielelezo cha uhuru na Mapinduzi yetu, pia ilikusudiwa kuwa ni kivutio au kitega uchumi cha kuweza kupata mapato. Lakini mradi ule utakamilika tu, pale na zile *project* nyengine ambazo zimekusudiwa kutekelezwa katika eneo lile litakapokamilika. Serikali ina mpango wa kujenga *Shopping Mall* katika eneo lile na hatua za ujenzi zimeshaanza. Mnara ule utaunganishwa na mradi wa ujenzi wa *Shopping Mall*, utafanyakazi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini katika maeneo yale pia serikali ina mipango mingine mizuri ambayo itakayovuta watu kuja katika eneo lile, Kwahani kuna *process* hizo hizo na serikali itatoa taarifa rasmi wakati utakapofika. Kwa hivyo, eneo lile lote litabadilika sura yake itakuwa ni eneo la kiuchumi, litaweza kuwapatia fursa ya ajira vijana wetu, lakini vile vile mapato katika serikali.

Mhe. Mwenyekiti, jengine la mwisho nilitaka nizungumzie kuhusiana na ununuzi wa meli ya mafuta, limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wajumbe, na wengine wakawa wanafikiria kwa nini tununue meli, pengine fedha zile zingetumika kwa ajili ya utengenezaji wa Bandari ya Mangapwani. Mhe. Mwenyekiti,

niliwahi kujibu hapa kwamba hii ni miradi miwili tofauti, ununuzi wa meli ni mradi wake, lakini na ujenzi wa bandari katika eneo la Mangapwani nao ni mradi mwengine na yote serikali itaitelekeza hatua kwa hatua.

Kwa upande wa meli, kwanza meli ya mafuta ambayo tunayo tayari imeshakuwa chakavu, lakini pia ina mkuku mmoja ambavyo sasa hivi kimataifa meli hizi zinatakiwa ziondoke na ndio maana serikali ikaamua kuja na wazo la kutengeneza meli nyengine ya mafuta itakayochukua nafasi ya MT. Ukombozi. Wazo hili lililetwa hapa Barazani Mhe. Mwenyekiti, kupitia Bajeti ya Serikali ya mwaka 2017/2018 na Waheshimiwa Wajumbe wote tuliunga mkono bajeti ile. Kwa hivyo, suala hili limo ndani ya bajeti hivi sasa ni utekelezaji wake tu. Sasa tunapohoji bajeti ambayo sisi wenyewe tumeipitisha, tumeikubali hapa na tupo kati kati ya utekelezaji wa bajeti hiyo nusu mwaka itashangaza na itawachanganya wananchi. *(Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti, suala la kukwama kwa miradi ya uvuvi ni kweli lakini zipo sababu na sababu hizo zinafanyiwa kazi. Tuna kampuni mbili za uvuvi ambayo moja ilikuwa ni *Holdo* ya China na ya pili ni *Pution Fisheries Company*. Baadhi ya kampuni hizi zinazokuja huwa zinataka kuwekeza katika eneo la maji madogo na kwenye *territorial water* ambayo maeneo haya serikali imeyaweka kwa ajili ya wananchi. Maana yake wakivua katika maeneo ya maji madogo ina maana kwamba watu wadogo wadogo unawaondoa katika hali hiyo. Sasa ukiwaondoa unao mbadala wa kuwapa ajira wananchi hawa. Sasa kinachofanyika ni kuzungumza na makampuni, tunazungumza nao na hivi karibuni tulikwenda China mimi na Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, tulizungumza na Wizara ya Kilimo ya kule, Naibu Waziri wa Kilimo alikuja Dar es Salaam hivi karibuni. Mhe. Waziri wa Kilimo hapa alikwenda akazungumza nae kuna maeneo mengi wamekubaliana.

Mhe. Mwenyekiti, mwanzoni mwa mwezi wa Machi ujumbe maalum utatoka katika Wizara ya Kilimo ya China kuja kuzungumza na wataalam wetu hapa kujua jinsi gani tutakavyokwenda katika masuala ya huo uwekezaji kwenye uvuvi na uvuvi wa bahari kuu. Kwa hivyo, suala hilo linafanyiwa kazi hii miradi haijakwama inafanyiwa kazi lakini inahitaji umakini katika serikali hii inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein ipo makini sana kuhakikisha kwamba miradi inayopitishwa haitoleta athari kwa wananchi wake.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mwisho kabisa ni *Penny Royal*. Suala hili hakuna haja ya kubadilisha sheria Mhe. Mwanasheria Mkuu, kwa sababu sheria tuliyokuwa nayo sasa hivi ingawaje tunataka kuifanyia mapitio na iko katika hatua za mwisho kukamilika, lakini vipo vivutio maalum ukitizama *schedule* kwenye sheria Nam. 11 ya mwaka 2004 kuna miradi iliyopo kwenye *EPZ* na vivutio vyake vimetajwa vizuri kabisa. Lakini pia kuna *schedule* inayozungumzia miradi iliyopo kwenye *prepo* vivutio vipo, lakini pamoja na hayo kifungu cha 20 cha sheria hii kinampa uwezo waziri anayehusika na masuala ya fedha kuweza kukubaliana na mwekezaji yeyote ku-*negotiate* vivutio maalum kwa ajili ya uwekezaji wa mradi.

Lakini hivi karibuni serikali Mhe. Mwenyekiti, imepitisha vivutio maalum kwa miradi ya kimkakati, hivi vivutio vizuri sana na *Penny Royal* ni mradi wa kwanza ambao umepewa fursa ya kutumia vivutio hivyo. Sasa hapa hakuna suala kabisa la kubadilisha sheria ingawaje sheria kwa sababu ya maeneo mengine tunaifanyia mapitio lakini sasa suala lililokuwepo hapa ni utekelezaji, tayari limeshasaini *legal notice* kwa ajili ya vivutio hivyo vya miradi. Kwa hivyo, hakuna suala la sheria au la kukwamisha, lakini lipo suala la utekelezaji wa yale maagizo ambayo sasa yameshatolewa na serikali na hilo tunalisimamia. Mimi mwenyewe na wizara inayohusika na Kilimo na Wizara

yetu ya Fedha na Mipango tutakutana ndani ya wiki ijayo kuhakikisha suala hili la utekelezaji wa mradi wa *Penny Royal* linakamilishwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hii na *inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujaalia mwezi wa Septemba tutatoa majibu kamili. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa ufafanuzi wako pamoja na michango yako. Sasa nampa nafasi Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ili na yeye aweze kuja kutoa hoja na kuchangia maoni.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti) Mhe. Mwenyekiti, niendelee kukushukuru sana lakini kwa jioni hii ya leo nimshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetujaalia kufika hapa tukiwa na hali ya uzima na afya njema. Pili, niwashukuru wajumbe wote wale waliochangia na waliokuwa hawakuchangia, wale waliokuwa hawakuchangia nilikuwa nikiwaona wametulia kabisa kusikiliza hoja ambazo zilikuwa zikitolewa na wajumbe, lakini na hoja ambayo Mhe. Waziri wa Fedha ameitoa. Kwa aina ya kipekee nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa ufafanuzi mzuri sana alioutoa, lakini hata na mimi nitatoa baadhi ya ufafanuzi uliolengwa katika kamati yangu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kwa heshima kubwa sana nitaje wale wajumbe ambao walichangia moja kwa moja lakini baadae nitawataja waliochangia kwa maandishi. Wajumbe wote waliochangia hoja yangu ni wajumbe 33, wajumbe 17 walichangia moja kwa moja na wajumbe 16 walichangia kwa maandishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima sasa naomba niwataje wale waliochangia moja kwa moja.

1) Mhe. Shehe Hamad Matar
2) Mhe. Asha Abdalla Mussa
3) Mhe. Bahati Khamis Kombo
4) Mhe. Abdalla Ali Kombo
5) Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
6) Mhe. Miraji Khamis Mussa
7) Mhe. Suleiman Sarahan Said
8) Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil
9) Mhe. Hamza Hassan Juma
10) Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
11) Mhe. Rashid Makame Shamsi
12) Mhe. Omar Seid Abeid
13) Mhe. Suleiman Makame Ali
14) Mhe. Simai Mohammed Said
15) Mhe. Jaku Hashim Ayoub
16) Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango

Lakini na wale waliochangia kwa maandishi naomba sasa niwataje nao ni:

1) Mhe. Nassor Salim Ali
2) Mhe. Ussi Yahya Haji
3) Mhe. Tatu Mohammed Ussi
4) Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
5) Mhe. Moh'd Mgaza Jecha
6) Mhe. Yussuf Hassan Iddi
7) Mhe. Ali Suleiman Ali
8) Mhe. Mussa Ali Mussa
9) Mhe. Shaib Said Ali
10) Mhe. Said Omar Said
11) Mhe. Hidaya Ali Makame

12) Mhe. Masoud Abrahman Masoud
13) Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
14) Mhe. Juma Ali Khatib
15) Mhe. Abdalla Maulid Diwani
16) Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa

Mhe. Mwenyekiti, wote waliochangia walichangia hoja hii kwa umakini mkubwa sana, wengi waliochangia walichangia michango yao ya kujenga sana lakini hata kuishauri serikali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wajumbe hawa walishauri serikali katika maeneo mbali mbali ikiwemo *ZIPA*, walilipigia kelele sana suala kubwa la *One Stop Centre*. Lakini Mhe. Simai Mohammed Said alizungumzia kuhusu SMZ *office* kwa kuwa ni kiunganishi chetu kikubwa cha mabalozi na taasisi za nje, lakini kuonesha jinsi gani sasa serikali iwaongezee nguvu, lakini vile vile iongeze na wafanyakazi wa pale kwa sababu Serikali ya Jamhuri ya Muungano imehamia Dodoma pale patakuwa hapana kiunganishi kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil yeye alizungumzia kwa hisia kubwa sana *Amani Industrial Park* jinsi gani unaweza ukakuza uchumi lakini leo vipi imekuwa, lakini jinsi gani inaweza ika-*create* ajira za wananchi mbali mbali pale. Nikushukuru sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hamza Hassan Juma alizungumza habari ya uvuvi na hasa kuitaja Hondom, nataka niiweke *hansard* sawa wale wataalam wa serikali hawakwenda Korea, wale walikwenda Mauritania na vielelezo vingi ambavyo tulikuwa navyo tatizo kubwa serikali haijibu barua inapoletewa. Sasa nataka kusema tu utawala bora huu tunaokwenda nao tuanze kuweka mipango imara au tuunde sheria, serikali inapoletewa barua na leo bahati kubwa

sana Makamo wa Pili wa Rais Kiongozi wa Shughuli za serikali hapa Barazani yupo, serikali yako inapopelekewa barua inachelewa kujibu kwa taasisi nyingi.

Tukuombe na tukushauri sana kama katiba inavyotwambia, wanapopelekewa barua wajibu hata kama hawataki waseme hili hatutaki au hili hatuliwezi huo ndio utawala bora, utawala bora tusiwe kwenye mambo mengine. Ukiambiwa kitu unatakitaka sema nakitaka, sikitaki serikali iseme haikitaki haiwezekani tuwe wakweli na tumtangulize Mwenyezi Mungu katika kazi zetu.

Suala la uwekezaji katika nchi hii limekuwa tete sana. Mhe. Jaku Hashim Ayoub alizungumza kwa hisia kubwa sana na utete wake inakuja sisi bado hatujajua nini tunachokitaka, tumekuwa kama tunafunga Ramadhan kila kitu tunacholetewa tunakitaka lakini hatuna maamuzi ya kweli kwenye serikali. Tuwaombe sana serikali tumtangulize Mwenyezi Mungu mbele lakini tuone jinsi gani tunavyofaidika na uwekezaji unapokuja katika nchi yetu.
Mhe. Mwenyekiti, hili la *Penny Royal* limeelezwa wazi kuna hekta 441 kulikuwa na makubaliano pale, lakini tumshukuru Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango sana kwa sababu amesema limemalizika. Mimi nilikuwa niishauri serikali na Kiongozi wa Shughuli za Serikali hapa Barazani yupo leo, nilitaka nimwambie mapema kuwa akae na taasisi zote kuona mradi huu umekwama wapi. Labda angekaa na Mhe. Mwanasheria Mkuu msomi sana na ninamuamini katika maisha yangu. Lakini angekaa na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, akakaa na Wizara ya Fedha na Mipango kuona mambo yote yanatatuka. Tumpongeze sana Dkt. Khalid Salum Mohamed kwa kazi kubwa anayoifanya na tunatarajia mambo haya yatatatuka na tuone miradi hii inawanufaisha wananchi wa Kijini Matemwe lakini hasa na Zanzibar kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, mengine yalikuwa mengi ya jumla jumla, lakini kubwa jengine zaidi nitaje jambo moja. Mimi yangu kwa upande wangu mengi nilishayasema lakini hii ya upimaji wa ardhi nimejaribu kuangalia bajeti ya mipango miji, mipango miji ya serikali hii katika kifungu (h), (n), (o), 10, 20, 30, 10, 20, 10.3 usimamizi na upimaji wa ardhi imetiliwa milioni mia tano na arubaini na moja laki saba na thamanini na saba kwa kipindi hiki. Kwa mipango miji lazima pesa hizi ni kidgo sana kwa sababu tumejumuisha kitu kimoja kimoja. Tuiombe sana serikali kuweza kuiongezea bajeti idara hii ili tuwe na *master plan* na tuone kila kitu tumekipanga vizuri. Tunapokosa *master plan* ndio hata hizi *sewage system* zinakuwa mbovu sana, tunapata *break down* ya *cholera* na mambo mengine kwa sababu kila pahala tumekuwa tunajenga. Tuiombe sana serikali kudumisha mipango miji.

Mhe. Mwenyekiti, lakini yangu kabla sijahitimisha hoja yangu hii ya leo naomba nimpe taarifa Mhe. Suleiman Sarahan Said. Mhe. Mwenyekiti, jana wakati nikirudisha Baraza kwenye *track* kutumia kanuni ya 23 na Mwenyekiti akakubali akamuamrisha Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, atoe hoja tena arudi kwenye *track* kwa kutumia kanuni ile. Mhe. Suleiman Sarahan Said alisema sijui ninalolifanya kwa sababu nilikataa hoja. Sasa nataka nimwambie nilikuwa najua nini ninachokifanya kwa sababu baada ya kurudi kwenye *track* ikatolewa hoja na kwenye hoja kuna demokrasia kukubali au kukataaa, mimi nilikataa kwa sababu nilitumia demokrasia yangu. Kwa hivyo niwaombe tu Waheshimiwa Wajumbe kanuni na katiba ya nchi hii ndio tu ambazo tunapaswa kuzitumia ndani ya Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada yamaelezo mazuri ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, baada ya maelezo mazuri ya Wajumbe wote na michango yao mizuri kwa serikali, naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa ninaomba niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Mwenyekiti, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sina budi niwashukuru sana kwa utulivu wenu na usikivu na kuweza kupitisha ripoti hii. Zaidi nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na kumuomba watendaji wake waifanyie kazi ripoti hii kwa vile ni ripoti mama sana katika mwelekeo wa nchi yetu. Lakini zaidi niwashukuru wajumbe kwa michango yao. Baada ya hapo naliakhirisha Baraza hili kwa siku ya leo hadi Jumatatu saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1.15 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 26/2/2018 saa 3:00 asubuhi)